**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

# RIPOTI YA JUMLA YA UKAGUZI WA UFANISI NA UKAGUZI MAALUMU KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 MACHI, 2018

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**Machi 2018**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

**Dira**

Kuwa kituo cha ubora cha ukaguzi wa hesabu katika sekta za umma

**Dhamiri**

**Kutoa huduma za ukaguzi wa hesabu zenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.**

**Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:**

**Uadilifu**

**Kuwa taasisi adilifu inayotoa huduma bila upendeleo.**

**Weledi**

**Tunalenga kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu kwa kuzingatia taratibu bora**

**Uaminifu**

**Tunahakikisha tuna na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.**

**Mkazo kwa watu**

**Tunalenga kufanikisha matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia wateja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.**

**Uvumbuzi**

**Kuwa taasisi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya taasisi**

**Matumizi bora ya rasilimali**

**Kuwa taasisi inayothamini na kutumia kwa umakini mkubwa rasilimali za umma ilizokabidhiwa.**

| | JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA<br><br>OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI | |
|---|---|---|

Mtaa wa Samora , S.L.P. 9080, Dar es Salaam
Simu ya Upepo : “Ukaguzi", Simu: 255(022)2115157/8, Nukushi: 255(022)2117527,BaruaPepe: ocag@nao.go.tz,
Tovuti : www.nao.go.tz

Kwa majibu tafadhali taja Kumb. Na.FA 27/249/33/2017/2018 27 Machi, 2018

Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
Barabara ya Barack Obama Na 1,
**11400 Dar es salaam.**

**Yah: KUWASILISHA RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU RIPOTI KUMI ZA UKAGUZI WA UFANISI**

Kwa mujibu wa ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa mwaka 2005) na kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti yangu ya tisa ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu.

Ripoti hii inajumuisha ripoti kumi za Ukaguzi wa Ufanisi ambazo zinahusu Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zilizowasilishwa Bungeni katika nyakati tofauti.

Ninawasilisha.

Prof. Mussa Juma Assad
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**YALIYOMO**


YALIYOMO ........ I

**ORODHA YA MAJEDWALI ........ III**

**ORODHA YA PICHA ........ IV**

**DIBAJI ........ V**

**SHUKRANI ........ VII**

**MUHTASARI ........ VIII**

**SURA YA KWANZA ........ 2**

**UTANGULIZI ........ 2**

**1.1.** USULI WA UKAGUZI ........ 2
**1.2.** LENGO NA MAWANDA YA RIPOTI ........ 4
**1.3.** MCHAKATO WA UTHIBITISHO WA TAKWIMU ........ 6
**1.4.** MUUNDO WA RIPOTI ........ 6

**SURA YA PILI ........ 7**

**USIMAMIZI WA MASUALA YA USALAMA TANZANIA ........ 7**

**2.1** USULI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA USALAMA ........ 7
**2.2** MIKAKATI YA USALAMA NJIA YA MAJI NA BARABARANI ........ 7
**2.3** MIKAKATI YA USALAMA WA CHAKULA ........ 8
**2.4** MIKAKATI YA USALAMA MAHALA PA KAZI ........ 9
**2.5** MIKAKATI YA UPANGAJI MIJI NA UDHIBITI WA MAENEO YA WAZI ........ 10
**2.6** MIKAKATI YA TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA KWA MIRADI YA MAENDELEO ........ 11

**SURA YA TATU ........ 13**

**USALAMA KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI ........ 13**

**3.1** UTANGULIZI ........ 13
**3.2** TATHMINI ISIYOJITOSHELEZA YA MAHITAJI YA USAFIRI WA BARABARANI NA MAJINI ........ 13
**3.3** UKAGUZI WA MAGARI NA MELI KUTOZINGATIA MASUALA HATARISHI ........ 15
**3.4** UTEKELEZAJI USIOJITOSHELEZA WA MKAKATI WA MAFUNZO YA USALAMA BARABARANI ........ 18
**3.5** USIMAMIZI DUNI WA SHERIA NA VIWANGO VYA USALAMA ........ 19
**3.6** KUTOTEKELEZWA KIKAMILIFU KWA MIPANGO YA KUANGALIA USALAMA ........ 23
**3.7** URATIBU DHAIFU BAINA YA WADAU WAKUU WA USAFIRI WA BARABARA ........ 24
**3.8** UFUATILIAJI NA TATHMINI ISIYOTOSHELEZA YA USALAMA KATIKA SEKTA YA USAFIRISHAJI ........ 25

**SURA YA NNE ........ 28**

**4.1** UTANGULIZI ........ 28
**4.2** MPANGOKAZI USIOJITOSHELEZA WA SHUGHULI ZINAZOHUSIANA NA USALAMA WA CHAKULA ........ 28
**4.3** MAZINGIRA HATARISHI YA UANDAAJI WA CHAKULA (NYAMA) ........ 30
**4.4** UKAGUZI HAFIFU WA VIWANDA VINAVYOSINDIKA CHAKULA, MAHALI PA KUSINDIKIA CHAKULA, NA SEHEMU CHAKULA KINAPOINGIZWA NCHINI ........ 32
**4.5** URATIBU HAFIFU WA WADAU WANAOJISHUGHULISHA NA USALAMA WA CHAKULA ........ 34
**4.6** UTOAJI TAARIFA USIOJITOSHELEZA WA MATOKEO YA USIMAMIZI WA USALAMA WA CHAKULA ........ 37
**4.7** UFUATILIAJI NA TATHMINI ISIYOJITOSHELEZA YA UKAGUZI WA CHAKULA ........ 37

SURA YA TANO ........ 40
USALAMA KATIKA MAKAZI YA WATU ........ 40
5.1 UTANGULIZI ........ 40
5.2 MIPANGO ISIYOJITOSHELEZA YA SHUGHULI ZA KUDHIBITI USALAMA KATIKA MAKAZI YA WATU ........ 40
5.3 UTEKELEZAJI DUNI WA SHUGHULI ZA KUBORESHA USALAMA KATIKA MAKAZI YA WATU ........ 43
5.4 USAJILI USIOTOSHELEZA ........ 47
SURA YA SITA ........ 54
HITIMISHO ........ 54
6.1 UTANGULIZI ........ 54
6.2 HITIMISHO LA JUMLA ........ 54
6.3 HITIMISHO MAALUMU ........ 54
SURA YA SABA ........ 60
MAPENDEKEZO ........ 60
7.1 UTANGULIZI ........ 60
7.2 MAPENDEKEZO YA KUBERESHA USALAMA KATIKA SEKTA YA USAFIRISHAJI ........ 60
7.3 MAPENDEKEZO YA KUBORESHA UDHIBITI WA USALAMA WA CHAKULA NCHINI ........ 60
7.4 MAPANDEKEZO YA KUBORESHA USALAMA KATIKA MAKAZI YA WATU ........ 61
MAREJELEO ........ 62
VIAMBATISHO ........ 64

## ORODHA YA MAJEDWALI


| | | |
|---|---|---|
| Jedwali 1.1: | Masuala ya usalama yaliyoangaliwa ikilinganishwa na jukumu la serikali | 3 |
| Jedwali 3.1 | Asilimia ya meli ndogo zisizokuwepo katika mpango ya ufuatiliaji | 10 |
| Jedwali 3.2 | Idadi ya meli ndogo ikilinganishwa na idadi ya wachunguzi | 11 |
| Jedwali 3.3 | Amri za Kusimamishwa uendeshaji meli na adhabu kwa wakiukaji wa Viwango vya Usalama | 14 |
| Jedwali 3.4 | Idadi ya ukiukwaji wa viwango vya Usalama | 15 |
| Jedwali 4.1 | Mazingira yasiyosalama yaliyobainika katika machinjio yaliyotembelewa | 21 |
| Jedwali 5.1 | Mlinganisho wa Mgawanyo wa Wakaguzi Kulingana na matukio ya moto katika mikoa mitano iliyotembelewa | 31 |
| Jedwali 5.2 | Fedha zilizotengwa kwa ajili ya ukaguzi wa majengo na ufuatiliaji wa vikosi vya zimamoto | 31 |
| Jedwali 5.3 | Asilimia ya majengo ya Umma yaliyo kaguliwa na bado yana Mapungufu | 33 |

**ORODHA YA PICHA**

| | | |
|---|---|---|
| Picha 3.1 | Alama ya mwisho wa mwendo wa kilomita 50 kwa saa iliyopauka imewekwa katika barabara mpya | 14 |
| Picha 3.2 | Alama ya barabara na kingoreli chakavu | 17 |

# DIBAJI

Nina furaha kuwasilisha Ripoti yangu ya Tisa ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu. Ripoti hii ya jumla inahusu ripoti kumi za Ukaguzi wa Ufanisi kwa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, na Mamlaka zenye wajibu wa kushughulikia masuala ya usalama kwa wafanyakazi pamoja na watumiaji wa huduma zinazotolewa na Serikali.

Ripoti hii inalenga kutoa taarifa kwa wadau (wabunge, maofisa wa serikali kuu na serikali za mitaa, wanahabari, wafadhili, na asasi za kijamii na zisizo za kiserikali kuhusiana na matokeo ya ukaguzi yaliyopo kwenye ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu zilizofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kufikia Mwezi Machi 2018. Ufafanuzi wa kina kuhusiana na taarifa zilizoandikwa kwa kifupi unapatikana kwenye ripoti husika za ukaguzi ambazo zilikabidhiwa kwa Maofisa Masuhuli (Makatibu Wakuu) wa wizara husika.

Ripoti hii imekabidhiwa kwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa mujibu wa ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Vifungu 34 (1) na (2) vya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008.

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama inavyorekebishwa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila taarifa aliyotoa kwa mujibu wa Ibara ndogo (2) ya Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Rais atamwelekeza waziri husika kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kabla ya siku saba kupita toka kikao cha kwanza cha Bunge kuanza. Ibara hiyohiyo inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge iwapo Rais kwa sababu zozote zile atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama sheria inavyotaka.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008, kumeimarisha uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu unatarajiwa kuniwezesha kupata taarifa na kuwa na udhibiti muhimu wa rasilimali zote zilizopo kwa ajili ya Ofisi ikiwa ni pamoja na rasilimaliwatu na fedha, ambazo zitaiwezesha Ofisi yangu kufanya kazi bila kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote zikiwemo zile ninazozikagua.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kunipa mamlaka ya kufanya Ukaguzi wa Ufanisi, Ukaguzi wa Utambuzi, Ukaguzi wa Mazingira, na Ukaguzi Maalumu. Aina hizi za ukaguzi ni zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha kama ambavyo tumekuwa tukifanya kwa miaka mingi.

Kimsingi, taarifa hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na matumizi sahihi na uwajibikaji, uwazi, na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma hususani katika masuala ya usalama kwenye huduma ya usafirishaji, makazi, mchakato, na uingizaji wa chakula nchini.

Lengo kuu la kufanya aina hizi za ukaguzi ni kuangalia iwapo rasilimali zilizotengwa zimetumika kwa ufanisi kwa kuzingatia uwekevu, tija, na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa.

Ni vizuri kufahamu kwamba wakati Ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa ripoti ya utendaji wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma kulingana na sheria katika taratibu zilizopo, wajibu wa kuhakikisha uwepo wa ufanisi, uwekevu, na tija katika matumizi ya rasilimali za umma ni wa Maofisa Masuhuli. Wakati huohuo, ni wajibu wa Maofisa masuhuli kuhakikisha uchunguzi unafanyika na mapendekezo niliyoyatoa yanatekelezwa kikamilifu.

Ni matarajio ya Bunge kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ataandaa taarifa za fedha kuhusu usimamizi wa rasilimali za umma ndani ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma kuhusiana na tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa programu mbalimbali za Serikali. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma. Kwa jinsi hiyo, Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, na Ofisi yangu kwa pamoja zina mchango mkubwa kwa Bunge katika kujenga imani kwa umma katika usimamizi wa rasilimali za umma. Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora kwa rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya wabunge na umma kwa ujumla, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta ya umma. Aidha, Ofisi yangu inahakikisha ukaguzi wake unalenga na kuyapa kipaumbele maeneo muhimu yanayochangia au kutarajiwa kuchangia maendeleo ya sekta ya umma hasa usimamizi wa masuala yahusuyo usalama wa wanachi wanapopata huduma mbalimbali. Hivyo, kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Ninapenda kutambua weledi na dhamira ya wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi, mishahara duni, na wakati mwingine kufanya kazi kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi.

Ninatarajia kuwa Bunge, vyombo vya habari na jamii kwa ujumla itaona taarifa hii ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa rasilimali za umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo, nitafurahi kupata mapendekezo ya jinsi ya kuboresha taarifa kama hii kwa siku zijazo.



Prof. Mussa Juma Assad,
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,**
**28 Machl 2018**

## SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioweka mazingira wezeshi kwangu kuweza kutimiza wajibu wangu wa kikatiba. Ninapenda kumshukuru kila mfanyakazi katika Ofisi yangu kwa jitihada zake ambazo zimeniwezesha kutoa ripoti kwa wakati. Ninalazimika kuishukuru familia yangu na za wafanyakazi katika Ofisi yangu kwa uvumilivu wao waliouonesha wakati wa kipindi chote cha kutimiza wajibu huu wa kikatiba.

Ninapenda kuishukuru Serikali na Bunge letu tukufu kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, shukrani za pekee ziende kwa jumuiya ya wafadhili hasa Ofisi ya Ukaguzi ya Uholanzi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden, Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani, Benki ya Dunia kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha na wote waliotutakia mema ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika Ofisi yangu. Mchango wao katika kuimarisha ujuzi wa wafanyakazi, mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano, na nyenzo mbalimbali umechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio yetu.

Halikadhalika, ninapenda kuwashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na Maofisa Masuhuli wa taasisi nilizozikagua kwa kutoa mchango mkubwa na taarifa muhimu zilizohitajika kwa ajili ya maandalizi ya ripoti mahususi za ukaguzi wa ufanisi ambazo ndizo zimewezesha uandaaji wa ripoti hii ya jumla.

Shukrani za kipekee ziende kwa jamii ya wanataaluma na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Chuo Kikuu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, wataalamu wa kujitegemea, na maofisa wastaafu wa serikali kwa michango yao ambayo iliboresha ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi kupitia maoni na uhakiki walioufanya katika rasimu za ripoti.

Ninapenda pia kuishukuru Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu ambayo ripoti hii pamoja na ripoti mahususi zitafikishwa kwa ajili ya uchunguzi, majadiliano, na kutoa maelezo yake. Tunatarajia kuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu itatupa maboresho na mwelekeo utakaotokana na mjadala wa ripoti hizi.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru Maofisa Masuhuli na watumishi wote wa taasisi za umma Tanzania nzima. Ninatambua pia mchango wa walipakodi ambao ripoti hii tunaitoa kwao. Mwenyezi Mungu awabariki nyote kadri mnavyojitoa katika kusimamia uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma nchini.

# MUHTASARI

## Utangulizi

Ukaguzi wa Ufanisi unalenga kuboresha muundo wa uwajibikaji na utendaji wa taasisi za serikali. Pia, unatoa tathmini huru ya namna ambavyo taasisi hizo zinatumia rasilimali katika kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia uwekevu, tija, na ufanisi. Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, namba 11 ya mwaka 2008 inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kufanya ukaguzi wa ufanisi kwenye sekta ya umma.

Taarifa hii ya jumla ya ukaguzi inaelezea mapungufu ya jumla yaliyobainika, hitimisho, pamoja na mapendekezo katika Ripoti kumi (10) za Ukaguzi wa Ufanisi uliofanyika mwaka 2014 na 2017 unaohusu usimamizi wa samani za barabarani; ukaguzi wa vyombo usafiri wa majini; ukaguzi magari na udhibiti wa mwendokasi; ukaguzi wa chakula na ufuatiliaji wa mitambo ya usindikaji na maeneo ya kuingizia chakula nchini; Udhibiti katika uzalishaji uchakataji wa nyama; Usimamizi wa usalama dhidi ya majanga ya moto katika majengo ya umma; tathmini za athari za mazingira katika maendeleo ya miradi; usimamizi wa mipango-miji; usimamizi wa mifumo ya udhibiti wa mazingira katika sekta ya madini; na kaguzi za ufuatiliaji.

Kwa ujumla, ripoti hii inalenga kuwasaidia wabunge, serikali, vyombo vya habari, umma, pamoja na wadau kufanya maamuzi sahihi ili kutekeleza pendekezo la kubana matumizi, na kuongeza tija na ufanisi kwenye kulinda usalama na afya kwa watumiaji mbalimbali wa huduma. Hata hivyo, ripoti hii haijalenga kuwa mbadala wa ripoti zingine kumi za ukaguzi zilizotajwa ambazo zilifanyika mwaka wa fedha uliopita. Hivyo basi, msomaji wa ripoti hii anashauriwa kuzingatia zaidi ripoti husika.

**Matokeo ya Ukaguzi**
Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi uliofanyika:

***Utekelezaji usiojitosheleza wa Mipango na Mpango Mkakati wa Mafunzo ya Usalama***

Wakala wa Barabara na Jeshi la Polisi Tanzania hawakuweza kutekeleza mipango na mpango mkakati wa mafunzo ya usalama kwa wafanyakazi wao. Pia, Jeshi la Polisi Tanzania halikuunganisha mpango mkakati wa mafunzo wa usalama na mpango wa rasilimaliwatu kwa ajili ya mafunzo ya kupeleka polisi kwenye maeneo yaliyotambuliwa kuwa na matukio mengi ya ajali.

TANROAD ilifanya mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wake katika ukaguzi wa usalama barabarani. Hata hivyo, wafanyakazi hao hawakupatiwa mafunzo ya kuweza kushughulikia au kusimamia masuala ya usalama. Wakala wa Barabara ilitoa kipaumbele cha chini katika utekelezaji wa mipango ya shughuli zilizowekwa kuhusu usalama. Hii ilisababisha samani za barabarani kutofanyiwa matengenezo au kutowekwa kabisa barabarani.

Kwa mfano, iligundulika kwamba Wizara ya ujenzi iliipa Wakala wa Barabara gawiwo la **shilingi millioni 310** kwa ajili ya uwekaji wa samani au alama za watu wenye ulemavu. Hata hivyo, Wakala wa Barabara haikuweka samani hizo kama ilivyotarajiwa.

Vilevile, utekelezaji wa mipango ya uchunguzi na ukaguzi wa meli ndogo haikufanyika ipasavyo. Ilivyogundulika kwamba asilimia 85 ya meli ndogo hazikufanyiwa uchunguzi na ukaguzi. Hii ni kwa sababu uhalisia wa shughuli za ukaguzi haukuwa sawa na mkataba wa makubaliano ya utekelezaji ya mwaka na pia haikulingana na mipango yao ya kaguzi. Hii ni kwa sababu Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini haikuanzisha kanzidata ya meli kubwa na meli ndogo.

***Usimamizi Duni wa Sheria na Viwango vya Barabarani na majini***

Uwekaji wa alama za barabarani, michoro na kingo za barabara kwa kiwango duni na kutokarabati samani za usalama barabarani zilizochakaa, zilizofutika, na zilizotelekezwa na Wakala wa Barabara ni ishara ya usimamizi duni wa sheria na viwango vya usalama.

Vilevile, kutokidhi viwango na sheria za usalama kwa vyombo vya usafiri wa majini kulisababishwa na usimamizi duni wa sheria ya viwango na usalama . Katika mwaka wa fedha 2011/2012 na 2015/2016 asilimia 1.85 tu ya wakiukaji sheria waliwajibishwa au waliadhibiwa. Kwa kuongezea, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini haikutoa amri ya kusimamisha wamiliki wa vyombo vya baharini waliokiuka sheria na viwango kwa meli zilizokuwa na kiwango cha chini cha kukidhi vigezo vya usalama. Badala yake, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilitoa vibali vya uendeshaji wa meli ambazo ni hatarishi kwa usalama wa watumiaji ambazo hazikukidhi vigezo. Hii

ilisababishwa na kiwango cha kutokidhi vigezo kwa asilimia 52 mwaka wa fedha 2011/2012 na asilimia 68 kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Ongezeko hili la kutokidhi vigezo lilisababishwa na kupungua kwa kaguzi za meli

Pia, kulikuwa na utekelezaji duni wa sheria kwa wakiukaji sheria za barabarani kwa faini zisizotija. Kwa mfano, idadi ya watuhumiwa 6,026 sawa na Shilingi milioni 338 kwa mwaka 2017 hazikukusanywa. Hii inaonesha kwamba kuna usimamizi duni wa sheria za barabarani.

### *Ufuatiliaji na Tathmini Isiyojitosheleza ya Usalama katika Sekta ya Usafirishaji*

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mwasiliano haikufuatilia na kutathmini utendaji wa usalama katika sekta ya uchukuziikiwa ni pamoja na mashirika na mamalaka zake. Vivo hivyo, Wizara ya Ujenzi, Wakala wa Barabara , Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Usafiri wa Nchikavu na Majini haikufuatilia na kutathmini utendaji wake katika kutekeleza shughuli zao kwa kulinganisha na malengo waliyojiwekea. Hii ilisababishwa na upungufu wa rasilimaliwatu wa kushughulikia na masuala ya usalama; ukosefu wa mipango ya ufuatiliaji na tathmini masuala ya usalama; ukosefu wa viashiria muhimu vya kiutendaji ili kupunguza ajali; na vipaumbele vya chini vilivyowekwa na wadau wakuu wa usalama katika sekta ya uchukuzi.

Vilevile Wakala wa Barabara haukuwasilisha ripoti za robo mwaka kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya uchunguzi na kaguzi za meli kama ilivyoelekezwa katika Mkataba wa Utendaji kati yao. Hii ilisababishwa na Wizara ya Ujenzi kutoweka kipaumbele shughuli za ufuatiliaji na tathmini kama ilivyoonesha wazi kuwa mwaka wa fedha 2012/2013 hakukuwa na fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya masuala ya usalama.

### *Hatua za Udhibiti wa Usalama wa Chakula katika Usindikaji na Uagizaji Usio na Ufanisi*

Hakuna uhakika kwamba chakula kinachosindikwa kwenye mitambio na kinachoagizwa kutoka nje na kusambazwa kwa wananchi ni salama kwa matumizi ya binadamu. Wizara ya Afya, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Serikali za mitaa na wakala zao ikiwa pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa na Shirika la Viwango Tanzania hazikutekeleza majukumu yao kuhakikisha usalama wa chakula kinachosambazwa kwa umma.

Hii ni kwa sababu Wizara zina upungufu wa hatua madhubuti za udhibiti wa usalama na ubora wa chakula nchini. Shughuli za kusimamia ukaguzi wa chakula, usajili wa mitambo ya kusindika chakulana usafirishaji chakula haukufanyika kwa ufanisi ili kuuhakikishia umma umadhubuti wao katika udhibiti wa hatari ya chakula vinavyozalishwa ndani ya nchi na vile vinavyoingizwa kutoka nje.

***Shughuli za Ukaguzi Ili Kusimamia Usalama wa Chakula Hazikufanyika kwa Ufanisi***

Mipango ya ukaguzi iliyoandaliwa na Wizara ya Afya; Wizara ya Kilimo na Mifugo; na TAMISEMI; na mashirika yake ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania pamoja na Shirika la Viwango la Tanzania viashiria vya hatari ya viwango vya bidhaa, malengo na ukaguzi wa ufanisi wa bidhaa za chakula na usindikaji wa chakula. Matokeo yake, Ukaguzi uliofanyika haukuwa na ufanisi kwa kuwa haukulenga vihatarishi vya bidhaa ya chakula na usindikaji wa bidhaa za vya chakula viwandani. Kwa hiyo, kulikuwa na hatari ya kuzalisha chakula kisichofaa na hivyo kupungua kwa uwezo wa matumizi ya kibinadamu yasiyowekewa tahadhari na hatua za haraka.

Ukaguzi usiojitosheleza ulisababishwa na upungufu wa rasilimaliwatu na fedha zisizotosheleza kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya shughuli za ukaguzi na ukosefu wa mipango ya kutosha kwa ajili ya ukaguzi unaozingatia vihatarishi wa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje. Sababu nyingine ni mtazamo usio wazi ambao umejikita katika ukaguzi wa shughuli zao, upungufu wa wakaguzi katika vituo vya kuhifadhia bidhaa, makontena yaliyoingizwa ikilinganishwa na idadi ya nyaraka au mizigo iliyokaguliwa kwa siku na usimamizi dhaifu wa sheria na kanuni za usalama wa madawa na bidhaa za chakula katika viwango vinavyohitajika.

Bandari ya kuingizia bidhaa kutoka nje ikiwa ni pamoja na didhaa za chakula haikukaguliwa kiufanisi. kwa hiyo. Hali hii huhatarisha au ni hatari kubwa kuagiza bidhaa za chakula kutoka nje zikiwa chini ya kiwango kinachotakiwa na kuhatarisha afya za watu kama wangetumia au wangekula chakula cha chini ya kiwango.

Kuhusu nyama, shughuli za ukaguzi wa nyama zilizofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka ya Chakula na Dawa na mamlaka za serikali za Mitaa hazikuwa za ufanisi na pia hazikuelekeza ufanisi katika tatizo la usafi wa mazingira ya machinjio na usindikaji wa nyama. Hii inaonesha kuwepo kwa wachinjaji wa nyama na machinjio yasiyosajiliwa ambazo hutumia magari madogo ambayo si usafi.

Vilevile, Mamlaka ya Chakula na Dawa , haikukagua vihatarishi katika mitambo yote ya usindikaji wa chakula ambayo huzalisha bidhaa nyingi hatarishi za chakula kama vile samaki, bidhaa za samaki, maziwa na didhaa za maziwa, nyama na bidhaa za nyama, pamoja na mboga zilizosindikwa, viungo vya chakula, na bidhaa za viungo vya chakula. Hakukuwa na ukaguzi wa ufanisi pia katika bidhaa za vyakula kama vile chokoleti, viambata vya mboga kama vile sosi za chili, asisi za vinywaji na biskuti na viungo vya chakula vinavyoingizwa kutoka nje. Hali hii inahatarisha afya watu wengi wenye magonjwa hatarishi yanayosababishwa na magonjwa yasiyoambukizwa ikiwa ni ukiukaji wa matumizi ya bidhaa za chakula ambazo hazikukaguliwa katika viwango vilivyowekwa.

Aidha ,uhakiki wa nyama haukufanywa vizuri kwa sababu kuna upungufu wa asilimia 40 ya wakaguzi wa nyama. Waliopo wanaelemewa na kazi ya ukaguzi ina walemea kutokana na ukubwa wa kazi. Wakaguzi wa nyama walikuwa wanatakiwa kukagua wanyama 100 hadi 150 kwa siku hali iliyoathiri ufanisi na usahihi wa ukaguzi. Kwa masuala ya nyama, miundombinu duni, machinjio mabovu, na vifaa duni vya kuchinjia pamoja na ujuzi usiofaa vilichangia ubora usiofaa wa nyama iliyozalishwa.

***Usajili wa Mitambo na Vifaa vya Usindikaji Chakula Havifanyiki ki ufanisi na kimadhubuti***

Usalama wa chakula ndani ya nchi haukuhakikishwa kwa sababu asilimia kubwa ya mitambo inayosindika chakula, majengo, na vifaa vya usafirishaji havikusajiliwa. Hii ni kwa sababu hakukuwa na hali ya usafi na usalama muhimu unaouhakikishia umma usalama wa chakula vilivyozalishwa viwandani. Pia, hakukuwa na viwango vya usafi na udumishaji usafi. Pia, mitambo yote ya kusindikia nyama au chakula, majengo, miundombinu na vituo vya usafirishaji wa chakula viliandikishwa vichache. Kwa uchache huo wasajili hawakuweza pia kudumisha hali ya usafi wa mazingira katika maeneo yake.

***Ukosefu wa Utaratibu wa Ufanisi na Mfumo wa Wadau Waliohusika Kutekeleza Usalama wa Chakula***

Ushauri wa wadau wanaohusika katika ukaguzi wa chakula katika mitambo ya usindikaji wa chakula na milango ya bandari kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Viwango ya Tanzania, Tume ya Ushindani wa Kibiashara, mamlaka ya serikali za mitaa, Bodi ya Boti, Bodi ya Sukari na Wizara ya Mifugo na Uvuvi hawakuunganisha uratibu wa pamoja wa kutosha. Hii ilisabishwa na mipango isiyofaa kukosekana kwa ukaguzi unaozingatia hatari au vihatarishi.

***Ufuatiliaji na Tathmini ya Shughuli za Usalama wa Chakula hazifanyi vya kutosha***

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Afya, Sekta ya Biashara na Uwekezaji, na serikali za mitaaa hazifanyi ufuatiliaji na tathmini ya kutosha ya shughuli za usalama wa chakula na mitambo ya kusindika chakula, miundombinu na vituo vya kusafirishia ndani na nje ya nchi ambyo ni bandari. Wizara hizo hazikuweka mipango madhubuti wa utekelezaji na utendaji wa Mamlaka za serikali za mitaa, mamlaka ya Chakula na Dawa na Shirika la viwango Ofisi ya Viwango Tanzania juu ya utekelezaji wa masuala ya usalama wa chakula kupitia shughuli zao za ukaguzi.

VileVile, Wizara hazielewi taratibu na utendaji, viashiria vya utendaji muhimu kwa kutathmini shughuli za utekelezaji kwa kuiangalia kwa karibu zaidi Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania kwa karibu Zaidi na Halmashauri hasa katika usimamizi wa usalama wa chakula hasa mitambo ya usindikaji wa chakula, miundombinu na maeneo ya kuingizia chakula nchini.

Aidha, Wizara haijaweza kupima ufanisi wa zana na leseni zilizosajiliwa katika kukabiliana na masuala ya usalama wa chakula na mitambo ya kusindika bidhaa za chakula, vifaa vya kuchinjia, na masuala ya milango ya bandari ya kuingizia bidhaa za chakula. Uwajibikaji usiojitosheleza wa Wizara katika uratibu kati ya Wizara tatu kuhusu majukumu yao katika utekelezaji na usimamiaji wa sheria zinazoongoza usalama wa chakula ni sababu kuu ya uratibu mbovu. Matokeo yake, Wizara hazitambui kiwango ambacho wamefikia malengo yao ya kuzuia madhara ya chakula na vihatarishi vinavyoweza kusababisha afya hatarishi ili kuboresha usalama na ustawi wa jamii au umma.

*Utekelezaji Duni wa Hatua za Usalama katika Majengo ya Umma*

Majengo mengi yanayotumiwa na umma yako katika hatari kwa kuwa kuna utekelezaji hafifu wa mahitaji ya usalama wa moto na Kikosi cha Zima Moto na Uokoaji chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Hii ni kwa sababu ya udhaifu uliobainika kutokana na ukaguzi wa majengo ya umma.

Vilevile, hii ni kutokana na ukweli kwamba vyombo vyenye mamlaka havijafanikiwa kupanga na kufuatilia shughuli zao ili kuhakikisha kwamba majengo yote ya umma yanachunguzwa, yanakaguliwa kwa ubora wa juu na ukaguzi unazingatia maeneo hatarishi na matokeo ya ukaguzi yakanawasilishwa kwa mmiliki wa jengo la umma kwa hatua za kurekebisha. Hali hii imefanya majengo mengi ya umma kuwa si salama kwa matumizi ya umma kwakuwa hayakuwa na viwango na vigezo vilivyohitajika kwa usalama dhidi ya moto.

*Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Si Rafiki kwa usalama wa Makazi ya Watu*

Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira wana usimamizi dhaifu na usiojitosheleza katika utekelezaji wa mahitaji ya usimamizi wa mazingira ndani ya nchi. Miradi ya maendeleo iliyokubalika kutekelezwa imekuwa vyanzo vya mafuriko na uchafuzi wa mazingira. Hii husasbabisha maeneo kuwa si salama kwa binadamu kuishi au kutumia baadhi ya bidhaa kama vile maji.

Hali hii imesababishwa na ukosefu wa ushirikishwaji wa wadau husika wakati wa upitiaji wa taarifa za miradi na taarifa za athari za Mazingira na ukaguzi usiofaa wa Taarifa za Mazingira kwa kuzingatia masuala muhimu kama vile kiwango cha hatari ya uchafuzi wa mazingira, aina au msisitizo wa sheria ya mazingira, ukiukaji na uharibifu wa eneo la kijiografia, na makazi ya binadamu.

**Udhibiti Usiojitosheleza wa Matumizi ya Ardhi**

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais TAMISEMI haijaweza kudhibiti matumizi ya ardhi kwa sababu kuna miji mingi ambayo haijajengwa kiutaratibu kwa sababu ya ukosefu wa mipango-miji.Katika mji uliopangiliwa, maeneo mengi ya wazi hayajasajiliwa na utekelezaji wake ni

kinyume na mipango iliyowekwa. Kwa mfano, matumizi ya ardhi yalibadilishwa kutoka maeneo ya viwanda na kuwa makazi ya watu au kiunyume chake.

Hii ilisababishwa hasa na utekelezaji dhaifu wa mamlaka ya mipango-miji na upungufu wa wafanyakazi. Udhibiti usiojitosheleza wa matumizi ya ardhi ulisababishwa makazi kuwa chini ya kiwango na miundombinu duni kutokana na kutowepo kwa miundombinu ya majitaka, mifereji ya maji ya mvua. Hali hii inahatarisha uwepo wa mafuriko na hivyo kuwa na ongezeko la magonjwa ya mara kwa mara ya kipindupindu na kuhara wakati wa mvua.

**Hitimisho**

Kwa ujumla, ukaguzi umetambua jitihada za serikali katika kutekeleza hatua za usalama na udhibiti katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, ripoti zimethibitisha kuwa serikali haijaweza kusimamia kwa ufanisi shughuli za utekelezaji wa hatua za usalama na udhibiti katika usafiri, makazi ya watu pamoja na usindikaji wa chakula na uagizaji wa chakula. Udhaifu umebainika katika mipango, utekelezaji, usajili, ujenzi wa uwezo, ukaguzi, uratibu, utoaji wa taarifa, mawasiliano, na ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zinazohusiana na usalama wa chakula, uchukuzi na makazi ya watu nchini.

**Mapendekezo ya Ukaguzi**

Ili kukabiliana na mapungufu yaliyobainika, Ofisi ya Waziri Mkuu inapaswa kuhakikisha wizara na mamlaka au wakala zinawajibika katika usalama katika maeneo matatu ambayo ni uchukuzi chakula na makazi ya watu. Miongoni mwa mapendekezo muhimu katika maeneo yote matatu yalitokana na kutokuwa na matumizi ya njia ya vihatarishi katika ukaguzi wa usalama, uratibu, ufuatiliaji, na ugawaji wa rasilimali katika utekelezaji na usimamizi wa shughuli za usalama. Kwa kifupi Ofisi ya Waziri Mkuu inapaswa:

1. Kutumia dhana ya mbinu msingi ya viashiria hatarishi katika kupanga na kufanya ukaguzi ambao utashughulikia masuala ya usalama katika uchukuzi, chakula na makazi ya watu.

2. Kuanzisha na kuimarisha utaratibu wa ufanisi ambao utahakikisha kupeana na kubadilishana taarifa kati ya wadau wote muhimu wanaohusika na usimamizi na utendaji wa usalama katika eneo la uchukuzi, chakula, na makazi ya watu.

3. Kuanzisha viashiria muhimu vya utendaji wa ufuatiliaji na tathmini ambavyo vitatumika kupima utendaji wa wadau wote wanaohusika na usalama kulingana na mamlaka zao walizowekewa kwa mujibu wa sheria.

4. Kuendeleza au kuanzisha mfumo wa kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali zote kama wafanyakazi, vifaa, na fedha za kutosha kushughulikia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za usalama. Rasilimali zinapaswa

kufanyiwa uchambuzi na usawa wa mgawanyo ikilinganishwa na uzito wa kazi yenyewe katika shughuli za usimamizi wa masuala ya usalama.

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1. Usuli wa Ukaguzi

Usimamizi wa usalama wa umma unahusisha uratibu na utawala wa rasilimali zinazotolewa kwa ajili ya kuhakikisha usalama katika bidhaa na huduma zinazotolewa. Serikali inahusika na kuweka viwango, kufanya ukaguzi, kuhakikisha kuwa viwango vinafikiwa, na kudumisha mpango wa utekelezaji madhubuti wa kukabiliana na wasiozingatia viwango. Kuna aina mbalimbali za vihatarishi vinavyoweza kuhatarisha maisha ya watu kutokana na shughuli za kijamii au kiuchumi. Shughuli hizi ni pamoja na ujenzi, usindikaji wa chakula, usafiri, na nyingine.

Hatari inayohusishwa na shughuli hizi ni pamoja na magonjwa, kuzuka kwa moto, ajali za barabarani, na za usafiri wa njia ya maji, na matukio mengine ambayo yanaweza kusababisha vifo, majeraha, au kupoteza mali. Serikali ina wajibu wa kulinda wananchi wake ikiwa ni pamoja na kutekeleza sheria na viwango vya usalama ili kupunguza hatari kwa kiwango cha kukubalika. Sehemu hii ya ripoti inaelezea hatari za usalama zinazoweza kutokea zinazohusiana na uchukuzi, usindikaji wa chakula na shughuli za makazi ya binadamu nchini.

Inakadiriwa kuwa mwaka 2014 kuliripotiwa matukio ya ajali barabarani milioni 1.2 ikilinganishwa na matukio milioni 0.7 mwaka 2013 nchini Tanzania. Hii ni ongezeko la asilimia 64. Matukio haya ya ajalibarabarani yalisababisha vifo vya watu 4,000 na majeruhi 15,000 nchini kote. Utafiti unaonesha kwamba asilimia 80 ya ajali za barabarani zinahusishwa na makosa ya kibinadamu. Hata hivyo, barabara na samani za barabara kukosa matengenezo kwa wakati, na ukosefu au upungufu wa alama za barabarani ni miongoni mwa sababu zinazochangia kutokea kwa ajali za barabarani.

Vilevile, katika usafiri wa njia ya maji, udhibiti wa usalama ni muhimu ili kulinda maisha ya watu, kupunguza majeruhi, na upotevu wa mali (mizigo) kwa kupunguza idadi ya ajali.

Nchini Tanzania, kumekuwa na malalamiko ya kuwepo kwa bidhaa za chakula ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu. Miongoni mwa mifano ya hivi karibuni ni maziwa ya watoto wachanga, nyama zisizofaa kutoka kwenye machinjio, pamoja na kurejeshwa kwa samaki walioingizwa nchini.[1]. Katika siku za hivi karibuni, kumekuwa

[1]http://www.mwananchi.co.tz/habari/Kitaifa/Nyama-hatari-yauzwa-nchini//1597296/2066152//145stot/-/index .html

na matukio ya bidhaa za chakula kuzuiliwa na vyombo husika kwa kuwa hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Aidha, karibu asilimia 80 ya machinjio hayafanyi kazi katika mazingira ya usafi na hayana miundombinu ambayo inaruhusu ukaguzi wa wanyama ufanyike kwa ufanisi. Kwa hiyo, kuna hatari kubwa ya kusambaza nyama isiyo salama kwa walaji.

Majanga ya moto ni miongoni mwa changamoto za usalama katika maeneo ya makazi. Tanzania imeshuhudia matukio ya moto katika majengo ya umma ambayo yalisababisha upotevu wa maisha na mali. Matukio kama haya ni pamoja na tukio la moto katika mabweni katika Sekondari ya Idodi mwezi Agosti 2009 na kujirudia mwezi Machi 2015; kuungua kwa ofisi za bohar la Dawa (MSD) Tanga mwezi Julai 2014; kuungua kwa Machinga Complex Dar es Salaam mnamo Novemba 2014, kuungua kwa ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo Julai 2015[2]. Zaidi ya hayo, utafiti[3] umeonesha kwamba majengo mengi ya umma yana uhaba wa watumishi wenye ujuzi na vifaa haba vya kukabiliana na au kijikinga dhidi ya moto.

Kwa upande mwingine, kumekuwa na matukio la ajali na hatari nyingine ambazo zimeathiri wafanyakazi wengi duniani kote ikiwa ni pamoja na Tanzania. Mwaka 2003 na 2004, idadi ya ajali kazini zilizoripotiwa Tanzania Bara zilikuwa 1,692 na 1,889 kwa mfuatano huo na jumla ya shilingi milioni 668.5 zilitumika kulipa fidia waathirika wa ajali zitokanazo na kazi.

Kuhusu masuala ya usalama wa mazingira, kulikuwa na hatari ya serikali kuruhusu miradi ya maendeleo kutekelezwa katika maeneo nyeti kwa uhifadhi wa mazingira bila kuchukua hatua zinazofaa za kupunguza athari. Hapa ilionekana kwamba taasisi muhimu zinazohusika na kusimamia mchakato wa tathmini ya mazingira hazikufanya kazi zake vizuri licha ya kupokea ruzuku kutoka serikalini.

Kutokana na umuhimu wa usalama katika maisha na ustawi wa kijamii na kiuchumi kwa Watanzania pamoja na tishio linalohusishwa na matatizo yaliyotajwa, Ofisi yaTaifa ya Ukaguzi iliamua kuelezea suala la usalama katika ripoti ya mwaka huu. Lengo la ripoti hasa ni kuchambua masuala ya usalama yaliyopatikana katika ripoti za ukaguzi wa ufanisi, kutoa picha kamili ya nini kinachofanyika na serikali wakati wa kukabiliana na masuala ya usalama hasa katika uchukuzi, usindikaji, na uingizaji wa chakula nchini, pamoja na makazi ya watu.

---

[2] Gazeti la Majira la Machi 10, 2015 (Idodi), gazeti la Mtanzania la Julai 25, 2014 (MSD), Gazeti la Mwananchi la Novemba 16, 2014 (Machinga Complex) na Gazeti la Tanzania Daima la 17 Julai 2015 (Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo).

[3] Utafiti kuhusu ya Uelewa wa Mipango ya Usalama wa Moto kwa Watumiaji na Wafanyakazi wa Maduka ya Ununuzi : Uchunguzi wa Kituo cha Mlimani na Ubora wa Dar es Salaam na Kikwasi G. J (2015)

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya Ukaguzi wa Ufanisi kupitia Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 28 cha Sheria hii kinasema “Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa lengo la kuthibitisha uwekevu, tija, na ufanisi katika matumizi ya fedha au rasilimali za taasisi ya umma, anaweza kukagua, kuchunguza, na kutoa ripoti kadri atakavyoona inafaa kuhusu:

(a) Matumizi ya fedha na rasilimali za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa, na mamlaka nyingine za serikali;
(b) Utekelezaji wa majukumu ya maofisa masuhuli, wakuu wa idara, na wakuu wa taasisi mbalimbali za umma;
(c) Utekelezaji wa matakwa ya sheria ya mazingira, kanuni, na sera za ndani za mazingira na viwango.

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu waheshimiwa wabunge, vyombo vya habari, umma, pamoja na wadau wengine ili waweze kutoa maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija, na ufanisi katika shughuli za serikali. Ripoti hii inatoa muhtasari wa mambo mbalimbali yaliyoonekana katika kaguzi za ufanisi zilizofanyika dhidi ya mambo yaliyotarajiwa kwa kuzingatia hatua zilizopangwa kuchukuliwa, utekelezaji wa hatua zilizopangwa, udhibiti wa vihatarishi, ufuatiliaji, na tathmini ya shughuli za udhibiti wa masuala ya usalama kwa watoaji na watumiaji wa huduma.

## 1.2. Lengo na mawanda ya ripoti

Ripoti hii imelenga kuonesha mapungufu yaliyooneshwa katika ripoti za ukaguzi wa ufanisi pamoja na hatua ambazo serikali imezichukua katika kusimamia masuala ya usalama kwa wananchi.

### 1.2.1 Lengo la ripoti

Lengo kuu lilikuwa ni kupima kiwango ambacho Serikali kupitia Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa inaimarisha utekelezaji wa mfumo wa usimamizi wa masuala ya usalama katika kupunguza athari. Ripoti inalenga hasa:

**a)** kutathmini iwapo taasisi za serikali zina mipango madhubuti ya kupunguza athari zinazoweza kutokea;
**b)** kutambua kiwango ambacho taasisi za serikali zinafanya ukaguzi, kutoa ripoti, kutoa adhabu, na kufuatilia utekelezaji wa mfumo wa usimamizi wa usalama katika shughuli za serikali za utoaji huduma;
**c)** kutambua iwapo kuna uratibu mzuri wa taasisi za serikali katika utekelezaji wa mfumo wa usimamizi wa usalama; na
**d)** kutathmini kiwango ambacho vyombo vya serikali kuu vinafuatilia utendaji wa mashirika yaliyo chini yake na vilevile mashirika na Mamlaka za Serikali za Mitaa hufuatilia utendaji wao wenyewe katika masuala ya salama.

### 1.2.2 Mawanda ya ripoti

Ripoti hii imelenga kuchambua masuala ya usalama katika ripoti nane(8) za ukaguzi wa ufanisi zilizochapishwa kati ya 2015 na 2017 na ripoti mbili za kufuatilia. Ripoti hizi zote zililenga kuangalia jinsi serikali inavyosimamia maeneo makuu matatu, yaani usalama katika chakula, usafiri, na makazi. Maelezo maalumu kuhusu mawanda ya kaguzi za ufanisi yametolewa katika ***Kiambatisho 2***. Muhtasari wa masuala ya usalama kwa kila eneo ni kama ilivyoelezwa katika Jedwali 1.1.

**Jedwali 1.1: Masuala ya usalama yaliyoangaliwa ikilinganishwa na jukumu la serikali**

| Huduma | Suala la Usalama | Jukumu la serikali kuhakikisha usalama |
|---|---|---|
| Usafiri | Usalama barabarani | Ukaguzi wa magari, utekelezaji wa kikomo cha kasi ya mwendo, usimamiaji wa samani za barabara |
| | Usalama katika usafiri wa majini | Ukaguzi wa vyombo vya maji, utekelezaji wa viwango vya usalama |
| Chakula | Usalama katika mchakato wa chakula | Udhibiti katika uzalishaji na uchakataji wa nyama; ukaguzi na ufuatiliaji, usindikaji na uingizaji wa chakula nchini. |
| | Usalama katika bidhaa zilizoingizwa nchini | Ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa |
| Makazi ya watu | Usalama katika majengo ya umma | Utekelezaji wa matakwa ya usalama dhidi ya moto katika majengo ya umma |
| | Usalama katika maeneo ya kazi | Usimamizi wa ukaguzi wa usalama katika maeneo ya kazi |
| | Usalama wa mazingira | Utekelezaji wa shughuli za matumizi ya ardhi, mipango-miji, maeneo ya wazi, na tathmini ya athari ya mazingira |

Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi na Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi

Ukaguzi umefanyika kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ufanisi. Viwango hivyo vinataka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kupanga na kukagua ili kupata ushahidi wa kutosha ambao utakuwa kigezo cha kutolea taarifa mapungufu yaliyoonekana na kutoa hitimisho kwa kuzingatia lengo la ukaguzi husika.

## 1.3. Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu

Wizara, Idara, Mashirika, Taasisi, na Wakala mbalimbali za Serikali zilizokaguliwa zilipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao juu ya matokeo ya ukaguzi na kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika rasimu ya taarifa ya kaguzi za ufanisi zilizohusika katika ripoti hii.

## 1.4. Muundo wa ripoti

Ripoti hii ya jumla imeundwa katika sura saba. Sura zilizobakia ni kama ifuatavyo: *Sura ya Pili* inaelezea usimamizi wa masuala ya usalama nchini Tanzania; *Sura ya Tatu* inaongelea masuala ya usalama katika sekta ya usafirishaji; *Sura ya Nne* inaelezea usalama wa chakula; *Sura ya Tano* inaelezea masuala ya usalama katika makazi; *Sura ya Sita* inalenga hitimisho; na *Sura ya Saba* inajielekeza katika kutoa mapendekezo.

**SURA YA PILI**

**USIMAMIZI WA MASUALA YA USALAMA TANZANIA**

## 2.1 Usuli wa Mfumo wa Usimamizi wa Usalama

Mfumo wa Usimamizi wa Masuala ya Usalama ni mpangilio wa mbinu za kusimamia usalama, ikijumuisha miundo muhimu ya kiutawala katika taasisi, dhana ya uwajibikaji, sera, na taratibu zinazoongoza shughuli nzima za kiusalama[4]. Jambo muhimu kwa mfumo wowote wa Usimamizi wa Usalama ni kutoa mbinu zinazowezesha kupunguza kiwango cha hatari zinazoweza kuathiri usalama ili kufikia kiwango cha hatari za kiusalama kinachokubalika kitalaamu.

## 2.2 Mikakati ya Usalama Njia ya maji na Barabarani

Katika usafiri wa majini, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini (Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini) inapewa mamlaka na Sheria ya Udhibiti wa Vyombo vya Majini Na. 21 ya mwaka 2003 ili kuhakikisha viwango vya usalama vilivyowekwa na sheria hii vinatekelezwa. Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini inawajibika kufanya ukaguzi kwa madhumuni ya kutoa hati kama vile uhalali wa usalama wa vyombo vya bahari kufavya shughuli za usafirishaji. Ukaguzi huo unafanywa kwa kutumia mwongozo unaoonesha mchakato wa ukaguzi husika. Kuna mwongozo maalumu wa ukaguzi kwa meli ndogo na meli kubwa. Miongozo yote inaonesha vipengele mbalimbali vinavyotakiwa kuzingatiwa wakati wa ukaguzi. Kimsingi, meli inatakiwa ifanyiwe ukaguzi wa awali kabla ya haijaanza kutoa huduma; ukaguzi unatakiwa kufanywa mara moja kila baada ya miezi 12; na kaguzi za ziada, kama hitaji linatokea.

Mkakati mkubwa wa serikali uliokuwa ukikaguliwa ni ukaguzi wa usalama barabarani na usimamizi wa samani na alama za barabarani. Ukaguzi wa usalama barabarani ulizingatia mwenendo wa dereva kwani tafiti zinaonesha kuwa asilimia 76 ya ajali za barabarani zinatokana na sababu za kibinadamu ikiwemo mienendo na tabia za maadereva wa vyomo vya moto barabarani. Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi Tanzania linawajibika kutekeleza sheria na kanuni za usalama barabarani kama zilivyoelezwa katika Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973.

Chini ya usimamizi wa alama na samani za barabarani, Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 na Sera ya Taifa ya Usalama wa Barabara ya mwaka 2009 iliamuru Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano kufanya ukaguzi wa usalama wa barabara katika kila hatua ya

[4] Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga (ICAO) Mwongozo wa Usimamizi wa Usalama wa Anga, 2013

utakelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara. Ukaguzi wa usalama barabarani unaangalia zaidi "kufaa kwa barabara kulingana na lengo la matumizi" badala ya kuzingatia viwango vya kiufundi[5]. Hii inamaanisha haja ya kuhakikisha kuwa mradi husika unakidhi mahitaji ya usalama ya kila mtumiaji wa barabara. Tahadhari maalumu hutolewa kwa watumiaji wa barabara ambao wako hatarini zaidi kwa kuwa uzoefu unaonesha kwamba wasanifu wa barabara huzingatia kwa kiasi kikubwa mahitaji ya vyombo vya moto kama vile magari.

TANROADS pia inatakiwa kufanya matengenezo ya kawaida (matengenezoya mara kwa mara) na ya vipindi maalumu pamoja na maboresho ya papo kwa hapo ya barabara kwa lengo la kuhakikisha kuwa barabara hizo ni salama kwa watumiaji wote. Matengenezo ya kawaida, pamoja na mambo mengine, yanashughulikia matengenezo ya alama na samani za barabara. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano kupitia TANROADS imeanzisha mfumo wa usimamizi wa matengenezo ya barabara. Mfumo huu unahusisha kanzidata za barabara za TANROADS inayotumika kupanga mipango/programu, mikataba ya ufuatiliaji, na utoaji wa ripoti za matenegenzo ya barabara.

### 2.3 Mikakati ya Usalama wa Chakula

Kazi ya kuhakikisha kuwa chakula kinachozalishwa au kuagizwa kutoka nje ya nchi ni salama kwa mutumizi ya binadamu ipo chini ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania. Ili kutekeleza mamlaka yake, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzaniainafanya ukaguzi wa bidhaa za chakula, majengo ya kuzalishia au kuhifadhia chakula, na hatua zinazohusiana na kuuza na kuagiza chakula kutoka nje ya nchi. Kwa upande mwingine, mfumo wa kusimamia ukaguzi wa bidhaa zilizoagizwa ikiwa ni pamoja na chakula pia unafanywa na Shiriaka la Viwango Tanzania.

Ndani ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania, ukaguzi unafanywa na Idara ya Usalama wa Chakula ambayo ina vitengo vitatu, ambavyo ni Ukaguzi na Utekelezaji wa Sheria za Chakula, Upimaji na Usajili ya Chakula, na Uchambuzi wa Vihatari vya Usalama wa Chakula. Kuna waratibu wa kanda wa serikali za mitaa wanaopatikana katika kanda tano ambao wanaripoti kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia Mkurugenzi wa Usalama wa Chakula. Waratibu hawa wana wajibu wa kufanya ukaguzi wa kawaida, ukaguzi wa dharura, na ukaguzi unaotokana na viashiria vya hatari za kiusalama. Kanuni za uchambuzi wa viashiria vya hatari na udhibiti wa usalama katika maeneo muhimu umetumiwa katika kusimamia usalama wa chakula.

---

[5] Wizara ya Miundombinu ; Mwongozo wa Ukaguzi wa Usalama wa Barabara, 2009

Kanuni hizi zinaonesha viashiria vya hatari na hatua za udhibiti ili kuhakikisha chakula ni salama kwa matumizi ya binadamu.

Mwongozo wa Ukaguzi wa Chakula wa mwaka 2009 unaitaka Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania kuyagawa machinjio yote ya wanyama katika makundi kulingana na viashiria vya hatari na kuweka kipaumbele katika kukagua machinjio hayo kwa kuzingatia viashiria hivyo vya hatari. Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania ilitoa mwongozo wenye orodha ya vigezo vya ukaguzi kwa ajili ya ukaguzi wa machinjio ya ng'ombe, kondoo, na mbuzi kupitia waraka wake wenye kumbukumbu Na. F13/DFS/FRA/GL/002 ili kuwasaidia wakaguzi wa machanjio kukagua majengo ya machinjio na kupendekeza hatua zitakazochukuliwa katika kuyasajili.

Zaidi ya hayo, mamlaka za serikali za mitaa kupitia wakaguzi wake wa nyama pia hufanya ukaguzi wa kila siku wa wanyama, nyama, machinjio, na magari ya kusafirishia nyama ili kuhakikisha kwamba nyama iliyoingizwa sokoni ni salama. Mkaguzi wa nyama anapaswa kutekeleza matakwa yote ya kisheria yanayohusiana na ukaguzi wa nyama kabla na baada ya uchinjaji na katika usafirishaji wa nyama.

Ukaguzi wa chakula kinachoagizwa kutoka nje ya nchi hufanyika kwa kutumia wakaguzi ambao amaa ni maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania au mtumishi yeyote wa umma kama ilivyooneshwa katika Sheria ya Udhibiti wa Viwango namba 2 ya mwaka 2009, sehemu ya 23(1). Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Viwango namba 2 ya mwaka 2009 sehemu ya 4 (1), chakula kilichoagizwa kinapaswa kukaguliwa katika kila mlango wa mpaka kilipoingilia kabla ya kuingia katika soko la Tanzania. Ili kuwezesha ukaguzi wa bidhaa, kulikuwa na mkataba wa makubaliano uliotumiwa katika masuala ya forodha yanayohusisha taasisi mbalimbali za serikali ikiwa ni pamoja na Shirika la Viwango Tanzania na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania

## 2.4 Mikakati ya Usalama Mahala pa Kazi

Kulingana na Sheria ya Afya ya Usalama Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003, Wakaguzi wa Usalama na Afya mahali pa kazi wanatakiwa kukagua maeneo yote ya kazi ili kujua iwapo sheria na viwango vya afya na usalama mahali pa kazi vinazingatiwa. Kuna aina mbili kuu za ukaguzi wa mahali pa kazi unaofanywa na Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, yaani ukaguzi wa wa jumla na ukaguzi maalumu.

Ukaguzi wa jumla unahusu ukaguzi wenye mawanda mapana ambapo mkaguzi anaainisha masuala mbalimbali ya afya na usalama mahali pa kazi. Ukaguzi maalumu hufanyika baada ya ukaguzi wa jumla ambapo mkaguzi anafanya ukaguzi juu ya suala maalumu kama vile

umeme, mitambo, na usafi wa viwanda wakati wa kutembelea mahali pa kazi. Sheria pia inahitaji Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi kusajili maeneo yote ya kazi nchini na kutoa mafunzo ya afya na usalama kazini.

Kuhusiana na usalama katika masuala ya moto, wamiliki na watumiaji wa majengo ya umma lazima wahakikishe vifaa vinavyohitajika kudhibiti majanha ya moto vinawekwa na kufanyiwa matengenezo yanayotakiwa. Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kupitia kifungu cha 15 (3) (b) cha Sheria ya Moto na Uokoaji namba 14 ya Mwaka 2007 linatakiwa kufanya ukaguzi kwa ajili ya kuhakikisha wadau wote wanatimiza mahitaji ya usalama ndani ya maeneo yao. Pia, kufungu cha 15 (3) (c) cha Sheria hiyo inaeleza kwamba Jeshi litatoa vyeti kwa wale waliotimiza matakwa ya Sheria ya Sheria ya Moto na Uokoaji. Kwa mujibu wa Kanuni za Moto na Uokoaji (ukaguzi wa usalama na utoaji vyeti vya ukaguzi) ya mwaka 2008, kanuni ya 12, cheti kitabaki halali kwa mwaka mmoja tangu ukaguzi ulipofanyika.

Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kinapaswa kufanya ukaguzi wa kawaida na wa kustukiza ili kutathmini kiwango cha usalama kuhusiana na hatari ya majanga ya moto katika majengo ya umma. Kikosi kinatakiwa kuchunguza na kubaini iwapo kuna vifaa vya kuzimia moto, vifaa hivyo vimewekwa vyema, vifaa vinakarabatiwa, na vinafanya kazi vizuri, na kisha kutoa ripoti ya ukaguzi kwa wamiliki wa majengo ya umma kwa ajili ya kuboresha.

## 2.5 Mikakati ya Upangaji Miji na Udhibiti wa Maeneo ya Wazi

Mchakato wa mipango-miji inahusisha mipango ya eneo, utekelezaji wake, pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango hiyo. Sehemu ya 79 (1) ya Sheria ya Mipango-Miji Namba 8 ya Mwaka 2007 inazitaka mamlaka za mipango, katika kipindi cha muda wa miezi kumi na mbili, kuwasilisha katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ripoti ya maendeleo na tathmini ya uendeshaji na utekelezaji wa mipango yao.

Kwa mujibu wa Waraka Namba 1 wa Mwaka 2006 wenye kumbukumbu Na. CA.91/329/01.C uliotolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi, mamlaka za mipango zinatakiwa kufanya ukaguzi wa kawaida na kuchukua hatua stahiki kila wakati kunapofanyika uendelezaji ambao haufuati taratibu za maeneo ya wazi ya umma yaliyopangwa.

Vivyo hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango-Miji Namba 8 ya Mwaka 2007, mamlaka za mipango zina uwezo wa kuhifadhi na kudumisha ardhi yote iliyopangwa kama maeneo ya wazi na bustani

ambazo zinaendana na mipango iliyoidhinishwa. Ili kuhakikisha sheria zinafuatwa, mamlaka za mipango zina wajibu wa kufanya ukaguzi katika maeneo ya wazi yaliyopangwa ndani ya mamlaka zao na kuchukua hatua zinazostahiki dhidi ya wavamizi.

Maofisa watendaji wa kata wanawajibika kusimamia na kulinda maeneo ya wazi ya umma yaliyo katika maeneo ya mamlaka zao na kutoa taarifa za shughuli zozote za uendelezaji wa maeneo husika zinazofanywa na wavamizi kwa mamlaka za mipango.

Ofisi ya Rais – TAMISEMI ina jukumu la kufuatilia utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kupata taarifa kupitia utekelezaji wa maagizo na miongozo iliyotolewa. Zaidi ya hayo, Ofisi hii inaratibu kwa kuwasiliana na wadau wakubwa wa mipango ya maendeleo ya miji ambayo inapaswa kutekelezwa na mamlaka husika za mipango.

## 2.6 Mikakati ya Tathmini ya Athari za Mazingira kwa Miradi ya Maendeleo

Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira linatakiwa kuhakikisha kwamba tathmini ya athari za mazingira katika miradi ya maendeleo zinafanywa na kupitiwa kwa ufanisi kabla ya Waziri wa Mazingira hajatoa idhini kwa mwenye mradi. Kwa kufanya hivyo, halmashauri zina jukumu la kufuatilia mchakato mzima wa tathmini ya athari za mazingira na utolewaji wa idhini yake. Mchakato unahusisha hatua nane ambazo ni usajili, uchunguzi wa awali, mawanda, tathmini ya athari, kupitia ukaguzi husika, usikilizaji wa maoni ya umma, maamuzi ya mazingira, na rufaa.

Kulingana na ISO 1900, Baraza la Taifa la Mazingira linatarajiwa kuanzisha malengo na mchakato unaohitajika kutoa matokeo kulingana na Tathmini ya Athari za Mazingira na Kanuni za Ukaguzi za Mwaka 2005. Kwa kutumia kanuni hii, Baraza la Taifa la Mazingira linatakiwa kuandikisha miradi ya maendeleo inayohitaji tathmini ya athari za mazingira kulingana na asili ya mradi au shughuli inayotaka kufanyika. Baraza la Taifa la Mazingira lina jukumu la kuchunguza miradi kwa lengo la kuamua iwapo tathmini ya athari za mazingira inahitajika au la.

Baraza la Taifa la Mazingira linatakiwa pia kuwasilisha nakala za taarifa ya tathmini ya mazingira na taarifa ya ukaguzi wa mazingira kwa zizara na taasisi yoyote ya umma na inapaswa kuujulisha na kualika umma kutoa maoni yake ndani ya siku kumi na nne (14) toka siku taarifa ya athari za maazingira ilipopokelewa.

Zaidi ya hayo, Baraza la Taifa la Mazingira linatakiwa kuanzisha Kamati za Kisekta za Ushauri wa Kitaalamu katika ngazi ya kitaifa na

ikiwa inafaa katika ngazi ya mamlaka za serikali za mitaa ili kushauri juu ya upitiaji wa taarifa zinazohusiana na tathmini za athari za mazingira. Kwa mujibu wa Waraka wa Marekebisho ya Sera ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1998, taasisi za serikali zinatakiwa kuwasiliana na mamlaka za serikali za mitaaa kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kuhusiana na hili, Kitengo cha Uratibu wa Kisekta katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI kinatakiwa kuwa kiungo kati ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu, na mamlaka za serikali za mitaa.

Pia, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inalitaka Baraza la Taifa la Mazingira kuwasilisha nakala za mwisho za Taarifa ya Tathmini ya Mazingira/Taarifa ya Ukaguzi wa Mazingira katika wizara za kisekta na halmashauri husika ambako mradi unapatikana ili taarifa hizi zitumiwe kama chombo cha kufanyia kazi za kuhakikisha sheria za usimamizi wa mazingira zinatekelezwa. Zaidi ya hayo, kifungu cha 182 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kinamtaka waziri anayehusika na mazingira kumteua kwa maandishi mfanyakazi yeyote wa halmashauri, wizara, au taasisi nyingine yoyote ya umma ama kwa jina au ofisi kuwa mkaguzi wa mazingira.

## SURA YA TATU

## USALAMA KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI

### 3.1 Utangulizi

Usalama katika sekta ya uchukuzi ni suala linalohitaji tahadhari kubwa ili kupunguza ajali na hivyo kuokoa maisha ya watu. Sura hii inajumuisha masuala yaliyoripotiwa na ripoti za ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa usalama wa uchukuzi katika sekta ya usafiri wa barabarani na majini.

Ripoti tatu za ukaguzi wa ufanisi wa utendaji zimetumika katika kuelezea masuala ya kushughulikia usalama wa usafiri wa barabarani na majini. Ripoti hizi za ukaguzi wa ufanisi ni:

- Ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa samani za barabarani;
- Ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa majini;
- Ripoti ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya usimamizi wa ukaguzi wa magari na vidhibiti mwendokasi nchini Tanzania ya mwaka 2017.

Wadau wakuu waliohusika katika usimamizi wa usalama wa usafiri wa nchikavu na majini ni: Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano; Mamlaka ya Usafiri wa Nchikavu na Majini; Wakala wa Barabara Tanzania; na Jeshi la Polisi Tanzania.

Ripoti zote tatu za ukaguzi wa ufanisi katika utekelezaji, usimamizi, na ukaguzi wa usalama zilijielekeza katika kupunguza ajali na kuboresha utendaji katika sekta ya uchukuzi wa nchikavu na majini. Ripoti zote tatu zilionesha bayana udhaifu na mapungufu katika mipango (tathmini ya mahitaji na ukaguzi unaozingatia vihatarishi); kujenga uwezo wa masuala ya usalama; na utekelezaji wa sheria na kanuni. Ripoti hizi pia zilionesha udhaifu katika utekelezaji wa mipango; uratibu baina ya wadau mbalimbali; na ufuatiliaji na tathmini. Sehemu zifuatazo za sura hii zinaonesha uchambuzi wa masuala yaliyoonekana katika ripoti husika.

### 3.2 Tathmini Isiyojitosheleza ya Mahitaji ya Usafiri wa Barabarani na Majini

Tathmini ya mahitaji ni mchakato wa taratibu za kushughulikia mapungufu yaliyopo kulingana na uhitaji wake wa wakati uliopo. Umuhimu wa tathmini ya mahitaji unajibainisha katika kusaidia: kupanga gharama za utekelezaji wa mahitaji, hatua sahihi za kufuatwa, kuelewa ukubwa wa shughuli yenyewe, kutambua na kulinganisha malengo yake, na ufumbuzi mbadala katika kujiwekea vipaumbele.

Ripoti zote tatu za ukaguzi wa ufanisi zimeonesha udhaifu wa tathmini ya mahitaji wakati wa mipango ya awali ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuweka alama na samani za barabarani; ukaguzi wa usalama barabarani; pamoja na uchunguzi na ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa majini. Kwa mfano, ripoti ya ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa alama na samani za barabarani ilieleza kuwa Wakala wa Barabara Tanzania haukuzingatia kwa ufanisi mahitaji ya watumiaji wa aina zote wa barabara katika awamu ya awali ya mipango ya uwekaji wa alama na samani za barabarani. Hii ilisababishwa na ushirikishaji mdogo au kukosekana kwa ushirikishaji wa wadau muhimu katika mipango husika. Mathalani, Wakala wa Barabara Tanzania katika usanifu wa barabara na upembuzi yakinifu wa awali wa barabara, hutumia mwendokasi wa magari ambao ni kilometa 50 hadi 100 kwa saa ambao ni kwa ajili ya vyombo vya mwendokasi tu. Hii inamaanisha kwamba watumiaji wengine wa barabara (waendao kwa miguu, walemavu, baiskeli n.k) husahaulika katika awamu za mwanzo kabisa za mipango ya uwekaji wa alama na samani za barabarani. Kwa hiyo, Wakala wa Barabara Tanzania ungeweza kuchangia kupunguza ajali kwa kuzingatia mahitaji ya awali kwa watumiaji wote wa barabara katika kipindi cha awali cha miradi yote ya barabara.

Katika ripoti hiyohiyo ya ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa alama na samani za barabarani imeelezwa kuwa ukarabati na matengenezo ya alama na samani za barabarani haujumuishwa katika mifumo ya mipango ya ukarabati wa barabara ya Wakala wa Barabara. Hii inatokana na mfumo unaotumika kupanga kazi tofauti za matengenezo au ukarabati wa barabarani kutokuwa na uwezo wa kukusanya taarifa za kuangalia idadi na hali ya alama na samani za barabarani. Matokeo yake, Wakala wa Barabara Tanzania haujafanya uchambuzi wa masuala ya usalama barabarani na kuweka hatua za kudhibiti matengenezo ya alama na samani za barabarani.

Vilevile, Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mwaka 2017[6] ilionesha ukosefu wa mfumo wa kupanga maeneo ya kuweka vituo vya ukaguzi wa magari katika barabara kuu nchini. Hii ilisababishwa na ugawaji wa maofisa polisi, vitendea kazi kama vile rada za kupimia mwendokasi, na vipimo vya ulevi kwa ukaguzi wa usalama barabarani katika mikoa tisa (9) iliyochunguzwa haukuzingatia uhitaji au mahitaji katika maeneo hatarishi. Hii inamaanisha kwamba kulikuwa na ukosefu wa thathmini ya mahitaji ya awali kabla ya kufikiria upangaji wa polisi wa usalama na vitendeakazi kwa maeneo hatarishi.

[6] Ripoti ya Ufatiliaji wa Utekelezaji wa Shauri (2017), Ukaguzi wa Usalama Barabarani na Vithibiti Mwendokasi

Vilevile, ilielezwa katika ripoti ya ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa uchunguzi na kaguzi za vyombo vya usafiri majini kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini haikuwa na kanzidata ya meli ndogo zilizosajiliwa. Matokeo yake, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini iliandaa mipango isiyo ya uhalisia ya uchunguzi na kaguzi za meli ndogo kwa kuwa idadi ya ziara zilizopangwa zisingetosheleza kuchunguza na kukagua vyombo vyote vya usafiri wa majini vinavyofanya kazi Tanzania bara.

Makadirio ya ukaguzi wa meli ndogo kwenye mikataba ya utendaji ya mwaka uliyosainiwa kati ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini kwa mwaka wa fedha 2013/2014 hadi 2015/2016 yalikuwa ya chini kwa asilimia 85 ikilinganishwa na sensa ya 2012 ambayo ilibainisha jumla ya meli ndogo 30,866. Hivyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini haikutoa sababu sahihi kuhusiana na kupungua kwa ukaguzi na uchunguzi wa meli ndogo ukilinganishwa na makubaliano yaliyopangwa. **Jedwali na 3.1** linatuonesha na kuthibitisha meli ambazo hazikuwekwa katika mipango ya uchunguzi na ukaguzi.

**Jedwali na 3.1: Asilimia ya meli ndogo zisizokuwepo katika mpango ya ufuatiliaji**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya Uchunguzi/Kaguzi Zilizopangwa kwa kila Makubaliano ya Utendaji wa Mwaka | Idadi ya Meli Ndogo kwa Sensa (2012) | Tofauti | Meli Ndogo Zinazotekelezwa kutokana na Mipango (%) | Meli Ndogo Ambazo Hazikuzingatiwa katika Mipango au Makubaliano (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 2760 | 30,866 | 33,626 | 9 | 91 |
| 2014/2015 | 4,600 | 30,866 | 26,266 | 15 | 85 |
| 2013/2014 | 4,400 | 30,866 | 26,466 | 14 | 86 |
| 2012/2013 | Haikutolewa | 30,866 | N/A | N/A | N/A |
| 2011/2012 | Haikutolewa | - | - | - | - |

**Chanzo**: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Ukaguzi ya Usimamizi wa Uchunguzi na Ukaguzi wa Vyombo vya Usafiri wa Majini (2017) "

Jedwali 3.1 linaonesha malengo yaliyowekwa ya uchunguzi na kaguzi za meli ndogo kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 hadi 2015/2016 ambapo zaidi ya asilimia 85 ya meli ndogo hazikushughulikiwa katika uchunguzi na ukaguzi ikilinganishwa na Sensa ya Mwaka 2012 jambo ambalo ni hatari kwa usalama wa watumiaji.

## 3.3 Ukaguzi wa Magari na Meli Kutozingatia Masuala Hatarishi

Kaguzi zinazozingatia vihatarishi zinatarajiwa zipendekeze hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza matukio ya ajali za barabarani na majini. Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa uchunguzi na ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa majini; na ripoti ya ufuatiliaji wa ukaguzi wa usalama barabarani umeonesha tatizo

linalohusiana na kaguzi zinazofanyika kutozingatia vihatarishi vya ajali kama ifuatavyo. Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa uchunguzi na kaguzi za vyombo vya usafiri wa majini imeeleza kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini haikutumia mbinu za ukaguzi unaozingatia viashiria vya hatari au ajali katika mipango ya ukaguzi wa meli. Hii ni kwa sababu Mamlaka ilishindwa kuandaa maelezo ya viwango vya vihatarishi vya ajali katika usafiri wa majini. Matokeo yake, viashiria vya hatari kwa ajili ya usafiri wa majini havikufanyiwa kazi.

Tathmini ya uzingatiaji wa vihatarishi vya ajali ingeisaidia mamlaka husika kugawa rasilimali chache zilizopo ili kuboresha usalama katika usafirishaji majini. **Jedwali 3.2** linaonesha ugawaji wa ufuatiliaji na ukaguzi wa meli kwa mikoa ikilinganishwa na idadi ya meli kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2012.

**Jedwali 3.2: Idadi ya meli ndogo ikilinganishwa na idadi ya wachunguzi**

| Mkoa | Idadi ya meli ndogo kwa Sensa ya Mwaka 2012 | Idadi ya ufuatiliaji na wakaguzi wa meli |
|---|---|---|
| **Mwanza** | 15,148 | 1 |
| **Tanga** | 202 | 1 |
| **Lake Tanganyika** | 1,619 | 1 |

**Chanzo:** Sensa ya meli ndogo (2012)[7] na wafanyakazi

Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilifanya kaguzi 684 wakati kulikuwa na meli ndogo 15,148 mjini Mwanza kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2012. Hii inamaanisha kuwa takribani asilimia 95 ya meli ndogo zinazofanya kazi Mwanza hazikuchunguzwa na kukaguliwa. Hii inaweza kuchangia ongezeko la matukio ya ajali katika usafiri majini.

Aidha, katika ripoti hiyo imelezwa kwamba kaguzi za meli kubwa na ndogo zilifanywa bila kutumia fomu ya orodha ya kukagulia. Kwa mujibu wa ripoti, wakaguzi hawakujaza orodha za kukagulia kwa meli 38 zinazofanya kazi mkoa wa mwanza.

Pia, katika mkoa wa Tanga, fomu za orodha za kukagulia 19 tu ndizo zilijazwa ambazo ni sawa na chini ya asilimia 10 ya meli ndogo 202 zinazofanya kazi mkoa wa Tanga. Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilitakiwa kufanya ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa majini kwa kuzingatia uwezo wa meli, mifumo ya umeme, na vifaa vinavyotumika katika usafiri wa majini.

[7] Ofisi ya Taifa ya Takwimu, takwimu za meli ndogo na orodha ya wafanyakazi

Badala yake, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilijikita kwenye ukaguzi wa makoti ya kujiokolea na vifaa vya kuzimia moto ambavyo havina mchango mkubwa kwa ajali za usafiri wa majini. Matokeo yake, ukaguzi wa usalama wa usafiri wa majini haukufanyika kwa utimilifu kwa kuhakikisha kuwa chombo chochote cha usafiri wa majini kinakidhi vigezo kwa matumizi na usalama wa watumiaji.

Ripoti ya ufuatiliaji wa ukaguzi wa ufanisi kwa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa usalama barabarani imeonesha kwamba ukaguzi wa magari barabarani haukuweka kipaumbele kushughulikia masuala makuu yanayochangia ajali za barabarani.

Mathalani, Jeshi la Polisi Tanzania lilijikita kwenye ukaguzi wa makosa ya kimitambo, leseni za barabarani, ukosefu wa pembe tatu za tahadhari, na ukosefu wa vizimia moto. Makosa haya hayana mchango mkubwa katika ajali zinazotokea ikilinganishwa na ajali zinazosababishwa na makosa ya kibinadamu ambayo huchangia hadi asilimia 74 ya ajali zote za barabarani nchini.

Iliripotiwa kuwa Jeshi la Polisi Tanzania halikuwa na mpango wa kitaifa kuhusu viashiria vya hatari au ajali kwa kuweka mfumo sawia ikilinganishwa na gawio la rasilimali chache zilizopo. Vivyo hivyo, Jeshi la Polisi Tanzania halikutekeleza mapendekezo kuhusu uhifadhi wa nyaraka za maamuzi yote yaliyotolewa katika mchakato wa uchambuzi wa viashiria hatarishi vya ajali barabarani.

Kutokuwepo kwa uendelezaji na uanzishaji wa mipango/mkakati au mfumo wa kusimamia ajali katika ukaguzi wa usalama barabarani na kutokuwepo kwa tathmini ya mahitaji ni mojawapo ya sababu za kutotekelezwa kwa mapendekezo. Hali hii ilisababishwa hususani na kutokuwepo kwa uanzishaji wa mpango wa njia za ukaguzi unaozingatia vihatarishi vya ajali.

Aidha, riporti ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ilionesha kuwa hapakuwa na mpango wa utekelezaji ulioandaliwa na Jeshi la Polisi Tanzania ili kushughulikia vihatarishi vya ajali kubwa zinazosababishwa na madereva kwa ajili ya usalama barabarani. Pia, hapakuwa na mikakati ya kupeleka maofisa wa polisi wa barabarani kwenye maeneo yaliyotambuliwa kuwa na kiwango kikubwa cha ajali za barabarani hapa nchini. Matokeo yake, Jeshi la Polisi Tanzania lilishindwa kupanga vituo vya ukaguzi wa magari barabarani kwa sababu ya ukosefu wa mpango wa utekelezaji wa ukaguzi unaozingatia vihatari vya ajali barabarani.

Ripoti ya Ufatiliaji wa Ukaguzi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mwaka 2017 ilitambua juhudi zilizofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania katika utekelezaji wa mapendekezo kwa kutumia vifaa vya kisasa ambavyo vinaweza kutoa taarifa za ukaguzi wa usalama barabarani kwa ufanisi zaidi. Miongoni mwa mifumo hiyo inayotumiwa na Jeshi la Polisi Tanzania ni pamoja na mfumo wa usimamizi wa taarifa za ajali za barabarani, ambao huhusisha kompyuta, mfumo wa kimataifa wa utambuzi wa mahali (GPS), simu za kisasa kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa, na rada za mwendokasi. Mifumo na vifaa hivi vinawezesha utambuzi wa maeneo hatarishi ya ajali za mara kwa mara.

Mbali ya kuwa na mfumo wa ukasanyaji taarifa za ajali barabarani, ripoti hiyo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ilionesha pia kutokuwepo kwa mfumo wa usimamizi wa vihatarishi unaotoa mchakato mzima wa taarifa za ajali barabarani na jinsi ya upatikanaji wa vihatarishi. Hii inatokana na kwamba hakukuwa na mipanga au mikakati madhubuti katika usimamizi wa ukaguzi wa usalama wa barabarani. Kwa hiyo, kungekuwepo na mfumo wa usimamizi wa vihatarishi vya barabarani kungesisitizwa maeneo muhimu ya usalama ili kuchukuliwa hatua za haraka za kupunguza ongezeko la kasi ya ajali.

## 3.4 Utekelezaji Usiojitosheleza wa Mkakati wa Mafunzo ya Usalama Barabarani

Ripoti mbili za ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi na utendaji wa shughuli za usalama kwenye sekta ya uchukuzi zimeonesha kuwa mamlaka husika hazikutekeleza mipango mkakati ya mafunzo ya usalama kwa usafiri wa barabarani kama inavyoelezwa hapa chini.

Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa alama na samani za barabarani ilionesha kuwa Wakala wa Barabara Tanzania haukutekeleza ipasavyo mpango wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake kwa ajili ya usimamizi kiufanisi wa usalama wa barabarani. Kwa mfano, katika mpango wa utekelezaji wa makubaliano kwa Wakala wa Barabara Tanzania kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hadi 2015/2016 ilipangwa kufanyika kwa mafunzo kwa wafanyakazi wake ya ukaguzi wa usalama barabarani. Hata hivyo, hakukuwa na uwezeshaji ili wafanyakazi husika waweze kupata mafunzo hayo.

Ilionekana pia kwamba Jeshi la Polisi Tanzania halikuendeleza mkakati wa mafunzo ambao ungeenda sambamba na kiwango cha rasilimaliwatu. Hii ni kutokana na sababu za awali zilizotolewa na Jeshi la Polisi Tanzania kuwa mpango wa rasilimaliwatu na usalama barabarani bado haujaandaliwa kwa ajili ya mkakati wa mafunzo. Matokeo yake, utekelezaji wa mafunzo ya usalama barabarani haukufanyika ili kuchangia punguzo la ajali barabarani.

## 3.5 Usimamizi Duni wa Sheria na Viwango vya Usalama

Sheria za usalama, kanuni, na viwango zinatarajiwa kutoa mwongozo kwa wadau wakuu wote wanaoshiriki katika kusanifu na kujenga miundombinu, na watumiaji wa huduma za usafiri wa barabarani au majini. Ili kupunguza ajali barabarani na majini, adhabu zinapaswa zitolewe kwa wavunjasheria viwango vya usalama barabarani. Hata hivyo, ripoti tatu za ukaguzi wa ufanisi zilizohusika kwenye eneo hili la usalama, zilibaini kuwa usimamizi wa sheria na viwango vya usalama barabarani haukufanyika kama inavyoelezwa hapa chini.

Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa alama na samani za barabarani ilionesha uwepo wa alama za barabarani, mistari iliyochorwa barabarani, na reli kingamo za barabarani ambazo ni za chini ya viwango vilivyotakiwa kama inavyooneshwa kwenye icha 3.1. Hii ilisababishwa na usimamizi dhaifu wa mwongozo wa alama za barabarani na udhaifu wa usimamizi wakati wa kuweka alama au samani za barabarani wakati wa ujenzi wa barabara.

**Picha 3.1: Mwisho wa alama ya mwendo wa kilomita 50 kwa saa zikiwa chini ya kiwango zilizoonekana kwenye barabara mpya**



Picha 3.1a: Alama ya mwisho wa mwendo wa kilomita 50 kwa saa ilionekana imefifia. Picha ilipigwa Desemba 13, 2016 kwenye Barabara ya Segera - Tanga




Picha 3.2b: Alama ya mwisho wa mwendo wa kilomita 50 kwa saa ilionekana imefifia. Picha ilipigwa Desemba 19, 2016 kwenye barabara mpya ya Mbeya - Lwanjilo - Chunya

**Chanzo: Picha zilipigwa na wakaguzi wa ufanisi**

Ukaguzi wa Ufanisi wa Utendaji wa Usimamizi wa uchunguzi na kaguzi za vyombo vya usafiri wa wa majini umebaini kuwa wamiliki na waendeshaji wa meli ndogo hawakukidhi vigezo vya kisheria na kanuni zinazosimamia sekta ndogo ya usafiri wa majini. **Jedwali 3.3** linaonesha adhabu zilizotolewa kwa wakiukaji wa viwango vya usalama.

**Jedwali 3.3: Amri za kusimamishwa uendeshaji wa meli na adhabu kwa wakiukaji wa Viwango vya Usalama**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Meli Ndogo Zilizokiuka Viwango vya Usalama | Idadi ya Vikwazo au Adhabu Zilizotolewa | | Kiwango cha Utekelezaji (%) | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Amri ya Kusimamishwa | Fai | Amri ya Kusimamishwa | Fai |
| 2015/2016 | 1,667 | 0 | 31 | 0 | 1.8 |
| 2014/2015 | 1,663 | 17 | 0 | 1.02 | 0 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2013/2014 | 2,933 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 2012/2013 | 4,161 | 159 | 0 | 3.82 | 0 |
| 2011/2012 | 2,513 | 0 | 0 | 0 | 0 |

**Chanzo:** Uchambuzi wa wakaguzi

Kutoka katika Jedwali 3.4, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilianza kutoa adhabu kwa wakiukaji wa sheria za usalama kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015 hadi 2015/2016. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2015/2016, ni asilimia 1.85 tu ya adhabu ndiyo ilitolewa kwa wakiukaji wa sheria za usalama. Matokeo yake, ukiukaji wa viwango vya usalama katika meli ndogo bado ni tatizo kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 3.4**.

**Jedwali 3.4. Idadi ya Matukio ya Kutokidhi Viwango vya Usalama**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya Uchunguzi na Ukaguzi (A) | Idadi ya Vyeti vya Usalama Vilivyotolewa (B) | Wasiokidhi Viwango vya Usalama (%) (1- B/A)*100 |
|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 3,748 | 2,081 | 46 |
| 2014/2015 | 4,502 | 2,839 | 37 |
| 2013/2014 | 4,634 | 1,701 | 63 |
| 2012/2013 | 6,156 | 1,995 | 68 |
| 2011/2012 | 4,825 | 2,312 | 52 |

**Chanzo:** Uchunguzi wa wakaguzi

Kupanda na kushuka kwa ukiukaji wa viwango kulitokana na ukaguzi na usimamizi dhaifu wa utekelezaji wa sheria na viwango vya usafiri wa njia ya maji. Ilibainika kuwa kukidhi viwango kulitegemeana na ongezeko la kaguzi na ufuatiliaji uliofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini.

Ripoti hiyohiyo ya ukaguzi ilionesha udhaifu katika utekelezaji wa sheria na viwango vya usalama katika ukaguzi wa meli ndogo zinazofanya kazi Tanzania Bara. Katika miaka ya fedha kati ya 2011/2012 na 2015/2016, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilifanya kaguzi chini ya asilimia 20 ya meli ndogo

30,866 zinazofanya kazi Tanzania[8]. Hii ilitokana na utekelezaji duni wa viwango vya usalama majini.

Pia, iliripotiwa kuwa meli ndogo nne zinazoitwa MV Vero, MV Juliana, MV Norris, na MV St. Mathew zilizokuwa zikifanya kazi katika mwaka wa fedha 2015/2016 zilipatiwa vibali huku zikiwa na mapungufu yaliyobainika wakati wa uchunguzi na ukaguzi. Hata hivyo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano haikuchukua hatua yeyote kuhusiana na utoaji wa vyeti kwa meli zilizotajwa hapo juu kwa kutokidhi vigezo vya usalama; vilevile, Wizara haikuwachukulia hatua wamiliki wa meli hizo. Hii ilisababisha uwezekano wa matukio la ajali katika vyombo hivyo kutokana na ukiukwaji wa viwango vya usalama.

Vilevile, ripoti ya kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya mwaka 2017 ilibaini utolewaji wa adhabu dhaifu kwa wavunjasheria za barabarani. Jeshi la Polisi Tanzania lilitumia vifaa vya kisasa mkoani Dar es Salaam, ambavyo havikuwa na mafanikio, kukamata na kuwapa adhabu au faini wavunjasheria za barabarani wenye mafanikio duni.

Kwa mfano, Jeshi la Polisi Tanzania lilianzisha njia za kutathmini ufanisi wa adhabu zinazotolewa na utekelezaji wake kupitia mfumo wa usimamizi wa usafiri wa magari, mfumo wa kompyuta kwa usajili wa madereva, na mfumo wa kompyuta wa usafiri wa magari. Njia hizi zilisaidia kutoa tiketi za kielektroniki uliofanywa mkoani Dar es Salaam. Kama mifumo hii ingekuwa imesambazwa nchi nzima ingeleta ufanisi na tija katika usimamizi wa sheria za usalama na utoaji adhabu kwa wavunjajisheria za usalama barabarani na kuleta tija na ufanisi kwa adhabu zinazotolewa na Jeshi la Polisi Tanzania. Pia, kwa kutumia mifumo hii imeonesha kuwa leseni za udereva za wavunjasheria zinaweza kusitishwa au kufutwa kabisa.

Hata hivyo, ripoti ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya mwaka 2017 ilibaini kuwa Jeshi la Polisi Tanzania lilishindwa kusitisha au kufuta leseni za udereva 56 katika miezi mitatu ya mwanzo tangu kuanzishwa kwa mfumo wa usimamizi wa usafiri wa magari. Kwa mfano, katika mwaka wa 2017 kulikuwa na makosa ya uvunjifu wa sheria za barabarani 6,026 sawa na adhabu ya faini ya kiasi cha shilingi milioni 338 ambazo hazikukusanywa na Jeshi la Polisi Tanzania. Sababu iliyotolewa na Jeshi la Polisi Tanzania ni kwamba mifumo hiyo ilikuwa haijaanza kufanya kazi rasmi bali ilikuwa kwenye majaribio kwa mkoa wa Dar es Salaam. Matokeo yake, udhibiti wa uvunjifu wa sheria za barabarani uliotarajiwa kutokana na adhabu zilizotolewa haukufankiwa.. Hali hii imefanya madereva wengi kurudiarudia makosa waliyoyatenda awali.

[8] Sensa ya Mwaka 2012: Idadi ya meli ndogo na wafanyakazi

## 3.6 Kutotekelezwa Kikamilifu kwa Mipango ya Kuangalia Usalama

Utekelezaji wa mipango na viwango vya usalama barabarani unachangia kwa kiwango kikubwa uboreshaji wa usalama barabarani kwa kudumisha na kuboresha hatua dhidi ya usalama. Kaguzi zilizofanyika zimeonesha mapungufu katika utekelezaji wa mipango kama inavyoelezwa hapa chini.

Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa alama na samani za barabarani iliripoti kuwa Wakala wa Barabara Tanzania ulipokea gawiwo la takribani shilingi milioni 310 kwa ajili ya uwekaji wa alama na samani za barabarani za watu wenye ulemavu kutoka Wizara ya Ujenzi. Hata hivyo, Wakala wa Barabara Tanzania ulizitumia kwa ajili yashughuli zingine za ukarabati na matengenezao ya barabara na si uwekaji wa alama za walemavu kama ilivyopangwa. Hivyo, Wakala wa Barabara Tanzania haukuweka alama za watu wenye ulemavu nchini. Hii ilisababishwa na kipaumbele cha chini/kidogo kilichowekwa na Wakala wa Barabara Tanzania katika utekelezaji wa mipango iliyopo. Kushindwa kuweka alama za barabarani za watu wenye ulemavu nchini huenda kulichangia ongezeko la ajali kwao, kwa kuwa hawakuweza kuongozwa vizuri na alama hizo.

Ukaguzi pia uliripoti kuwa alama na samani nyingi hazikuwekwa barabarani na hazikufanyiwa matengenezo kwa kwa sababu ya utekelezaji dhaifu wa mpango wa matengenezo ya alama na samani za barabarani. Hii ilisababishwa na Wakala wa Barabara Tanzania kujiwekea vipaumbele vya ukarabati wa barabara na miundombinu mikubwa au barabara kuu badala ya alama na samani za barabarani pia. Matokeo yake, kulikuwa na alama na samani za barabarani ambazo hazikufanyiwa matengenezo. Hii inaweza kuwa ilichangia ongezeko la ajali barabarani. Kwa mfano, Picha 3.2 inaonesha alama za barabarani na reli kingamo za barabarani zikiwa hazijafanyiwa matengenezo.

**Picha 3.2: Alama za barabarani na reli-kingamo zikiwa hazijafanyiwa matengenezo**




Picha 3.2a: Alama ya mwanzo wa mwendo wa kilomita 50 kwa saa imeliwa na kutu. Picha ilipigwa na wakaguzi maeneo ya Chimala, barabara ya Igawa, Mbeya (TANZAM) tarehe 20/12/2016



Picha 3.2b: Reli kingamo za barabarani zilizokosa baadhi ya vipande na kuliwa na kutu zaidi ya kilometa 2. Picha ilichukuliwa na wakauguzi maeneo ya Mikindani, Mtwara

**Chanzo**: Picha ilipigwa na wakaguzi wa ufanisi

## 3.7 Uratibu dhaifu baina ya wadau wakuu wa usafiri wa barabara

Miongoni mwa mambo muhimu ya ushirikiano katika kuratibu ni pamoja na kubadilishana takwimu na habari, mtiririko mzuri wa habari baina ya wadau, na ufahamu wa kina wa majukumu ya kila mdau wa usalama. Usalama katika sekta ya usafirishaji itaendelea kuwa changamoto ikiwa uratibu wake ni dhaifu. Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi katika utendaji wa usimamizi wa alama na samani za barabarani ilionesha udhaifu katika uratibu baina ya wadau wakuu na wadau wengine muhimu wa usalama barabarani.

Kulikuwa na ushirikiano dhaifu kati ya Wizara ya Ujenzi, Usafirishaji, na Mawasiliano; Wakala wa Barabara Tanzania; na wadau wengine muhimu kama vile Jeshi la Polisi Tanzania. Mufumo wa takwimu na ushirikiano wa kuchangia taarifa baina yao haukuwa mzuri. Kwa mfano, taarifa za mfumo wa kimataifa wa utambuzi wa eneo kwenye sehemu za barabara zenye matukio mengi ya ajali kupitia mfumo wa taarifa au habari za ajali barabarani haukuhuishwa mara kwa mara na hivyo haukutumiwa ipasavyo na Wizara ya Ujenzi; Wakala wa Barabara Tanzania; na Jeshi la Polisi Tanzania. Matokeo yake, masuala yanayohusiana na usalama barabarani hayakushirikishwa vizuri baina ya wadau wakuu kwa lengo la kuwa na juhudi za pamoja za kupunguza ajali na kuboresha usalama barabarani. Hii ilisababishwa na uratibu dhaifu kati ya Wizara ya Ujenzi; Wakala wa Barabara Tanzania; na Jeshi la Polisi la Tanzania.

Pia, ilibainika kuwa kulikuwa na ushirikishaji dhaifu baina ya Wakala wa Barabara Tanzania na TAMISEMI kwa barabara za mijini kuhusu utaratibu wa uwekaji wa mabango ya matangazo yaliyoko chini ya serkali za mitaa kwenye barabara zinazomilikiwa na Wakala wa Barabara Tanzania. Kwa mujibu wa Wakala wa Barabara Tanzania, mabango hayo huziba alama au samani za barabarani zilizowekwa karibu na mabango hayo na kuweza kusababisha ajali. Hii ilisababishwa na uratibu hafifu kati ya Wakala wa Barabara Tanzania na TAMISEMI kuhusu taratibu za uwekaji mabango katika barabara za mijini. Matokeo yake, mabango hayo yamekuwa yakizuia alama za barabarani kuonekana vizuri na hivyo kuwa na uwezekano wa kuchangia ongezeko la ajali za barabarani.

Vivyo hivyo, ripoti hiyo ilionesha kuwa kulikuwa na juhudi tofauti kati ya Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania katika utambuzi wa sehemu zenye matukio mengi ya ajali kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Tanzania. Hii ni kwa sababu hakukuwa na majukumu ya wazi kati yao. Pia, iligundulika kuwa Wakala wa Barabara Tanzania na Wizara ya Ujenzi wote walifanya kazi moja ya ukaguzi wa usalama barabarani. Utaratibu huu ni gharama kubwa kwa serikali. Hii ilisababishwa na matumizi mara mbili ya rasilimali za serikali (yaani muda, watu, pesa na vifaa) kwa kazi moja, ambayo ingefanywa na mmoja wao. Iwapo kazi hiyo ingeunganishwa kati ya Wakala wa Barabara Tanzania na Wizara ya Ujenzi, gharama za ukaguzi zingepunguzwa kwa kiasi kikubwa. Hii ilisababishwa na mipango na juhudi za usalama barabarani kutounganishwa katika utekelezaji wake. Pia, imesababishwa na kushindwa kutambua kwa wakati stahiki wa visababababishi vya ajali za mara kwa mara kwenye maeneo hatarishi na kushughulikiwa katika hatua tofautitofauti za miradi ya ujenzi wa barabara kwa ujili ya kuboresha usalama katika usafiri wa barabara.

### 3.8 Ufuatiliaji na tathmini isiyotosheleza ya usalama katika sekta ya usafirishaji

Ufuatiliaji na tathmini inahusisha utambuzi wa udhaifu kwa lengo la kuboresha na kufanikisha malengo yaliyowekwa. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano; Wakala wa Barabara Tanzania; Jeshi la Polisi Tanzania; na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini walitarajiwa kufuatilia na kutathmini utendaji wao katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku. Vilevile, Wizara ya Ujenzi ilitakiwa kufuatilia na kutathmini utendaji wa mamlaka, wakala, pamoja na mihimili ya udhibiti iliyopo chini yake kuhusu utendaji wao katika kutekeleza shughuli zao.

Riporti ya ukaguzi wa ufanisi katika utendaji wa usimamizi wa alama na samani za barabarani ilionesha kwamba Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano, na Wakala wa Barabara Tanzania

hazikufanya kwa ufanisi ufuatiliaji na tathmini ya alama na samani za barabarani. Hii ilisababishwa na ukosefu wa mpango wa ufuatiliaji na tathmini uliotakiwa kuwekwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano pamoja na Wakala wa Barabara Tanzania.

Wakati huohuo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano ilitumia ukaguzi wa usalama barabarani kama nyenzo na sehemu ya mchakato wa kufuatilia na kutathmini usalama barabarani. Hata hivyo, Wakala wa Barabara Tanzania na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano hazikufanya ukaguzi wa usalama barabarani katika hatua zote za miradi ya ujenzi wa barabara (yaani tathmini ya awali, usanifu, upembuzi yakinifu, ujenzi, na wakati wa kuitumia barabara) kama ilivyoelezwa katika ripoti ya ukaguzi na ufanisi wa alama na samani za barabarani. Ripoti hiyo ilisisitiza kuwa ni kaguzi tano tu ndizo zilifanyika kati ya kaguzi 66 za usalama barabarani zilizotakiwa kufanyika chini ya ukaguzi wa ufanisi na usimamizi wa alama na samani za barabarani. Hata hivyo, shughuli za ukaguzi wa usalama barabarani hazikufuatiliwa wala hazikutathminiwa kwa ajili ya viashiria ili kukabiliana na tahadhari za usalama ambazo zinapaswa kushughulikiwa katika mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti ya Ukaguzi wa Usalama Barabarani. Hii ilisababishwa na ukosefu wa rasilimali-watu katika Wakala wa Barabara Tanzania na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano hivyo kusababisha kutofanyika kikamilifu kwa ukaguzi wa usalama barabarani ili kuashiria maeneo hatarishi kwa lengo la kuboresha usalama barabarani.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Utendaji wa Usimamizi wa Tafiti na Kaguzi za Vyombo vy Usafiri wa Majini ilionesha kuwa kulikuwa na ufuatiliaji na tathmini dhaifu katika ukaguzi wa meli au vyombo vya usafiri wa majini. Hii ni hata baada ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano ilianzisha mkataba wa makubaliano ya utendaji kama chombo cha kupima utendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini.

Makubaliano ya mkataba huo yaliitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini kuwasilisha taarifa za robo mwaka kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano na kisha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini kupata mrejesho kutoka Wizarani.

Hata hivyo, katika miaka ya fedha kuanzia 2013/2014 hadi 2015/2016 hakukuwa na taarifa za robo mwaka zilizopelekwa wala maoni kutoka Wizarani. Hivyo, hakukuwa na ufuatiliaji na tathmini iliyofanyika kuanzia mwaka wa fedha wa 2012/2012 hadi 2015/2016 kwa masuala ya uchunguzi na kaguzi za vyombo vya usafiri wa majini. Hii ilisababishwa na kushindwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano kuweka kipaumbele katika shughuli za ufuatiliaji na

tathmini ili kuhakikisha kuwepo kwa usalama katika usafiri wa majini kwakuwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2012/2013 hadi 2015/2016 hakuna matumizi yoyote ya fedha kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini katika kitengo cha "Usalama wa Usafirishaji na Mazingira"[9]. Hivyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini haikufikia malengo yaliyowekwa ya kupunguza idadi ya ajali za meli na matukio ya asilimia sifuri kwa meli kubwa na asilimia 10 kwa meli ndogo.

Ripoti hiyo pia iliongezea kuwa kulikuwa na utekelezaji wa ufuatiliaji na ukaguzi usiojulikana wa vyombo vya usafiri wa majini. Hii ni kwa kwa sababu Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilishindwa kufanya tathmini ya utendaji wa kila mwaka wa utekelezaji wa uchunguzi na kaguzi za meli zote ndogo hapa nchini[10]. Matokeo yake, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilishindwa kuwianisha kaguzi zake halisi za meli ndogo na takwimu za Sensa ya Mwaka 2012 ili kutathmini utendaji wake kwa lengo la kuboresha usalama katika usafiri wa majini. Hii ingeweza kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini picha halisi ya utendaji wake kuelekea malengo iliyojiwekea na pia ingeonesha maeneo ya kuboreshwa wakati wa uchunguzi na ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa majini kwa usafiri salama na bora.

Hata hivyo, ukaguzi wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo wa mwaka 2017 ulionesha kwamba ufuatiliaji wa ukaguzi wa usalama barabarani unaofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania ulikuwa finyu. Jeshi la Polisi Tanzania halikufuatilia utendaji wa wafanyakazi wake katika ukaguzi wa usalama barabarani unaozingatia vigezo au mambo manne. Vigezo vitatu kati ya hivyo ambavyo havikutekelezwa upimaji wa kiwango cha ulevi kwa madereva, upatikanaji wa vifaa vya ukaguzi, na utendaji yakinifu wa maofisa wa Jeshi la Polisi Tanzania. Hii ilisababishwa na vipaumbele vya kiwango cha chini vilivyoweka na Jeshi la Polisi Tanzania kuhusiana na ufuatiliaji na tathmini. Matokeo yake, masuala makubwa hayakuzingatiwa wakati wa ukaguzi wa usalama barabarani ili kuboresha usalama na pia kupunguza ajali barabarani.

[9] Ripoti za Utendaji wa Mwaka za Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majinikwa mwaka wa fedha 2011/2012 hadi 2015/2016

[10] Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini (2013 / 14-2017 / 18)

# SURA YA NNE

# USALAMA WA USINDIKAJI NA UINGIZAJI CHAKULA NCHINI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza masuala yaliyobainika katika kusimaimia usalama wa chakula nchini. Imejikita katika maeneo matatu ya usalama wa chakula ambayo ni usalama wa chakula kinachoandaliwa viwandani na kwenye machunjio, usalama wa chakula kinachoingizwa nchini, na usalama katika mchakato wa kuandaa nyama.

Hoja zimegawanywa katika makundi sita, ambayo ni mipango, ukagunzi, uratibu, utoaji taarifa za ukaguzi, ufuatiliajia na tathmini za shughuli zote zinazohusiana, na utekelezaji wa sheria za usindikaji na uingizaji wa chakula nchini.

## 4.2 Mpangokazi Usiojitosheleza wa Shughuli Zinazohusiana na Usalama wa Chakula

Serikali kupitia Wizara za Afya, Kilimo, Mifugo, na Uvuvi; na Ofisi ya Rais – TAMISEMI; pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania, na Shirika la Viwango Tanzania imeandaa mpangokazi ambao ni mwongozo wa utekelezaji wa majukumu yao ya usimamizi wa chakula nchini kulingana na mamlaka zao. Kaguzi 2 kati ya 3 za usalama wa chakula zimeeleza mapungufu mbalimbali yanayohusiana na uandaaji wa mpangokazi wa utekelezaji wa matakwa ya usalama wa chakula kama inavyoelezwa hapa chini.

### 4.2.1 Mpangokazi wa ukaguzi wa usalama wa chakula usio wa ufanisi

Ripoti ya ufuatiliaji wa usimamizi wa ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa nchini imeeleza kuwa Shirika la Viwango Tanzania haliandai mpangokazi kama inavyotakiwa. Upitiaji wa ratiba za ukaguzi katika vituo vinne[11] vya kuingiza bidhaa nchini vilivyotembelewa na wakaguzi umebaini kuwa ni kituo kimoja tu kilichokuwa na mpangokazi wa ukaguzi. Hata hivyo, ratiba hiyo ilikosa vipengele muhimu kama vilivyotajwa hapo juu. Vituo vingine vitatu havikuwa na ratiba ya ukaguzi ambavyo ni Sirari, Holili, na Namanga. Pia, katika vituo vyote vinne ambavyo ni Bandari ya Dar es Salaam, Lango la Mpaka wa Sirari, Lango la Mpaka wa Holili, na Lango la Mpaka wa Namanga hapakuwa na mfumo wa vihatarishi kwa ajili ya kuandalia mpangokazi wa ukaguzi. Kukosekana kwenye mpangokazi vipengele kama viwango vya vihatarishi vya bidhaa inayotarajiwa kukaguliwa inaashiria uwezekano mkubwa wa kuingizwa nchini bidhaa zisizokidhi viwango.

[11] Vituo vya kuingiza mizigo vilivyotembelewa ni Bandari ya Dar es Salaam na bandari zake kavu; na milango ya Mipaka ya Sirari, Holili, na Namanga.

Hii imesababishwa na udhaifu katika mwongozo wa Shirika la Viwango Tanzania, ambao hautoi mwongozo wowote katika maeneo yafuatayo:

a) Tathmini ya vihatarishi kwa ajili ya kutambua bidhaa inayoingizwa toka nje ya nchi inayoonesha vihatarishi vya hali ya juu ili ipewe kipaumbele cha ukaguzi.
b) Sampuli inayolenga kuruhusu kupima matokeo ya ukaguzi ya nchi nzima.
c) Njia ya aina moja ya kufanya ukaguzi, ambayo inahusisha mfumo mzima wa mawasiliano wa kutunza matokeo ya ukaguzi.
d) Programu ya ufuatiliaji kwa waagizaji wa bidhaa toka nje ya nchi ili kuhakikisha hatua zinachukuliwa; na
e) Uhakiki wa ubora ili kujiridhisha iwapo ukaguzi umefanyika vizuri na kiuthabiti.

Ukaguzi wa ufuatiliaji katika usimamizi wa ukaguzi wa chakula na ufuatiliaji kwenye viwanda vinavyosindika chakula na wakati wa kuingiza chakula bandarini uliripoti kuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania ina mpangokazi wa ukaguzi ambao hauna vipengele vya ukaguzi unaojikita kwenye vihatarishi.

Pia, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania imeweza kuainisha bidhaa za chakula na viwanda vya usindikaji wa chakula ambavyo ni hatarishi kulingana na aina ya bidhaa inayosindikwa. Hata hivyo, bidhaa na viwanda hivyo havikuoneshwa kwenye mpangokazi unaotumika kwenye ukaguzi. Mpangokazi haukuzungumzia mzunguko wa ukaguzi utakavyofanyika kwenye viwanda vinavyosindika bidhaa hatarishi na bidhaa za chakula zinazoingizwa nchini ambazo zina kiwango kikubwa cha vihatarishi.

Kwa kusema hivyo, makundi ya viwanda vinavyosindika chakula chenye vihatarishi wa hali ya juu, kati, na chini vyote vilipewa kipaumbele sawa wakati wa ukaguzi. Hata ofisi za kanda za Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania hazijaonesha mzunguko wa ukaguzi zaidi ya kutaja tu kwa ujumla kuwa ukaguzi utafanyika kwenye viwanda vyote vinavyofanya shughuli za usindikaji kwenye maeneo husika.

Hii imebainika kuwa kinyume na mwongozo wa ukaguzi wa tahadhari ya mapema unaowataka mameneja wa kila kanda kuainisha viwanda vyote vinavyosindika bidhaa ambazo zina vihatarishi vikubwa na kuandaa mzunguko wa ukaguzi. Kukosekana kwa mzunguko wa ukaguzi kwenye mpangokazi kunapelekea viwanda vya usindikaji chakula kuzalisha chakula kisicho salama kwa matumizi ya binadamu.

## 4.3 Mazingira Hatarishi ya Uandaaji wa Chakula (nyama)

Ripoti ya udhibiti wa usafi katika uandaaji/usindikaji wa nyama imebainisha mapungufu katika mazingira ya uandaaji wa nyama. Mathalani, miundombinu ya machinjio haikuwa katika hali ya usafi. Kulingana na ripoti, machinjio 9 kati ya 12 yaliyotembelewa hayakuwa katika hali usafi inayokubaliwa na sheria ya magonjwa ya wanyama. Jedwali 4.1 linaonesha udhaifu uliobainika pamoja na asilimia ya machinjio yaliyobainika kuwa na udhaifu huo.

**Jedwali 4.1: Mazingira yasiyo salama yaliyobainika katika machinjio yaliyotembelewa**

| Udhaifu uliobainika | Asilimia ya machinjio yenye udhaifu |
|---|---|
| Ukosefu wa maeneo ya kufanyia usafi wa miguu, mikono, ukaguzi wa nyama | 67 |
| Kutokuwepo kwa maji ya kutosha kwa ajili ya kufanyia usafi | 50 |
| Harufu mbaya inayoweza kuharibu nyama | 67 |
| Sakafu chakavu na chafu inayoweza kusababisha uchafu kwenye nyama | 42 |

Hii imesababishwa na usimamizi dhaifu wa sheria na kanuni zilizopo na uwezo mdogo wa miundombinu ya machinjio.

### 4.3.1 Usajili hafifu wa viwanda vinavyozalisha chakula, maeneo, na vyombo vya kusafirishia

Kaguzi tatu za ufanisi zilizofanyika zimeonesha udhaifu wa usajili wa maeneo ya uzalishaji wa chakula, viwanda vinavyozalisha chakula, na vifaa vya kusafirishia chakula. Udhaifu ulihusiana na usajili hafifu, ufanisi mdogo katika kusajili vifaa, na kutofuata taratibu za usajili zinazotakiwa kama ilivyoelezwa hapa chini.

Ripoti ya ufuatiliaji wa usimamizi wa ukaguzi wa chakula na ufuatiliaji kwenye viwanda vinavyosindika na vinapoingizwa nchini imeeleza kutokuwepo na uthibitisho wa kuonesha kuwa viwanda vyote vya chakula vilikuwa na leseni au vilikuwa vimesajiliwa. Kwa hivyo, viwanda vyote vya chakula havijaonekana katika rejista ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania. Kulingana na ripoti, rejista ina sensa ya ukaguzi tu. Hivyo, kuna hatari ya kuwa na viwanda vya usindikaji wa chakula ambayo vinafanya kazi bila kufikia viwango vinavyotakiwa kwa usalama wa chakula.

Ripoti ya udhibiti wa usafi katika uandaaji/usindikaji wa nyama, iliripoti kuwa machinjio 912 kati ya 932 (sawa na asilimia 98) yalikuwa hayajasajiliwa. Hii ni kinyume cha sheria Na.1, sehemu ya 18(1) ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania ya Mwaka 2003; na kanuni Na. 5(1) ya Magonjwa ya Wanyama ambayo inataka machinjio yote yasajiliwe kabla ya kuanza kazi.

Ripoti ilionesha kwamba machinjio yalikuwa yakiendeshwa huku yakiwa yamekosa vitu muhimu kama vyoo, sehemu ya kuoshea miguu na kunawa mikoni, na upimaji wa afya za wafanya, masuala ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuweka uhakika wa hali ya usafi wa mazingira ya uandaaji wa nyama. Kulingana na ripoti hiyo, uandaaji wa nyama katika mazingira yasiyo safi huleta hatari ya kuweza kupeleka nyama isiyo salama kwa umma.

Pia ripoti hiyo ilionesha magari ya kubebea nyama toka machinjioni yalikuwa hayajasajiliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika. Magari hayakukidhi vigezo vya kubeba nyama kwakuwa yalikuwa katika hali ya uchafu na yenye kutu. Pia, ripoti iliendelea kuonesha kuwa nyama ilikuwa ikibebwa kwa kutumia njia ambazo hazijaidhinishwa kama vile pikipiki. Hii ilileta hatari ya nyama kuchafuliwa na kuhatarisha afya za watumiaji.

Kulingana na ripoti ya ukaguzi wa ufanisi, usajili hafifu ulisababishwa na ukaguzi mdogo na usimamizi hafifu wa sheria na kanuni zake. Pia, imeeleza kuwa uwepo wa wadau watatu tofauti wenye jukumu la kusajili machinjio bila kuwepo mipaka ya kiutendaji kunaathiri usajili wa machinjio.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania walikuwa na sheria tofauti za usajili wa machinjio bila kutengeneza mipaka ya kila mmoja. Matokeo yake, machinjio hayakusajiliwa kila mmoja akijua kuwa mwezake ameshafanya.

### 4.3.2 Mapungufu ya Mwongozo wa Usajili

Ukaguzi wa ufanisi katika udhibiti wa usafi katika uandaaji/usindikaji wa nyama umebaini kuwa mwongozo wa usajili unaotumiwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; na Bodi ya Nyama Tanzania umeweka matakwa ya msingi ya kusajili machinjio ambayo ni kufikisha asilimia 55 ya matakwa yote yanayotakiwa. Matokeo yake, asilimia 50 ya machinjio yaliyosajiliwa yalikosa mambo muhimu[12] yanayotakiwa kwa jili ya kuzuia uchafuzi wa nyama. Pia, imeelezwa katika ripoti ya usimamizi

[12] Uwepo wa vyoo visafi na vya kutosha; uwepo wa maji na yenye msukumo wa kutosha; sakafu za machinjio zenye vining'inizio vya kutosha kwa ajili ya kutundikia nyama; wakaguzi wa nyama wenye sifa stahiki; uondoshaji madhubuti wa taka; miundombinu kwa ajili ya kusafishia vifaa; takwimu za matibabu kwa wafanyakazi.

wa ukaguzi wa chakula na ufuatiliaji kwenye viwanda vinavyosindika na vinapoingia nchini kuwa mwongozo wa ukaguzi wakati wa usajili unaotumika una mapungufu. Hii ni kwa sababu eneo linalokaguliwa linapofikisha kiwango fulani cha alama, eneo linaweza kuchukuliwa kuwa limefikisha sifa stahiki za kupata usajili na leseni/kibali au likapata sifa ya kusajiliwa na kupewa leseni kwa masharti ya kufanya maboresho zaidi baadaye.

## 4.4 Ukaguzi Hafifu wa Viwanda Vinavyosindika Chakula, Mahali pa Kusindikia Chakula, na Sehemu Chakula Kinapoingizwa Nchini

### 4.4.1 Uwezo na ufanisi mdogo wa ukaguzi wa viwanda na vifaa vya kuzalisha chakula

Ripoti ya udhibiti wa usafi katika uandaaji/usindikaji wa nyama ilionesha kuwa ukaguzi wa shughuli za uzalishaji wa nyama unaofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania; na mamlaka za serikali za mitaa ulikosa ufanisi na umakini katika kushughulikia tatizo la mazingira machafu ya uandaaji wa nyama. Kulingana na ripoti hiyo, ufanisi wa ukaguzi wa machinjio ulikuwa haujitoshelezi kutokana na kuwepo kwa machinjio yasiyosajiliwa yakiwa yanafanya kazi na magari ya kubebea nyama ambayo hayakuwa katika hali ya usafi. Hali hii ilitakiwa irekebishwe kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara.

Pia, ripoti ilionesha kuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania na Wizara ya Mifugo na Uvuvi haikufanya ukaguzi wa kutosha ili kubaini kiwango cha utekelezaji wa matakwa ya kiafya na kimazingira. Hii ilikuwa muhimu ili kuhakikisha kuwa mazingira ya uandaaji wa nyama yanakuwa katika hali ya usafi.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kuanzia mwaka wa fedha 2010/11 hadi 2013/14, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania iliweza kukagua asilimia 37.7 (380 kati ya 1009) ya machinjio yote nchini; ambapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi haikufanya ukaguzi wowote kuazia mwaka wa fedha 2011/12 hadi 2014/15. Sababu za kufanya ukaguzi usiojitosheleza kwenye viwanda vinavyozalisha chakula ilikuwa uchache wa rasilimaliwatu na rasilimali-fedha zilizotengwa na Mamkala ya Chakula na Dawa Tanzania na Wizara ya Mifugo na na Uvuvi kwa ajili ya ukaguzi.

Ukaguzi wa ufuatiliaji wa ripoti ya usimamizi wa ukaguzi wa chakula na ufuatiliaji kwenye viwanda vinavyosindika na vinapoingia bandarini iliripoti kuwa viwanda vyote vinavyosindika chakula hatarishi havikukaguliwa.

Ripoti iliainisha pia kutofanyika ukaguzi kwenye viwanda vyote vinavyozalisha bidhaa hatarishi kama samaki na bidhaa zitokanazo na samaki, maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa, nyama na bidhaa zitokanazo na nyama, mboga zilizochakatwa, na viungo. Hii huiweka nchi nzima na watu wake katika hatari ya kupata magonjwa yatokanayo na chakula kama viwanda vinavyozalisha chakula havijakaguliwa na vinakiuka matakwa ya usalama wa chakula.

Kwa mujibu wa ripoti ya ukaguzi, sababu zilizopelekea kushindwa kukagua viwanda vinavyozalisha bidhaa hatarishi ni pamoja na ukaguzi usioeleweka unaotarajiwa kufanyika na mpangokazi wa ukaguzi wa chakula usiojitosheleza. Sababu nyingine ilikuwa kutotumia vinzuri rasilimali zilizopo za ukaguzi (rasilimali zote ambazo ni watu, fedha, na vifaa) na pia mwangozo wa ukaguzi uliokuwa hauoneshi vitu muhimu kuhusiana na ukaguzi wa chakula.

### 4.4.2 Ukaguzi wa nyama haukufanyika vizuri

Ripoti ya udhibiti wa usafi katika uandaaji/usindikaji wa nyama ilionesha kuwa uchache wa wakaguzi ulisababisha kushindwa kufanyika ukaguzi katika mchinjio yote. Ripoti ilionesha upungufu wa asilimia 40 ya wakaguzi wa nyama na kupelekea wakaguzi wa nyama kuelemewa na kazi.

Ripoti ilionesha pia kwamba wakaguzi wa nyama walitakiwa kukagua wanyama 100 -155 kwa siku, idadi ambayo ni kubwa na hivyo kuathiri utendaji na usahihi wa ukaguzi. Sababu nyingne ya ukaguzi wa nyama kutofanyika vizuri ni pamoja na mfumo mbaya, miundombinu ya machinjio isiyojitosheleza, na ujuzi mdogo wa wakaguzi wa nyama.

### 4.4.3 Ukaguzi bandarini haukufanyika katika maeneo yote

Ukagunzi wa ufuatiliaji wa ukaguzi wa usimamizi wa bidhaa toka nje ulionesha kuwa kwenye bandari kavu 10 zinazosimamiwa na bandari ya Dar es Salaam zilizotembelewa, wastani wa asilimia 39 hadi 73 ya majalada au mizigo ilishughulikiwa kwa siku. Kwa wastani, bandari kavu zinapokea jumla ya majalada/mizigo 284 kwa siku. Pia, bandari kavu 8 ambazo hupokea mafaili/mizingo 158 kwa siku husimamiwa na wakaguzi watatu tu.

Hii ilisababishwa na kukosekana kwa mpangokazi unaojitosheleza wenye mfumo wa vihatarishi kwa ajili ya ukaguzi wa bidhaa toka nje. Wakaguzi kupoteza saa za kazi wanapotoka bandari moja kwenda nyingine. Kuna wakaguzi wachache kwenye bandari kavu ikilinganisha na idadi ya majalada au kiasi cha mizingo inayotakiwa kushughulikiwa kwa siku.

## 4.5 Uratibu Hafifu wa Wadau Wanaojishughulisha na Usalama wa Chakula

Ukaguzi wa ufuatiliaji wa ripoti ya usimamizi wa ukaguzi wa chakula na ufuatiliaji kwenye viwanda vinavyosindika na vinapoingia bandarini ilionesha kuwa kuna uratibu hafifu baina ya Idara ya Mipango na Idara ya Tathmini ya Vihatarishi wakati wa kuaanda mpangokazi wa ukaguzi wa chakula katika Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania. Idara ya Mipango katika Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania haitumii taarifa yoyote kutoka Idara ya Tathimini ya Vihatarishi wakati wa kuandaa mpangokazi wa ukaguzi wa chakula.

Idara ya Tathimini ya Vihatarishi haitumii makubaliano ya ukaguzi wakati wa kuandaa makundi ya vihatarishi ya viwanda vinavyosindika chakula na bidhaa za chakula zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Pia, hakukuwa na mkaguzi hata mmoja anayetumia taarifa ya uchambuzi wa chakula wakati wa kufanya ukaguzi wa chakula. Hii itasababisha ukaguzi usiojitosheleza na kusababisha jamii kupata chakula kisicho salama.

Pia, ripoti hiyo ya ukaguzi ilibaini kuwa utoaji taarifa wa matokeo ya ukaguzi na utaratibu wa utoaji wa mrejesho wa kaguzi za chakula zilizofanyika ulikuwa haufanyi vizuri na haukuratibiwa ipasavyo. Hii ni kwa sababu taarifa za ukaguzi kutoka kwenye kanda za Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania zilichelewa kuwawasilishwa makao makuu. Hii imefanya iwe vigumu kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania kukusanya, kuchambua, na kutoa mapendekezo kwa aajili marekebisho.

Taarifa hiyo ilionesha kuwa uratibu baina ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania na idara nyingine za serikali ulikuwa mdogo. Hii ilithibitishwa na mambo manne yafuatayo:

### i) Kutoshirikishana takwimu zinazohusiana na ukaguzi wa chakula

Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania haijaanzisha utaratibu wowote ambao utawasaidia wakaguzi wake kutumia taarifa kutoka taasisi zingine za serikali. Taarifa kama vile wingi wa chakula kinachotarajiwa kuingizwa kutoka nchi nyingine hazikutafutwa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania; orodha ya viwanda vyote vinavyofanya shughuli ya usindikaji wa chakula viliyosajiliwa na BRELA haikutafutwa; waagizaji wa chakula toka nje ya nchi waliosajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania haikutafutwa; na taarifa ya utendaji wa viwanda mbalimbali vya usindikaji wa chakula na waagizaji wa chakula toka nje ya nchi hazikutafutwa kutoka kwa wazalishaji wa chakula husika. Hii iliathiri uandaaji wa mpangokazi wa ukaguzi wa chakula katika ngazi zote mbili yaani ngazi ya viwanda vya usindikaji pamoja na bandarini.

Taasisi kadhaa za serikali kama vile Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Idara ya Afya kwa Umma; mamlaka ya serikali za mitaa; na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania ilifanya ukaguzi wa chakula. Hata hivyo, ilibainika kwamba taasisi hizi za serikali hazikushirikishana matokeo ya ukaguzi wao ingawa walikuwa na lengo moja.

Ripoti ya udhibiti wa usafi katika uandaaji/usindikaji wa nyama ilionesha kwamba Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania na mamlaka za serikali za mitaa haziwasilishi au kushirikishana ripoti zao za ukaguzi kwa wadau muhimu ambao walitakiwa kupokea ripoti hizo. Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania huwasilisha ripoti za ukaguzi kwa mamlaka za serikali za mitaa, sekretarieti za mikoa, na wamiliki wa machinjio. Mara chache huwasilisha taarifa za ukaguzi kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Ripoti za ukaguzi hazikutumwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi au Wizara ya Afya.

Pia, iliripotiwa kuwa mamlaka za serikali za mitaa zilikuwa zikiwasilisha mara chache matokeo ya ukaguzi katika ofisi za makatibu tawala wa mikoa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Hata hivyo, mamlaka hizi hazikuwasilisha taarifa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi wala Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Vilevile, tawala za mikoa haziwasiliani na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Mara chache huwasiliana na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto; mamlaka za serikali za mitaa; Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania; na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Hali hii ilisababisha kuwepo utekelezaji duni wa mapendekezo ya ukaguzi.

Ripoti ya ukaguzi ilibainisha kwamba kushindwa kuwasilisha ripoti za ukaguzi kwa wadau wote muhimu kuliathiri utekelezaji wa hali ya usafi kwa sababu wadau/washiriki wengine, ambao pia walikuwa wasimamizi walikosa nafasi ya kutumia taarifa za ukaguzi katika kuchukua hatua ili kufanya marekebisho. Aidha, ukaguzi uliripoti kuwa uratibu duni/hafifu kati ya wadau muhimu katika sekta ya mifugo ulichangia tatizo hilo. Pia, kushindwa kuweka kumbukumbu sahihi za matokeo ya ukaguzi ilitokana na ukosefu wa usimamizi wa karibu na utekelezaji wa sheria katika machinjio.

**ii) Mfumo usioeleweka wa utoaji wa taarifa za ukaguzi**

Pamoja na ukweli kwamba maofisa wa afya (wakaguzi wa chakula) kutoka Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto walikuwa wakifanya ukaguzi wa chakula na kuandaa ripoti za ukaguzi

wa chakula, taarifa hizo hazikuwasilishwa kwenye Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania.

Wizara ya Afya ilisema kuwa ilikuwa vigumu kushirikisha taarifa zao na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania kwani wao ndio wizara mama na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania ilitakiwa kutoa taarifa hiyo kwa Wizara.

**iii) Kutooanisha shughuli za ukaguzi kwenye bandari**

Wakaguzi wa chakula kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto na wale kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania walikuwa wakifanya ukaguzi wa chakula. Wakaguzi wa Wizara ya Afya walikuwa wakifanya ukaguzi wa chakula kulingana na Sheria ya Afya kwa Umma Namba 12 ya Mwaka 2009 pamoja na wakaguzi wa chakula wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania.

Makundi yote wawili ya wakaguzi yalifanya ukaguzi wa aina moja unaolenga usalama wa chakula. Hii ilionesha kwamba licha ya ukaguzi wa chakula kuwa wa aina moja na ni shughuli za Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania, hakukuwa na mipaka yoyote kuhusiana na ukaguzi wa chakula kati ya wadau hawa wawili. Ukaguzi wa chakula kufanywa na vyombo mbalimbali vya udhibiti kunaweza kusababisha usumbufu kwa waagizaji/wazalishaji wa chakula na kupandisha gharama ya kufanya biashara nchini.

**iv) Uratibu hafifu kati ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Idara za Wizara**

Hakukuwa na ushirikiano mzuri kati ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na idara za wizara. Ofisi ya Rais - TAMISEMI haikuwa na viashiria muhimu vya utendaji kwa mamlaka za serikali za mitaa na tawala za mikoa ili kuchunguza utendaji wao katika idara ya mifugo hasa katika usafi wa mazingira ya machinjio.

Vilevile, hakukuwa na ripoti iliyopatikana katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI inayoonesha utendaji wa huduma za mifugo na mamlaka za serikali za mitaa licha ya kuwa na mratibu anayehusika na sekta hiyo. Ripoti pekee iliyopatikana ni ile inayohusiana na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, ambapo kipengele cha usafi katika uandaaji wa nyama hakikuwepo wakati wa uandaaji wa mpangokazi na utekelezaji wa mikakati mbalimbali.

Pia, hakukuwa na kipengele hicho katika Mkakati wa Maendeleo ya Mifugo wa Mwaka 2010, ambao unataka kuanzishwa kwa mfumo wa pamoja wa udhibiti wa magonjwa ya *'zoonotic'* kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Afya; na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa lengo la kulinda afya za wananchi.

Badala yake, wizara tatu hukutana mara chache sana na zikikutana inakuwa ni baada ya kuripotiwa kwa hali hatarishi ya uchafu. Iliripotiwa wakati wa ukaguzi kwamba mbinu inayotumika kusimamia na kufuatilia hali ya usafi katika mchakato wa uandaaji wa nyama haikuwa endelevu kutokana na ukosefu wa mgawanyo unaoeleweka wa mipaka ya uwajibikaji.

## 4.6 Utoaji Taarifa Usiojitosheleza wa Matokeo ya Usimamizi wa Usalama wa Chakula

### 4.6.1 Utoaji wa taarifa ya matokeo ya ukaguzi wa bidhaa toka nje ya nchi

Ripoti ya ukaguzi wa ufuatiliaji wa usimamizi wa ukaguzi wa bidhaa toka nje ya nchi ilibaini kuwa sababu ya kuwaelekeza kufanya ukaguzi zaidi kwenye baadhi ya mizigo haijawafikia kikamilifu maofisa wanaotakiwa kufanya uchunguzi/ukaguzi huo wa pili. Aidha, maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania huwa hawatunzi matokeo ya ukaguzi huo.

### 4.6.2 Utoaji wa taarifa usiojitosheleza wa matokeo ya ukaguzi na ufuatiliaji wa chakula

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania, taratibu za uendeshaji wa ukaguzi wa chakula zinawataka wakaguzi wa chakula kuandaa na kuwasilisha taarifa za ukaguzi. Taarifa hizo za ukaguzi huchukuliwa kama zana mojawapo wakati wa ufuatiliaji inayotumika na idara ya mipango na utawala ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania wanapofanya tathmini ya kaguzi zilizofanyika.

Ripoti ya ufuatiliaji wa ukaguzi wa usimamizi wa ukaguzi na ufuatiliaji wa chakula kwenye viwanda vinavyosindika chakula na vinapoingia bandarini ilionesha kuwa mkataba wa ukaguzi hauruhusu wakaguzi kutoa maoni juu ya maagizo ya awali ya ukaguzi aliyopewa mmiliki wa kiwanda kinachosindika chakula. Aidha, orodha ya ukaguzi haionesha idadi ya maagizo ya awali yaliyotekelezwa au ambayo hayajatekelezwa ili yapewe kipaumbele katika ukaguzi ujao.

## 4.7 Ufuatiliaji na Tathimini Isiyojitosheleza ya Ukaguzi wa Chakula

Ukaguzi wa Ufuatiliaji juu ya ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa toka nje ya nchi ilionesha kuwa Wizara ya Viwanda, Biashara, na Uwekezaji haijaweka viashiria vya utendaji kwa ajili ya kuchunguza utendaji wa Shirika la Viwango Tanzania kwenye shughuli za ukaguzi. Linapokuja suala la kutathmini utendaji wa Shirika la Viwango Tanzania, Wizara inathibitisha tu iwapo fedha zimetumiwa kwa

mujibu wa mpangokazi na kama mikakati imetekelezwa kwa usahihi lakini haigusi kabisa mambo yanayohusu chakula toka nje ya nchi.

Hii ilisababishwa na Wizara kukosa mwongozo wa kuwaongoza wafanyakazi wake kufanya ufuatiliaji na tathmini ya kazi inayofanywa na mashirika yaliyopo chini yake. Viashiria vya ufuatiliaji vilivyopo vilikuwa katika hali ya juu katika kuangalia utendaji wa sekta hiyo. Hii imesababisha Wizara kutofahamu changamoto ambazo zinalikabili Shirika la Viwango Tanzania na wateja/waagizaji wa bidhaa, takwimu, na mambo mengine ya utendaji ambayo yanaweza kutumika kama msingi wa kuboresha utendaji wa Shirika la Viwango Tanzania. Hali hii inaongeza hatari ya upatikanaji wa chakula ambacho si salama nchini.

Pia, iliripotiwa kuwa Shirika la Viwango Tanzania limetengeneza mfumo wa ndani wa ufuatiliaji lakini haijatengeneza zana za ufuatiliaji na mbinu za kutumiwa kwa mujibu wa matakwa ya Mwongozo Namba 17020 (2012) wa Shirika la Kimataifa la Viwango/Tume ya Kimataifa ya Viwango vya Kielektroniki-Ufundi. Kwa hiyo, hakukuwa na taarifa yoyote ya ufuatiliaji na tathmini iliyoweza kuandaliwa kuhusu hali ya ukaguzi. Hata hivyo, kutokana na rekodi ya mkurugenzi juu ya hatua zilizochukuliwa ilibainika kuwa ufuatiliaji wa ndani ulifanyika bila kuwa na viashiria vya utendaji.

Hata hivyo, masuala ya utendaji kama uwepo wa mpangokazi wa ukaguzi, kiwango cha ukaguzi kilichofanyika, idadi ya mapendekezo yaliyotolewa na kutekelezwa, ufuatiliaji kwa wale wanaokiuka, ukamilifu wa ukaguzi, na maoni kwa ajili ya maboresho ambayo ni muhimu kwa ufanisi wa ukaguzi wa bidhaa toka nje ya nchi hayakukaguliwa.

Kutokana na hili kuna uwezekano mkubwa wa kuingiza chakula kilicho chini ya kiwango na kuathiri afya ya wananchi. Hii imesababishwa na ukosefu wa viashiria vya ufuatiliaji na utendaji, ambavyo vinaonesha hatua muhimu za utendaji wa shughuli za ukaguzi na ukosefu wa taratibu zilizowekwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za ukaguzi wa ndani. Ripoti ya ufuatiliaji wa usimamizi wa ukaguzi wa chakula na ufuatiliaji kwenye viwanda vinavyosindika chakula na vinapoingia bandarini ilionesha kwamba hakuna ufuatiliaji na tathmini yoyote iliyofanywa na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania kwenye ofisi zake zote za kanda tano ili kupima utendaji wa shughuli za ukaguzi wa chakula kwenye viwanda vinavyosindika chakula na bandarini. Hii ilisababishwa na kukosekana kwa viashiria vya kutosha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa chakula. Kushindwa kufuatilia utendaji wa shughuli za ukaguzi kwa kulinganisha na malengo ya ukaguzi kuliwanyima Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania fursa ya kujua iwapo inafanya

vizuri au iko nyuma ikulinganishwa na malengo yaliyokusudiwa kwa kipindi husika.

Ripoti ya udhibiti wa usafi katika uandaaji/usindikaji wa nyama ilibainisha kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI haifuatilii utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa katika uzalishaji wa nyama salama kwa umma. Badala yake, TAMISEMI inafuatilia tu shughuli zinazohusiana na uzalishaji wa ngozi za wanyama. Kutokana na hili, TAMISEMI haijui kiwango cha usafi katika mchakato wa uandaaji/uzalishaji wa nyama na hakuna mkakati uliofanywa ili kuleta afya kwa umma.

Pia, iliripotiwa kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jumii, Jinsia, Wazee, na Watoto haisimamii kikamilifu utendaji wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania ili kuhakikisha inasimamia utekelezaji wa usafi katika uzalishaji/uandaaji wa nyama. Vilevile, iliripotiwa kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi haivifuatilii vituo vyake vya kanda vya mifugo ili kuhakikisha machinjio yote katika maeneo yao ya mamlaka yanatambuliwa na kupeleka fomu ya machinjio yenye taarifa za magonjwa ya wanyama kama inavyotakiwa.

Hii imesababishwa na mifumo ya utoaji wa ripoti isiyofaa ambayo ni pamoja na: (a) ripoti kutozingatia usafi wa nyama, (b) kukosekana kwa viashiria muhimu kwa ajili ya kufuatilia utendaji wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania, (c) mamlaka za serikali za mitaa, na vituo vya kanda vya mifugo kutofanya na kutotoa taarifa za ukaguzi, (d) uratibu hafifu kati ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI na wizara za kisekta, (e) wizara kutogawiwa taarifa za ufuatiliaji, (f) ripoti za ufuatiliaji na tathmini kutoelezea mazingira ya uchafu katika mchakato wa uandaaji wa nyama, na (g) ufuatiliaji na uthamini hafifu ya tawala za mikoa kwenye ukaguzi wa chakula.

# SURA YA TANO

## USALAMA KATIKA MAKAZI YA WATU

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya usimamizi wa usalama katika makazi ya watu nchini yaliyotolewa katika ripoti tano za ukaguzi wa ufanisi zilizopita. Matokeo hayo yalihusu vipengele vitano vya usalama katika makazi ya watu ikiwa ni pamoja na usalama dhidi ya moto katika majengo ya umma, afya na usalama mahali pa kazi, utekelezaji wa udhibiti wa uendelezaji wa maeneo ya wazi ya umma, pamoja na mipango-miji.

Mapungufu yaliyobainishwa yalihusu mipango, ukaguzi, uratibu, utoaji wa taarifa za matokeo ya shughuli za usalama, na ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zote zinazozingatia kupunguza hatari zinazohusiana na usalama katika makazi ya watu. Yafuatayo ni madhaifu yaliyo onekana:

### 5.2 Mipango Isiyojitosheleza ya Shughuli za Kudhibiti Usalama katika Makazi ya Watu

Upangaji wa shughuli za kudhibiti usalama katika makazi ya watu ni muhimu kwa ajili ya kuweka mwongozo na kuwezesha uratibu wa shughuli za utekelezaji wa usalama. Shughuli za kutekeleza ni pamoja na ukaguzi na ufuatiliaji na utathmini. Pia, huongeza matumizi bora ya rasilimali maana huwezesha shughuli kutekelezwa kwa wakati na kufikia malengo ya pamoja yaliyotarajiwa. Ripoti tano za ukaguzi wa ufanisi zilibainisha udhaifu unaohusiana na mipango ya shughuli za kuimarisha usalama wa makazi ya watu kama ifuatavyo.

#### 5.2.1 Mipango ilikosa mikakati na miongozo yenye malengo na hatua muhimu zinazoeleweka

Ripoti ya usalama dhidi ya moto katika majengo ya umma ulionesha kuwa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakikuandaa mpangokazi wa ukaguzi wa usalama dhidi ya moto kwenye majengo ya umma. Hii ilionekana katika makao makuu ya Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji na pia katika ofisi zake mikoa mitano iliyotembelewa[13]. Badala yake, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kilifanya ukaguzi wa kila siku kulingana na matakwa ya maofisa wake.

Pia, ripoti hiyo ilionesha kuwa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakikuwa na malengo na miongozo ya kukiongoza katika kukamilisha malengo yake ya kufanya ukaguzi wa usalama dhidi ya majanga ya moto katika majengo ya umma. Hii ilisemekana kuchangia kuongezeka kwa matukio ya majanga ya moto katika majengo ya umma, ambayo yanasababisha kupoteza maisha ya watu na mali.

[13] Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, na Dodoma

Vilevile, ripoti kuhusu udhibiti wa uendelezaji wa maeneo ya wazi ya umma ilibainisha kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI haikuwa na mikakati na mipango inayoeleweka na inayozingatia utekelezaji wa uendelezaji wa maeneo ya wazi yaliyopangwa.

Hii ilisababisha mamlaka za mipango-miji[14] kushindwa kutoa hatimiliki kwa wizara, idara, na wakala wa ardhi na majengo ya umma zilizo chini ya usimamizi wao kwa kuwa haikuwa na miongozo, mikakati, na mipango kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Matokeo yake, maeneo ya wazi yalivamiwa na kutumiwa kwa matumizi tofauti na yaliyokusudiwa.

Hali hii ilihatarisha usalama wa watu ambao walitaka kutumia maeneo hayo kwa ajili ya shughuli za kijamii kama vile michezo mbalimbali mfano mashindano ya riadha, mpira, mafunzo ya mbio, mafunzo ya gofu, ngoma za jadi, shughuli ambazo ni muhimu kwa ajili ya kujenga afya ya wanajamii.

Pia, ripoti ya udhibiti wa athari za mazingira katika sekta ya madini ilionesha kuwa mipango ilikosa malengo ya utekelezaji, viashiria muhimu vya utendaji, pamoja na matokeo yaliyotarajiwa ya utekelezaji. Matokeo yake, mipango ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lilishindwa kushughulikia matatizo ya mazingira katika maeneo ya madini yaliyokuwa na hatari ya kusababisha uchafuzi wa mazingira na yenye athari mbaya kama vile umwagaji wa kemikali za sumu, uchafuzi wa hewa na maji, na uharibifu wa majengo ambayo moja kwa moja huathiri makazi ya watu.

### 5.2.2 Ukosefu wa Mipango-Miji Madhubuti

Ripoti ya usimamizi wa mipango miji ilionesha kwamba kulikuwa na miji mingi ambayo imeendelezwa kiholela. Hii ilidhihirishwa na kuwepo kwa nyumba zilizojengwa katika maeneo hatarishi kama vile kwenye mwambao wa bahari na ziwa, miteremko ya milima, na karibu na vyanzo vya maji au maeneo ya kuhifadhia maji kama mabwawa, sehemu ambazo hazikuwa salama kwa makazi ya watu.

Hii ni kwa sababu asilimia 80 ya miji nchini haikuwa na mpango-miji madhubuti kwa ajili ya kutoa mwongozo wa kupanga matumizi ya ardhi kama vile maeneo ya viwanda, makazi, biashara, mpangilio wa miundombinu, maeneo ya burudani, maeneo ya wazi, na vituo vya umma kwa ajili ya huduma za kijamii kama shule, na vituo vya afya. Uendelezaji wa mipango-miji kiholela umepelekea ongezeko la matukio ya mafuriko kutokana na ujenzi holela ambao huzuia mifumo ya mifereji ya maji ya mvua na kusababisha mafuriko, na hivyo hufanya makazi ya watu kutokuwa salama.

---

14 Ofisi ya Raisi - TAMISEMI, Wizara ya Viwanda, na mamlaka za serikali za mitaa

### 5.2.3 Mipango Isiyozingatia Viashiria vya Hatari

Ripoti ya Mfumo wa Udhibiti wa Mazingira katika Sekta ya Madini ilionesha kwamba mpango wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira halikuweka kipaumbele katika kuzingatia viashiria vya hatari kama vile hatari ya uharibifu wa mazingira, na aina au kiwango cha madhara ya ukiukaji wa sheria za mazingira katika maeneo husika na kwenye makazi ya watu. Ripoti hii ilieleza kuwa kukosekana kwa ripoti za awali za uchunguzi; kanzidata za ukaguzi wa awali zinazoonesha historia ya migodi ya kutofuata taratibu zilizopo; ukosefu wa taratibu zinazoeleweka za mchakato wa uandaaji wa mpangokazi; na uratibu na ushirikianaji duni wa taarifa ndani ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira zilikuwa sababu zilizochangia kutokuwepo kwa mipango yenye viashiria vya hatari katika makazi ya watu.

### 5.2.4 Ugawaji usiojitosheleza wa rasilimali katika kusimamia usalama kwenye makazi ya watu

*Ripoti ya Usalama dhidi ya Majanga ya Moto katika Majengo ya Umma ilionesha kuwa* Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakikugawa kikamilifu rasilimali-fedha na rasilimali-watu kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa usalama dhidi ya majanga ya moto kwenye majengo ya umma na kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa utendaji wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji wakati na baada ya ukaguzi. Ilibainika kuwa mikoa yenye takwimu kubwa za matukio ya majanga ya moto ilikuwa na hatari kubwa ya kuzuka kwa moto. Kwa hiyo, ukaguzi ulitakiwa ufanyike zaidi ili kutambua na kushughulikia maeneo yote ambayo hayakidhi matakwa ya usalama dhidi yamajanga ya moto.

Ripoti ilionesha pia kuwa ugawaji wa wakaguzi haukufanyika kwa usawa, kwani wakaguzi wengi walipelekwa katika mikoa yenye matukio machache ya moto kama ilivyooneshwa katika Jedwali 5.1:

**Jedwali 5.1: Uwiano wa mgawanyo wa wakaguzi kulingana na matukio ya moto katika mikoa mitano iliyotembelewa**

| Mkoa | Idadi ya matukio ya moto | Idadi ya wakaguzi | Uwiano wa matukio ya motopo na idadi ya wakaguzi |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 404 | 140 | 3 |
| Dodoma | 63 | 10 | 7 |
| Mwanza | 135 | 12 | 12 |
| Arusha | 126 | 12 | 11 |
| Mbeya | 69 | 10 | 7 |

**Chanzo**: *Data zilizokusanywa kutoka katika Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kuanzia 2013/14 hadi 2015/16*

Kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 5.1, Mbeya na Dodoma kulikuwa na idadi ndogo ya matukio ya moto, lakini wakaguzi wengi walipangwa maeneo hayo ikilinganishwa na Mwanza na Arusha. Matokeo yake, vikosi vya zimamoto na uokoaji vilishindwa kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa kutosha kwenye majengo ya umma.

Pia, ripoti ilionesha kulikuwa na utoaji wa rasilimali-fedha usiojitosheleza kwa ajili ya ukaguzi na ufuatiliaji wa vikosi vya zimamoto kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali 5.2:

**Jedwali 5.2: Fedha zilizotengwa kwa ajili ya ukaguzi wa majengo na ufuatiliaji wa vikosi vya zimamoto**

| Mwaka wa Fedha | Bajeti Iliyotengwa (Milioni TShs) | Kiasi Kilichotolewa (Milioni TShs) | Asilimia ya Kiasi Kilichotolewa (%) |
|---|---|---|---|
| 2015/16 | 1,617 | 1,215 | 75 |
| 2014/15 | 2,660 | 1,139 | 43 |
| 2013/14 | 2,826 | 912 | 32 |
| 2012/13 | 861 | 821 | 95 |
| 2011/12 | - | - | - |

***Chanzo**: Jeshi a Zimamoto na uokoaji mfumo wa utendaji wa matumizi muhula wa kati kuazia mwaka 2011/12 mpaka 2015/16*

Jedwali 5.2 linaonesha kuwa kwa miaka ya fedha minne (2012/13 hadi 2015/16) asilimia ya fedha zilizotolewa ilikuwa kati ya 32 na 95. Hali ilikuwa mbaya zaidi kwa miaka miwili ya fedha ya 2013/14 na 2014/15 ambayo ni asilimia 32 na 43 tu ya fedha iliyotengwa ndiyo iliyotolewa.

Ripoti ya mipango-miji ilionesha kuwa kuna upungufu wa asilimia 74 ya wafanyakazi kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mipango-miji. Upungufu wa rasilimali-watu umepunguza uwezo wa mamlaka za mipango-miji wa kusimamia utekelezaji wa shughuli za usalama kwenye makazi ya watu. Mipango duni husababisha kutokea kwa mafuriko kutokana na ujezi holela ambao huziba mifumo ya maji ya mvua. Hii hupelekea kuzuka mara kwa mara kwa magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na kuhara hasa wakati wa mvua ambayo huathiri maisha ya watu.

## 5.3 Utekelezaji Duni wa Shughuli za Kuboresha Usalama katika Makazi ya Watu

Utekelezaji wa shughuli zilizolenga kuboresha usalama katika makazi ya watu uliripotiwa kukosa tija. Ripoti nne za ukaguzi wa ufanisi zilionesha mapungufu kama vile ubora wa kazi, ufanisi wa utekelezaji, na mwelekeo wake katika kulinda usalama kama inavyoelezewa kwa kina hapa chini.

### 5.3.1 Shughuli zisizotosheleza za kuboresha usalama katika makazi ya watu

Ripoti ya mipango ya miji iliripoti kuwa mamlaka chache za mipango-miji zilizokuwa na skimu za mipango hazikutekeleza mipango hiyo. Hivyo, matumizi ya ardhi yalibadilishwa. Kwa mfano, maeneo mengi ya viwanda yalibadilishwa kuwa makazi ya watu. Sababu zilizoonyeshwa kwenye ripoti zilijumuisha utekelezaji dhaifu wa sheria wa mamlaka za mipango-miji uliotokana na mwingiliano wa majukumu na mamlaka

katika kazi za mipango-miji na kukosekana kwa uratibu baina ya mamlaka hususani Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, na mamlaka za serikali za mitaa. Matokeo yake, majengo ya makazi ya watu yalijengwa maeneo yanoweza kukabiliwa na mafuriko na hivyo kuhatarisha usalama katika makazi hayo pindi yatokeapo mafuriko kutokana na uwezekano wa watu kupoteza maisha na mali zao.

Ripoti ya Ukaguzi Udhibiti wa Uendelezaji wa Maeneo ya Wazi ya Umma ilionesha kuwa mamlaka za mipango-miji hazikuhimiza utekelezaji wa mipango ya kudhibiti uendelezaji wa maeneo ya wazi ya umma. Hii ilisababishwa na ukosefu wa vipaumbele vya utekelezaji wa udhibiti wa uendelezaji wa maeneo ya wazi ya umma. Matokeo yake, mamlaka za mipango-miji zilishindwa kuimarisha usalama wa miji kwa kukosa mipango-miji mizuri.

Kwa hiyo, jumla ya maeneo ya wazi ya umma 573 kutoka kwenye mamlaka saba zilizotembelewa hazikukaguliwa na mamlaka za mipango-miji husika. Hivyo, asilimia 78 ya maeneo ya wazi ya umma yalivamiwa na kubadilishwa matumizi yake yaliyokusudiwa.

Ripoti hiyo pia ilionesha kuwa kushindwa kufanya ukaguzi kulisababisha mamlaka za mipango-miji kutofahamu maeneo yaliyovamiwa na hivyo kushindwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya wavamizi wa maeneo ya wazi ya umma. Kulingana na ripoti hiyo, hii imesababisha kuwepo kwa mzunguko mdogo wa hewa, ukosefu wa maeneo kwa ajili ya shughuli za kijamii kama mazoezi na burudani, na hivyo kusababisha athari za kiafya katika jamii.

Ukosefu wa vifaa vya usafiri, upungufu wa wafanyakazi, ukosefu wa mpango wa ukaguzi, na ukosefu wa ufadhili wa shughuli za kulinda maeneo ya wazi ya umma viliripotiwa kuwa ni sababu kuu za kuwa na ukaguzi usiotosha wa maeneo ya wazi ya umma.

Zaidi ya hayo, ripoti ya Tathmini ya Athari za Mazingira katika Miradi ya Ujenzi ilionesha kuwa kwa kipindi cha miaka ya fedha kuanzia 2010/11 hadi 2014/15, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lilipitia ripoti za tathmini za athari za mazingira 1,602 kati ya 3,811 katika miradi ya ujenzi iliyosajiliwa. Hii ni sawa na asilimia 42 ya miradi yote kwa wakati huo. Hii inamaanisha kuwa miradi ya ujenzi 2,209 iliyosajiliwa ilijengwa kwenye makazi ya watu bila ya tathmni za athari mazingira kupitiwa.

### 5.3.2 Ukaguzi kutofanyika kama ilivyohitajika

Ripoti ya Usalama dhidi ya Moto katika Majengo ya Umma ilionesha kuwa kwa zaidi ya mwaka mmoja, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakikufanya ukaguzi wa kuangalia usalama dhidi ya moto katika majengo ya umma. Ripoti ilionesha kuwa Kikosi cha Zimamoto na

Uokoaji kilitakiwa kufanya ukaguzi na majaribio ya vifaa vya kinga dhidi ya moto kwa ajili ya kuhakikisha zinakidhi matakwa ya usalama. Hata hivyo, ripoti ilieleza kuwa mazingira ya majengo ya umma mfano majengo ya Chuo Kikuu cha Mzumbe, Tawi la Mbeya, katika Jiji la Mbeya yalikuwa hayajakaguliwa kwa zaidi ya mwaka mmoja, japokuwa majengo hayo yanabeba idadi kubwa ya watu kwa mara moja. Hii inaisharia hatari ya uwepo wa mazingira yasiokidhi matakwa ya usalama dhidi ya moto na pia kuwepo kwa hatari iwapo tukio la mlipuko wa moto litatokea.

Kwa mujibu wa ripoti hii, sababu za kutokuwepo kwa ukaguzi usiotosheleza ni pamoja na ukosefu wa mipango ya ukaguzi na ugawaji usiotosheleza wa fedha, wafanyakazi, pamoja na vifaa.

### 5.3.3 Ubora duni wa shughuli za usalama

Ripoti ya Usalama dhidi ya Moto katika Majengo ya Umma ilionesha kuwa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakikufanya ukaguzi wa kina kubaini udhaifu wa usalama dhidi ya moto katika majengo ya umma.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa majengo ya umma yaliyokaguliwa bado yalikuwa na mapungufu mbalimbali kama inavyoonekana katika Jedwali 5.3:

**Jedwali Na.5.3: Asilimia ya majengo ya umma yaliyokaguliwa na bado yalikuwa na mapungufu**

| Mapungufu ambayo hayakubainishwa wakati wa ukaguzi | Idadi ya majengo yaliyokaguliwa na Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji | Idadi ya majengo yaliyokuwa na Mapungufu | Asilimia ya majengo yaliyokuwa na mapungufu |
|---|---|---|---|
| Mitungi mibovu ya kuzimia moto/mtungi uliokwisha muda wake | 20 | 11 | 55 |
| Ukosefu wa kifaa cha kugundua moshi | 20 | 11 | 55 |
| Uwepo wa vizuizi kwenye milango/njia za dharura za kutokea wakati wa moto | 14 | 1 | 7 |
| Ukosefu wa mipira ya maji ya kuzimia moto | 11 | 7 | 64 |

***Chanzo**: Uchambuzi uliofanywa na wakaguzi kulingana na yaliyoonekana kwenye mikoa iliyotembelewa*

Kama inavyoonekana kwenye Jedwali 5.3, zaidi ya nusu ya majengo yaliyokaguliwa yalionekana kuwa na vifaa vibovu vya zimamoto, vifaa vilivyokwisha muda wake, ukosefu wa vifaa vya kugundua moshi, na kukosekana kwa mipira ya maji ya kuzimia moto. Hii ilitokana na ukosefu wa umakini wa watumishi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji wakati wa ukaguzi. Matokeo yake, wamiliki wa majengo hawakuweza

kuboresha kiwango cha kukidhi matakwa ya usalama dhidi ya moto. Pia, hali hii iliashiria hatari kubwa ya kupoteza mali pamoja na maisha ya watu iwapo mlipuko wa moto ukitokea.

Ripoti ya Tathmini ya Madhara ya Miradi ya Maendeleo kwenye Mazingira ilionesha kuwa mapitio ya ripoti za tathmini ya athari za mazingira katika miradi ya ujenzi haikufanyika kwa ufanisi. Hii ni kwa sababu ripoti hizo hazikuweza kubaini madhara yanayoweza kutokea wakati wa ujenzi wa miradi na kuanisha hatua za kuchukua ili kupunguza athari hizo. Ripoti hiyo ilitoa mfano wa yadi ya magari ya mradi wa mabasi yaendayo haraka iliyojengwa Jangwani, eneo ambalo hukabiliwa na mafuriko hasa wakati wa mvua kubwa. Matokeo yake, ilisababisha uharibifu wa makazi ya watu na upotevu wa mali.

### 5.3.4 Ukaguzi haukujikita katika maeneo yenye hatari kubwa

Japokuwa ukaguzi wa usalama dhidi ya moto uliofanywa na Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji ulipaswa kuangalia zaidi majengo ya umma yenye idadi kubwa ya watu; majengo yaliyo kwenye hatari kubwa ya kutokea kwa moto; majengo yanayotumika kwa kiwango kikubwa; na kuzingatia aina ya vifaa vilivyohifadhiwa kwenye jengo husika, ripoti ya usalama dhidi ya moto ilibaini kuwa mambo haya hayakuzingatiwa wakati wa kuchagua majengo ya kukagua. Kwa mujibu wa ripoti hii, majengo yaliyokuwa yanaangukia ndani ya makundi haya kama Chuo Kikuu cha Mzumbe – Tawi la Mbeya hayakukaguliwa, hali ambayo inayafanya majengo kuwa katika hatari ya moto.

Ripoti hiyo ilionesha kuwa kutofanyika kwa ukaguzi wa kutosha kulichangia ongezeko la idadi kubwa ya matukio ya moto katika majengo ya umma. Kwa mfano, kwa kipindi cha kati ya mwaka 2011/12 na 2015/16 katika mikoa mitano iliyotembelea, jumla ya watu 44 walipoteza maisha yao, na 80 walijeruhiwa kutokana na majanga ya moto. Ripoti hiyo ilionesha kuwa ndani ya kipindi hicho, vifo 40 na majeruhi 38 yaliripotiwa katika mkoa wa Dar es Salaam peke yake.

Ukaguzi wa usalama dhidi ya moto kwenye majengo ya umma ulielekezwa sana kwenye maeneo yaliyokuwa na uhakika wa kukusanya ada za ukaguzi na maeneo ambayo yalionekana kusita kulipa ada za ukaguzi hayakupewa kipaumbele hata kama majengo yalikuwa na hatari kubwa kiusalama dhidi ya moto.

Ripoti ya ukaguzi kwenye migodi ya madini ilionesha kuwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lilifanya ukaguzi wa kudhibiti uharibifu wa mazingira kwenye migodi mikubwa ambayo ina teknolojia kubwa za kuzuia uchafuzi wa mazingira ukilinganishwa na migodi midogo. Ripoti hii ilionesha kuwa kwa mwaka 2013/14, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lilikagua migodi 12. Kati ya hiyo, 11 ilikuwa ni migodi mikubwa na mmoja ulikuwa ni mgodi mdogo. Wakati athari katika

mazingira kwenye migodi midogo ilionekana wazi ardhini (mashimo, vumbi yenye vyuma na uchafuzi wa maji) na hata matumizi ya kemikali zenye sumu katika migodi hiyo, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira halikutoa kipaumbele kwenye migodi hiyo.

## 5.4 Usajili Usiotosheleza

Usajili usiotosheleza ulitajwa kuathiri shughuli zinazohusiana na usalama katika makazi ya watu. Ripoti tatu za ukaguzi wa ufanisi zilionesha mapungufu yafuatayo.

### 5.4.1 Maeneo ya Wazi ya Umma katika Miji Hayakusajiliwa vya Kutosha

Ripoti ya Udhibiti wa Uendelezaji wa Maeneo ya Wazi ya Umma ilionesha kuwa mamlaka sita za mipango-miji kati ya saba zilizokaguliwa, zilikuwa hazijaanza taratibu za kusajili maeneo ya wazi licha ya kukummbushwa mara nyingi na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Hivyo, maeneo ya wazi ya umma 573 yaliyopo kwenye mamlaka za mipango-miji saba zilizo kaguliwa hayakuwa yamesajiliwa na hayakuwa na hatimiliki. Hii ilitoa mwanya kwa watumishi na wananchi wasiokuwa waaminifu kushiriki katika kugawa na kubadili matumizi ya ardhi kinyume na madhumuni yaliyokusudiwa. Matokeo yake, watu walishindwa kupata maeneo kwa ajili ya shughuli za kijamii kama vile burudani na michezo, ambazo ni shughuli muhimu kwa ajili ya kujenga usawa katika jamii.

### 5.4.2 Baraza la taifa la usimamizi wa mazingira halikufanya usajili wa kutosha wa migodi ya madini na ujenzi wa miradi ya maendeleo

Usajili wa migodi ya madini na ujenzi wa miradi ya maendeleo ni muhimu sana katika kupanga shughuli zinazolenga kudhibiti usalama katika makazi ya watu na mazingira. Kwa hiyo, ni muhimu kutathmini athari zote mbaya na nzuri zinazoweza kutokea kwenye mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi ili kupendekeza hatua za kupunguza athari kubwa na mbaya. Athari hizi ni kama vile umwagaji wa majitaka; uchafuzi wa mazingira unaotokana na vumbi chafu kutokana na shughuli za madini linaloweza kuathiri afya kwa watu wanaoishi karibu na mgodi; mlipuko wa baruti kutoka kwenye migodi unaoweza kusababisha mipasuko ya nyumba za watu; na usambazaji holela wa uchafu na gesi kama moshi mzito na chembechembe za uchafu.

Ripoti ya Tathmini ya Athari za Mazingira ya Ujenzi wa Miradi ya Maendeleo ilionesha kuwepo kwa upungufu wa usajili wa ujenzi wa miradi ya maendeleo, ambapo ni miradi 3,811 tu kati ya 15,266 sawa na asilimia 25 ndiyo iliyokuwa imesajiliwa na Baraza la Taifa la Mazingira kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2010/11 hadi 2014/15. Hii ilitokana na kukosekana kwa mfumo wa kufuatilia taarifa za mapendekezo ya miradi ya ujenzi iliyosajiliwa na Bodi ya Usajili wa

Makandarasi. Hivyo, ujenzi wa miradi mingi ya maendeleo ilitekelezwa bila kujali athari zake katika mazingira.

Vilevile, ripoti hii ilionesha kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinatoa vibali vya ujenzi bila kuwa na ushahidi wa vyeti vya tathmini ya athari za mazingira au maamuzi yaliyotolewa. Ripoti ilionesha kuwa mamlaka za serikali za mitaa zilitoa leseni za biashara bila kuthibitisha iwapo tathmini ya athari za mazingira imefanyika. Hii ilisababishwa na udhaifu wa ushirikiano baina ya mamlaka za serikali za mitaa na Baraza la Taifa la Mazingira.

Hali kama hii ilionekana pia katika ripoti ya Mfumo wa Kudhibiti Athari za Mazingira katika sekta ya madini ambapo Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira halikufahamu idadi ya migodi ya madini iliyosajiliwa nchini. Hii ilitokana na ukosefu wa mfumo mzuri wa kushirikishana taarifa kati ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na Wizara ya Nishati na Madini. Kwa sababu hiyo, ripoti hiyo ilionesha kuwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lilishindwa kuwa na mpango-kazi mzuri wa kuhakiki usalama na hatimaye kusababisha hatari ya uharibifu wa mazingira na makazi ya watu.

## 5.5 Uratibu Usiotosheleza wa Shughuli za Kuhakikisha Usalama katika Makazi ya Watu

Ripoti mbili za ukaguzi wa ufanisi zilionesha mapungufu katika suala la uratibu wa wadau mbalimbali wanaohusika katika kuhakikisha usalama kwenye makazi ya watu kama inavyoelezewa hapa chini.

Ripoti ya Tathmini ya Athari za Mazingira kwenye Miradi ya Maendeleo ilionesha kuwa maelezo ya miradi 19 kati ya 214 ndiyo yaliyowasilishwa katika mamlaka za serikali za mitaa, tawala za mikoa, na wizara husika kwa ajili ya kufanyiwa tathmini; ikilinganishwa na idadi ya maelezo ya miradi yaliyopokelewa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira.

Ripoti hiyo ilionesha kwamba katika miradi 38 iliyoteuliwa kutoka katika kanda tano za Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, hakuna maelezo yoyote yaliyowasilishwa katka mamlaka za serikali za mitaa, sekretarieti za mikoa, na katika ofisi za kanda za Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira. Vilevile, ripoti hiyo ilionesha kuwa katika miradi 214 iliyotekelezwa kwenye mamlaka za serikali za mitaa kumi na moja (11), yalipatikana maelezo ya miradi kumi na tisa tu (19) toka halmashauri tano (5).

Kwa upande wa ripoti ya tathmini ya athari za mazingira na ripoti ya ukaguzi wa athari za mazingira, ilionekana kuwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira halikupeleka nakala za ripoti kwa wadau wake na katika ofisi zake za kanda. Hii ni kinyume na Kanuni ya 23 (1)

ya Tathmini ya Athari Mazingira na Kanuni za Ukaguzi wa Athari za Mazingira za mwaka 2005 ambazo zinalitaka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kuwasilisha nakala za tathmini ya athari za mazingira na ripoti ya ukaguzi wa athari za mazingira kwa kila idara za Wizara na mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika na mradi huo, na kuzijulisha na kuzitaka zitoe maoni ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupokea taarifa husika.

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2010/11 hadi 2014/15, iliripotiwa kuwa jumla ya ripoti za tathmini ya athari za mazingira na ripoti ya ukaguzi wa athari za mazingira 153 zilipelekwa kwa wadau, lakini hakukuwa na kumbukumbu iliyodhihirisha kuwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lilipokea maoni kutoka kwa wadau waliopatiwa taarifa hizo ili wazipitie na kutoa maoni. Hii ilikuwa hasa kwenye mamlaka za serikali za mitaa za mkoa wa Dar es Salaam.

Vilevile, ripoti hiyo ilibainisha kwamba kutowashirikisha wadau kwenye kupitia taarifa za ripoti za tathmini ya athari za mazingira na ripoti ya ukaguzi wa athari za mazingira hakutoi uhakika kwamba mradi huo umezingatia masuala ya mazingira na usalama wa wadau wote wanaoguswa na mradi huo. Hali hii ilisababisha utekelezaji wa miradi bila kuzingatia matakwa ya mazingira na usalama wa watu wanaoishi karibu na eneo la mradi.

Zaidi ya hayo, iliripotiwa pia kuwa kutohusisha kwa wadau kulisababisha mgongano wa maamuzi baina ya wadau kulingana na maoni yao kuhusu matokeo ya ripoti ya tathmini ya athari za mazingira na ripoti ya ukaguzi wa athari za mazingira. Ripoti hiyo ilitoa mfano wa cheti cha tathmini ya athari za mazingira na ripoti ya ukaguzi wa athari za mazingira kilichokataliwa mwaka 2014.

Hii ni baada ya rufaa dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na Waziri wa Maji kwa Waziri wa Mazingira baada ya utoaji wa cheti cha tathmini ya athari za mazingira na ripoti ya ukaguzi wa athari za mazingira kwa ajili ya mapendekezo ya Kituo cha Mabasi cha Igumbilo katika Manispaa ya Iringa. Hii ilitokana na hoja iliyotolewa na Waziri wa Maji kwamba mradi huo uliopendekezwa ungeongeza uchafu kama vile mafuta machafu katika Mto Ruaha eneo ambalo kuna mtambo ambao hauna uwezo wa kuchuja kaboni katika maji.

Vilevile, ripoti ya Mipango-miji iliripoti kuwa mamlaka za mipango-miji hazikuwahusisha wadau wengine kama vile Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, taasisi za umma zinazohusika katika utoaji wa huduma za msingi kama vile maji, umeme, na barabara wakati wa maandalizi na utekelezaji wa mipango ya skimu za mipango-miji.

Iliripotiwa pia kuwa kushindwa kuhusisha wadau hawa muhimu kulizuia utoaji wa huduma zinazohitajika kama vile zimamoto na uokoaji, maji, na umeme kwa sababu baadhi ya mahitaji ya miundo hayakuzingatiwa. Kwa hiyo, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hushindwa kutoa huduma za msingi kwa kiwango cha kutosha kwa jamii na hivyo usalama wao unahatarishwa hasa ikiwa kuna matukio ya milipuko ya moto.

## 5.6 Ufuatiliaji usiotosheleza wa shughuli za kuhakikisha usalama katika makazi ya watu

### 5.6.1 Ukosefu wa viashiria vya ufuatiliaji

Ripoti ya Mipango-miji ilionesha ukosefu wa viashiria au zana za ufuatiliaji kwa ajili ya kupima utendaji katika kufikia malengo ya mipango-miji. Matokeo yake, ripoti za ufuatiliaji zilizoandaliwa zilikuwa na taarifa chache. Ripoti hiyo ilieleza kuwa ripoti za ufuatiliaji zilionesha changamoto pekee zinazozikabili mamlaka za mipango-miji badala ya kuonesha ni kwa kiasi gani idara hizo zimeweza kufikia malengo kama mwongozo wa skimu ya upangaji unavyoelekeza.

Ripoti hiyo pia ilionesha kuwa mamlaka zote saba za mipango-miji zilizokaguliwa hazikufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa skimu za upangaji isipokuwa Mji wa Babati. Kulingana na taarifa hiyo, upungufu wa ufuatiliaji ulisababisha ujenzi holela wa makazi ya watu ambao ulichangia kukosekana kwa huduma katika makazi mapya na hivyo kuweka hatarini maisha ya wakazi.

### 5.6.2 Ufuatiliaji haukufanyika kwa kiwango cha kuridhisha

Ripoti ya Mipango-miji ilieleza kuwa taratibu zilizotumika kufuatilia shughuli zilizofanywa na mamlaka za mipango-miji hazikuweza kutoa taarifa za kutosha kuiwezesha Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuelewa kiwango cha utekelezaji wa maagizo au miongozo iliyoyatoa. Pia, iliripotiwa uwepo wa kiwango kidogo cha majibu ya taarifa zilizohitajiwa za mwelekeo wa mikakati iliyoandaliwa na Idara ya Maendeleo ya Miji ili kuhakikisha kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI inakuwa na taarifa ya hali halisi ya utekelezaji wa maagizo na miongozo iliyoitoa.

Kuhusu ufuatiliaji wa shughuli za mamlaka za serikali za mitaa, ripoti hiyo ilionesha kwamba shughuli zinazofanywa na Idara ya Maendeleo ya Miji zilipewa kipaumbele kidogo. Matokeo yake, ufuatiliaji wa shughuli zilizofanywa na mamlaka za mipango-miji zilikosa miongozo na haikusimamiwa. Hii ilitokana na Ofisi Rais - TAMISEMI kutojua idadi halisi ya maeneo ya wazi ya umma yaliyotengwa.

Ripoti ya Usalama dhidi ya Moto katika Majengo ya Umma ilionesha kuwa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji nchini hakikufanya ufuatiliaji wa kutosha wa vikosi vya zimamoto na uokoaji vya mikoa katika kuhimiza utekelezaji wa shughuli za usalama. Hii ni kwa sababu Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakikuwa na mpango wa ufuatiliaji na uhakiki wa utendaji na mfumo wa kufuatilia utendaji wa vikosi vya zimamoto na uokoji vya kanda katika majukumu waliyopewa.

Vilevile, iliripotiwa kukosekana kwa mpango wa ufuatiliaji. Badala yake, ofisi za zimamoto za mikoa zilifanyiwa ufuatiliaji kwa kutumia ripoti za taarifa za shughuli zao za kila siku na pale zilipotembelewa na maofisa kutoka makao makuu. Ripoti hiyo ilionesha kuwa huu si ufuatiliaji wa ufanisi kwani hautoi fursa ya kumtathmini kila mmoja kulingana na kiwango alichotarajiwa kufikisha kulingana na mipango.

Ukosefu wa mpango wa ufuatiliaji umesababisha Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kushindwa kusimamia vikosi vya zimamoto katika utekelezaji wa shughuli zao. Vilevile, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakijafanya juhudi za kutosha katika kufuatilia utendaji wa kuhimiza usalama dhidi ya moto kwenye majengo ya umma.

### 5.6.3 Uwasilishaji usiotosheleza wa taarifa za shughuli za kuboresha usalama katika makazi ya watu

Ripoti ya Mipango-miji ilibainisha kuwa mamlaka za mipango-miji hazikutoa taarifa kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi; na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhusu utekelezaji wa mpango/ skimu ya uendelezaji wa miji. Vilevile, Idara ya Mipango-miji haikufanya ufuatiliaji wa mwelekeo wa utekelezaji wa mipango.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa hapakuwa na utaratibu rasmi wa utoaji wa taarifa ulioanzishwa na TAMISEMI wa kufuatilia maendeleo ya mara kwa mara ya shughuli za mipango-miji. Ripoti ziliwasilishwa TAMISEMI pale tu zilipohitajika. Vilevile, ripoti hiyo ilionesha kuwa baadhi ya mamlaka za mipango-miji zilizotembelewa hazikufahamu uwepo wa idara mpya ya mipango-miji pamoja na kazi zake jambo lililoashiria kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI haijafanya ufuatiliaji wa kutosha katika mamlaka za mipango-miji. Hii inaonesha kuwa kuna udhaifu katika ufuatiliaji wa utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa na kuhakikisha uwajibikaji hususani katika shughuli za mipango-miji.

Pia, ilieleza kuwa maofisa watendaji-kata hawakufanya kazi zao kama ilivyotakiwa kwakuwa hawakutoa ripoti iliyohusu masuala ya mipango-miji. Hii ilisababisha maofisa watendaji-kata kutojaza rejesta zilizotolewa na pia hawakufanya ufuatiliaji wa maendeleo yaliyofanywa na wananchi katika maeneo yao ya mamlaka ili kuhakikisha kwamba walifuata viwango na kanuni.

Ripoti ya Maeneo ya Wazi ya Umma ilionesha kuwa Wizara ya Ardhi haikupokea taarifa ya mwelekeo wa utekelezaji wa mpango kabambe na mambo mengine yaliyohusu vibali vya ujenzi, ulinzi wa maeneo ya wazi ya umma, na mabadiliko ya matumizi ya ardhi.

Ripoti ya Usalama dhidi ya Moto katika Majengo ya Umma nayo ilionesha kuwa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji nchini kilitakiwa kupima utendaji na kutoa maoni yanayofaa kwa wahusika ili kuhimiza maboresho na kuhakikisha usalama dhidi ya milipuko ya moto.

Hivyo, ilipaswa mara ukaguzi unapofanyika, taarifa ya matokeo na mapendekezo ya ukaguzi itolewe kwa wakati kwa taasisi zilizokaguliwa ili ziweze kuchukua hatua za marekebisho ili kuleta maboresho.

Hata hivyo, ripoti ilibaini kuwepo kwa ucheleweshaji wa utoaji wa ripoti ya ukaguzi kwa wamiliki wa majengo. Ingawa matokeo na mapendekezo ya ukaguzi yalipaswa yatolewe kwa wamiliki wa majengo ya umma kati ya siku tatu hadi saba mara baada ya kukamilika kwa ukaguzi, ripoti 7 kati ya 11 za ukaguzi zilitolewa baada siku saba kumalizika. Hii ilitokana na ukweli kwamba Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakikuweka kipaumbele katika kutoa taarifa za ukaguzi na kufanya jitihada za kutosha ili kuhakikisha taarifa za ukaguzi zinawafikia wamiliki na / au watumiaji wa majengo ya umma.

### 5.6.4 Utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa ajili ya kuboresha usalama katika makazi ya watu

Ripoti ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ilionesha kwamba taasisi zilizokaguliwa[15] zimeweza kuchukua hatua za kuboresha usalama katika makazi ya watu hasusani katika maeneo ya kazi.

Ripoti hiyo ilionesha kuwa mapendekezo 20 kati ya 27 (sawa na asilimia 74) yaliyotolewa kwa taasisi zilizokaguliwa yalitekelezwa kikamilifu kama ilivyotakiwa. Mapendekezo 6 kati ya 27 (sawa na asilimia 22) yalitekelezwa kwa kiasi, na pendekezo 1 kati ya 27 (sawa na asilimia 4) halikutekelezwa kabisa.

Kulingana na ripoti hii ya ufuatiliaji, Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira ya Vijana, na Watu Walemavu ilifanya meboresha yafuatayo.

15 Ofisi ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira ya Vijana, na Walemavu (PMO-LYED)

Ripoti hiyo ilibainisha kuwa mwaka 2016, Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi iliweza kuanzisha sheria ndogondogo mpya, ambazo ziliweza kuipa nguvu zaidi ya Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya kutoa faini kwa makosa ya ukiukaji wa kanuni za usalama mahali pa kazi. Kwa mujibu wa ripoti hii, sehemu za kazi 22 zilishitakiwa kwa kushindwa kufanya usajili kwa mwaka 2014/2015 na nyingine 9 kwa kushindwa kulipa ankara ndani ya muda ulitengwa.

Maboresho mengine yaliyofanywa na Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi kama ilivyobainishwa katika ripoti ni pamoja na uimarishaji wa ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara. Kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania, Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi imeweza kuandaa viwango vya vumbi la saruji; vumbi la pamba; kiwango cha joto; na kiwango cha mwanga na mionzi ya *ionizing* (lighty intensity and ionizing radiation). Pia, Mamlaka imefanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kulingana na mapungufu yaliyoonekana na kuyafanya yawe ya lazima katika kozi kama vile huduma ya kwanza. Zana za ufuatiliaji ziliandaliwa na kuanza kutumika, ikiwa ni pamoja na ziara za ufuatiliaji kwenye kanda zinazosimamiwa na makao makuu ya Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

Hata hivyo, ripoti hiyo ilionesha kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi haikuweza kuandaa mkakati unaotekelezeka wa kutambua na kusajili maeneo yote ya kazi ambayo hayajasajiliwa. Haikuandaa pia mwongozo wa kufanya ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi. Vilevile, Mamlaka haikutoa kipaumbele na kukamilisha ukaguzi katika maeneo ya kazi yaliyokuwa na viashiria vikubwa vya hatari ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali.

Ripoti hii pia ilionesha kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira, na Walemavu haikuweza kuandaa mipango ya afya na usalama mahali pa kazi katika ngazi ya kitaifa. Vilevile, Wizara haikuweza kuandaa mpango wa ufuatiliaji na tathmini ya usalama na afya mahali pa kazi.

## SURA YA SITA

## HITIMISHO

### 6.1 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho kutoka kwenye mapitio na tathmini ya hoja zilizotoka kwenye ripoti kumi za kaguzi za ufanisi zilizotumika kwenye ripoti hii ya jumla.

### 6.2 Hitimisho la Jumla

Kwa ujumla, ripoti zilitambua juhudi za serikali katika usimamizi na utekelezaji wa taratibu za usalama katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, masuala yaliyobainishwa na ripoti za ukaguzi yamepelekea kuhitimisha kwamba serikali haijaweka mkazo wa kutosha katika usimamizi na udhibiti wa usalama katika maeneo ya uchukuzi, makazi ya watu, na kwenye uandajia/uzalishaji na uingizaji wa chakula nchini. Mapungufu haya yanasababishwa na ukosefu wa mbinu zinazozingatia viashiria hatarishi katika kupanga na kutekeleza mikakati ya shughuli za kusimamia usalama.

Mikakati hiyo ni pamoja na usimamizi wa sheria na viwango va usalama, usajili, ukaguzi, na utoaji wa taarifa na ufuatiliaji wa matokeo ya kaguzi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoza faini kwa wanaoshindwa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa. Eneo lingine linalohitaji kuboreshwa ni uratibu na ufuatiiaji na tathimini ya wetendaji wanaohusika na usalama.

### 6.3 Hitimisho Maalumu

#### 6.3.1 Mfumo wa vihatarishi haikutumika kikamilifu katika kupanga na kutekeleza mikakati ya shughuli za kusimamia usalama

Kimsingi, taasisi zilizokaguliwa hazikutumia kiufanisi mfumo wa kuzingatia viashiria hatarishi katika kupanga na kutekeleza mikakati ya shughuli za kudhibiti usalama. Miongoni mwa sababu kuu ni ukosefu wa mfumo wa usimamizi wa viashiria vya vihatarishi uliowekwa katika mchakato na mikakati inyotumiwa na taasisi za serikali katika kukabiliana na hatari zinazohusiana na usalama. Hii inazuia ugawaji bora wa rasilimali za serikali ambazo ni rasilimali-watu na fedha katika kusimamia usalama.

Kwa mfano, hatua za usalama zilizotumiwa katika kukabiliana na ajali katika usafiri wa majini na barabarani hazikuzingatia masuala ya hatari. Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini na Jeshi la Polisi Tanzania halikutumia mbinu za kuangalia viashiria hatari katika kupanga na kutekeleza ufuatiliaji wa meli na mienendo ya manahodha.

Udhaifu kama huo ulibainika pia katika usalama wa chakula ambapo Shirika la Viwango Tanzania na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania ilitoa vipaumbele sawa kwa ukaguzi aina zote za chakula kinachotoka nje ya nchi na kinachosindikwa hapa nchini bila kujali aina na ukubwa wa hatari zinazohusiana na shughuli hizo au chakula chenyewe.

Pia, katika makazi ya watu, hali hiyo ilionekana katika kufanya ukaguzi wa makazi na usalama wa moto ambapo vigezo vya uhatarishi havikupewa kipaumbele. Vilevile, shughuli za mipango-miji zilikosa kipaumbele katika kusimamia uendelezaji wa maeneo ya wazi ya umma na kuyaacha katika hatari ya kuvamiwa.

Miongoni mwa mifano michache inayoonesha hali hii ilikuwa ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchikavu na Majini, ambayo ilishindwa kuaanda mchoro unaoonesha maeneo hatarishi majini. Mbali na kutokutumia mbinu ya kuzingatia kiwango cha vihatarishi katika ugawaji wa rasilimali-watu, ugawaji wa wachunguzi ambao wana wajibu wa kuangalia masuala ya usalama haukuendana na ukubwa wa kazi.

Matokeo yake, katika mwaka wa fedha 2015/16 Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilifanya kaguzi 684 wakati kulikuwa na meli ndogo 15,148 jijini Mwanza kwa mujibu wa Sensa iliyofanyika mwaka 2012. Hii ina maana kwamba karibu asilimia 95 ya meli ndogo zilizokuwa zinazafanya kazi Mwanza hazikukaguliwa. Hii ilichangia hatari zaidi katika sekta nzima ya usafiri wa majini kwa kuwa kutokukagua meli hizo kunaathiri maandalizi ya mfumo wa tathmini ya viwango vya vihatarishi ambao ni muhimu katika mfumo wa usimamizi wa usalama wa usafiri wa majini.

### 6.3.2 Viwango vya usalama hazikutekelezwa kwa ufanisi

Bila kujali kuwepo kwa sera ya usalama na sheria, taasisi za serikali zinazohusika katika kutekeleza sheria na viwango vya usalama, sheria na viwango hivyo havikuwa na ufanisi. Mara nyingi, usajili na ukaguzi wa usalama haukufanyika vya kutosha kuhakikisha usalama katika chakula, usafirishaji, na makazi ya watu kwakuwa usajili na ukaguzi haukufanyika kwa kiwango cha kutosha.

Pia, matokeo ya ukaguzi hayakuwekwa kwenye maandishi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi haukufanyika. Zaidi ya hayo, kulikuwa na utozaji usiotosheleza wa faini kwa wakosaji.

Katika maeneo yote matatu, yaani usafiri, chakula, na makazi ya watu, ukaguzi haukufanyika vya kutosha. Kwa mfano, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilishindwa kusajili meli ndogo. Matokeo yake, asilimia 50 ya meli ndogo zilizokuwa zinafanya shughuli zake Tanzania Bara hazikusajiliwa.

Wakala wa Barabara Tanzania haukusimamia vya kutosha viwango vya ubora wa barabara nchini hususani ufungaji wa alama na thamani za barabarani. Kwa mfano, alama za barabarani, reli kingamo za barabarani, na mistari ya barabarani iliyowekwa ilikuwa chini ya kiwango. Kwa kuongezea, baadhi ya alama na samani za barabarani zilizokosekana kabisa hazikufanyiwa kazi ili kuhakikisha zinakuwepo. Kukosekana kwa alama na samani za barabarani kungeweza kusababisha kutokea kwa ajali za barabarani.

Ukaguzi unaofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania; na mamlaka za serikali za mitaa haukufanyika kwa ufanisi na ufasaha ili kusimamia usafi kwenye machinjio.

Hii ilibainishwa na uwepo wa asilimia 98 ya machinjio yanayofanya kazi bila kusajiliwa. Vilevile, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakikufanya ukaguzi wa kutosha wa usalama wa moto katika majengo ya umma. Kuchelewa kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kuandaa mawanda na hadidu za rejea kuliathiri zaidi ya nusu ya miradi ya maendeleo iliyokaguliwa.

Katika kipindi kuanzia mwaka wa fedha 2011/12 hadi 2015/16, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini ilitoza faini asilimia 1.85 tu ya wale walioshindwa kufuata sheria na viwango vya usalama wa usafirishaji majini na nchikavu. Vilevile, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakikutoza faini kwa wamiliki wa majengo ya umma ambao hawakukidhi matakwa ya usalama dhidi ya moto kama inavyotakiwa na Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Namba 14 ya Mwaka 2007 na kanuni zake.

Pia, mfumo wa utekelezaji wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania uliruhusu kuendelea kuwachukulia hatua wakiukaji wa mara kwa mara wa sheria na kanuni. Hata hivyo, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania ni mara chache sana imekuwa ikitoza faini kwa wakiukaji wanaojirudia. Kwa sababu hiyo, viwanda vya usindikaji na waagizaji wa chakula toka nje ya nchi vinapata motisha kidogo ya kuboresha mchakato kwa sababu hakuna madhara makubwa kwa kukiuka mara kwa mara matakwa ya usalama wa chakula.

### 6.3.3 Uratibu duni wa taasisi za serikali katika utekelezaji wa shughuli za usalama

Taasisi za serikali zinazojihusisha na kuhakikisha usalama katika usafirishaji, chakula, na makazi ya watu hazikuandaa na kuoanisha mifumo yao ya udhibiti wa usalama ili kuhakikisha hatari zote za usalama ndani ya maeneo yao zinashughulikiwa kwa ufanisi.

Mara nyingi, ukaguzi ulibaini kuwa usalama hauonekani kwa ujumla na wadau tofauti ndani ya serikali. Kulingana na mamlaka ya kila mdau, kuna hatari ya kuingiliana katika vipaumbele vya masuala ya usalama kama vile kuboresha mikakati ya usalama miongoni mwa wadau wanaofanya kazi katika sekta moja kama vile ukaguzi wa chakula unaofanywa bandarini.

Kwenye usafirishaji, uratibu wa Jeshi la Polisi Tanzania wa masuala ya usalama katika sekta ya usafiriashaji haujitoshelezi pamoja na kwamba wote wanasimamia sekta moja na utendaji wao unategemeana. Kwa mfano, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano; Wakala wa Barabara Tanzania; na Jeshi la Polisi la Tanzania hawapeani taarifa kuhusu usalama barabarani.

Hivyohivyo kwenye makazi ya watu, uratibu ulikuwa miongoni mwa changamoto inayoyowakumba wadau katika sekta hii. Ilibainika kuwa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji haishirikishwi na mamlaka ya serikali za mitaa kwenye mchakato mzima wa upitishaji wa michoro ya nyumba ili kuhakikisha nyumba zote zinazojengwa zinakidhi matakwa ya usalama dhidi ya moto.

Pia, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira halijawashirikisha vya kutosha wadau mbalimbali katika shughuli zake. Wadau hao ni kama vile maofisa usimamizi wa mazingira katika kufanya mapitio ya miradi. Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira halikuhakikisha wakaguzi wa manzingira wa kutosha wanateuliwa kwenye mamlaka za serikali za mitaa wakati mamlaka hizo zina wataalamu wenye sifa hizo za kuteuliwa.

Hii insababisha upungufu mkubwa (asilimia 92) wa wakguzi wa mazingira. Pia, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira halipeleki taarifa za tathmini ya athari za mazingira na uchambuzi wa athari za mazingira katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Kitengo cha Uratibu wa Kisekta). Matokeo yake, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inakosa fursa ya kufanya uchambuzi wa athari za mazingira kwenye maeneo yao ya utawala.

Kwa upande mwingine, wakati wa uandaaji wa mipango-miji, hakukuwa na ushirikishaji wa mashirika/taasisi za serikali zilizopewa jukumu la kutoa huduma za msingi kama maji, umeme, na barabara wakati wa uandaaji wa mipango kabambe licha ya ukweli kwamba taasisi hizo zinafanya kazi muhimu sana wakati wa utekelezaji. Hii husababisha serikali kuingia gharama kubwa zinazohusiana na uhamishaji wa miundombinu ambayo ingeweza.

### 6.3.4 Wizara zinazohusika hazifanyi ufuatiliaji wa kutosha wa utendaji wa taasisi za usalama zilizo chini yao

Ufuatiliaji na tathmini ya mikakati ya usalama katika kushughulikia hatari na utendaji wa taasisi inayohusika haujitoshelezi. Hii ni kwa sababu mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ulioandaliwa kwa ajili ya kupima utendaji na matokeo ya mikakati iliyowekwa haujatoa majukumu, malengo, viashiria vya utendaji, pamoja na kuweka mfumo wa utoaji wa taarifa ili ufuatiliaji na tathmini iwe na ufanisi na tija.

Kukosekana kwa mfumo kumeathiri utunzaji wa taarifa za matokeo au maendeleo yaliyofanyika ikilinganishwa na rasilimali zilizotumika katkia mikakati mbalimbali ya usalama. Hali hii inaathiri ufanisi kwa kutumia uzoefu wa awali na muda uliotumika kuchukua hatua kwa ajili ya maboresho.

Katika maeneo yote matatu, hapakuwa na mfumo sahihi wa kuzuia na kurekebisha maamuzi ya pamoja yaliyofanyika. Kwa mfano, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Mambo ya Ndani hazifuatilii utendaji wa Wakala wa Barabara Tanzania; Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini; na Jeshi la Polisi Tanzania kuhusu mambo ya usalama barabarani, majini, na ukaguzi wa magari kwa ajili ya kuboresha usalama barabarani na majini.

Ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa bidhaa za chakula, pamoja na usimamizi wa usafi haukufanyika vya kutosha. Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na Wizara ya Afya ziliandaa mpango wa ufuatiliaji na tathmini lakini hazikufanya ufuatiliaji na tathmini ya usimamizi wa usafi.

Wizara ya Afya ilikosa mpango madhubuti wa ufuatiliaji wa utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania katika kutekeleza hali ya usafi kupitia ukaguzi. Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania haikusimia shughuli za ukaguzi na usajili wa machinjio kwa mamlaka za serikali za mitaa.

Aidha, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania haikufuatilia kwa ufanisi na kusimamia utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa licha ya kuwapa majukumu yake. Kwa njia hiyo, wizara zinazohusika na afya na mifugo zilikosa mfumo wa utoaji wa taarifa unaoeleweka na unaofanya kazi kuhusu hali ya usafi kwenye machinjio. Matokeo yake, miundombinu mingi ya machinjio ilionekana kuwa katika hali ambayo si rafiki kwa usafi.

Aidha, katika makazi ya watu, ufuatiliaji wa vituo vya zimamoto na uokoaji haukufanyika kwa wakati ili kubaini hali halisi ya utekelezaji wa matakwa ya usalama wa moto. Ufuatiliaji wa mamlaka za mipango-

miji na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi haikufanywa kwa kutumia viashiria vya utendaji.

Matokeo yake, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa ulizingatia changamoto badala ya kiwango cha utekelezaji wa mipango kabambe ulioidhinishwa na malengo mengine yaliyowekwa. Hata ufuatiliaji ulipofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, hakuna mrejesho uliotolewa kwa mamlaka za mipango-miji.

Hii inamaanisha kuwa mamlaka za mipango-miji hazipati mapendekezo kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhusiana na utendaji wao.

Ufuatiliaji uliofanywa na mamlaka za mipango-miji ulifanyika kwa kusudi maalumu kwa sababu hakukuwa na mpango wowote ulioandaliwa na kuingizwa kwenye mfumo wa matumizi wa mamlaka za mipango-miji husika. Katika baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa, ufuatiliaji wa shughuli za upangaji mji zilizotekelezwa ulifanywa na wapima-ardhi ambao waliingizwa kwa majaribio wakati wa mradi unaazishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi.

Vilevile, hakukuwa na tathmini iliyofanyika ya utekelezaji wa mpango kabambe katika ngazi za serikali kuu na serikali za mitaa. Cha kushagaza, miji ilikuwa ikipanuka na kuendelezwa kiholela.

## SURA YA SABA

## MAPENDEKEZO

### 7.1 Utangulizi

Mahitimisho yaliyotokana na uchambuzi uliofanywa kutoka katika ripoti kumi za ukaguzi wa ufanisi umeonesha kwamba kuna udhaifu katika maeneo yote matatu ambayo ni usalama katika makazi ya watu, sekta ya chakula, na uchukuzi. Kwa hiyo, sura hii inatoa mapendekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kulingana na mahitimisho yaliyotolewa kuhusiana na kinachofanyika ili kukabiliana na udhaifu uliobainishwa. Lengo likiwa ni kuboresha mipango na utekelezaji wake, usajili, ukaguzi, uratibu, utoaji taarifa, mawasiliano, na ufuatiliaji na tathmini ya masuala ya usalama nchini.

### 7.2 Mapendekezo ya Kuberesha Usalama katika Sekta ya Usafirishaji

Ofisi ya Waziri Mkuu inapaswa kuhakikisha kwamba Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano; Wizara ya Mambo ya Ndani; Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini, Wakala wa Barabara Tanzania; na Jeshi la Polisi Tanzania:

1. Wanatumia mbinu ya ukaguzi yenye kuzingatia viashiria vya hatari katika kuandaa na kufanya ukaguzi wa usalama ili kukabiliana na mambo muhimu ya hatari ambayo huchangia zaidi ajali kwa watumiaji wa usafiri wa barabarani na majini;

2. Wanatengeneza mfumo madhubuti wa ufuatiliaji ili kupima maendeleo yaliyofanywa na watumiaji mbalimbali wa usafiri wa majini na barabarani katika kutekeleza na kutii matakwa ya usalama kwa kuwianisha na mikakati inayotumika kusimamia usalama;

3. Waimarishe mifumo ya uratibu hasa katika eneo la kubadilishana taarifa za ajali baina ya wadau muhimu katika sekta ya usafiri.

### 7.3 Mapendekezo ya Kuboresha Udhibiti wa Usalama wa Chakula Nchini

Ofisi ya Waziri Mkuu inapaswa kuhakikisha kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Viwanda, Biashara, na Uwekezaji; na Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na wakala ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa; na Shirka la Viwango Tanzania:

1. Wanaanzisha utaratibu utakaowezesha ukaguzi wa mara kwa mara wa viwanda vya uchakataji na usindikaji wa chakula na sehemu za kuingizia chakula kutoka nje ili kuhakikisha kwamba wazalishaji wa chakula, wamiliki wa viwanda vya usindikaji wa chakula, na

waagizaji wa chakula wanafuata sheria, kanuni, na viwango vya usalama wa chakula;

2. Wanaanzisha mfumo wa utaratibu utakaohakikisha ufanisi katika uratibu wa wadau wote muhimu wanaohusika na kuimarisha usalama wa chakula katika uandaaji na utekelezaji wa mipango, mikakati, na katika kubadilishana taarifa kuhusu usalama wa chakula;

3. Wanatengeneza vigezo vya kupima utendaji katika ufuatiliaji na ufanyaji tathmini ya maendeleo ya taasisi za serikali kuu na mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika na utekelezaji wa shughuli za usalama wa chakula ikiwemo usindikaji wa chakula, machinjio, usafirishaji, na katika milango ya mipaka ya kuingizia chakula kutoka nje;

4. Wanaandaa mfumo wa kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali ikiwemo nguvukazi, vifaa, na fedha za kutosha kushughulikia utekelezaji wa matakwa ya usalama wa chakula.

### 7.4 Mapandekezo ya Kuboresha Usalama katika Makazi ya Watu

Ofisi ya Waziri Mkuu inapaswa kuhakikisha kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Mambo ya Ndani; Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji; Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Ofisi ya Makamu wa Rais - Kurugenzi ya Mazingira, na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira:

1. Wanaanzisha mfumo na utaratibu utakaohakikisha ufanisi katika uratibu wa wadau wote muhimu wanaohusika na kuimarisha usalama wa katika makazi ya watu katika uandaaji na utekelezaji wa mipango na mikakati, na katika kubadilishana taarifa kuhusu usalama wa makazi nchini;

2. Wanabuni vigezo vya kupima utendaji katika ufuatiliaji na ufanyaji tathmini ya maendeleo ya taasisi za serikali kuu na mamlaka za serikali mitaa zinazohusika na utekelezaji wa shughuli za usalama wa makazi.

## MAREJELEO


1. Agarwal, P.K., Jain, V., & Bhawar, U. (2013). *"Development of a hierarchical structure to identify critical maintenance components affecting road safety. Procedia-Social and Behavioural Sciences, 104, 292-301"*.
2. Controller and Auditor General (2014). "*Performance Audit on the Management of Food Inspection*". The National Audit Office of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
3. Controller and Auditor General (2016). "*Performance Audit on the Management of Urban Planning In Tanzania*". The National Audit Office of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
4. Controller and Auditor General (2017). "*Follow-Up Report On The Implementation Of The Controller And Auditor General's Recommendations For The Five Performance Audit Reports Issued And Tabled To Parliament Between 2012 And 2013*"
5. Controller and Auditor General (2017). "*Performance Audit on the Enforcement of Fire Safety in Public Buildings*". The National Audit Office of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
6. Controller and Auditor General (2017). "*Performance Audit on The Enforcement Of Development Control For The Planned Public Open Spaces In Tanzania*". The National Audit Office of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
7. Controller and Auditor General. (2014). "*Performance Audit on the Management Inspection of Imported Goods in Tanzania*". The National Audit Office of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
8. Controller and Auditor General. (2016). "*On the Management of Environmental Impact Assessment Process in Development Projects*". The National Audit Office of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania
9. Controller and Auditor General. (2016). "*Performance Audit on the Hygiene Control in Meat Production Process*". The National Audit Office of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
10. Controller and Auditor General. (2017). "*Performance Audit Report on Management of Roads Furniture*". The National Audit Office of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
11. Controller and Auditor General. (2017). "*Performance Audit Report on the Management of Surveys and Inspection of vessels in Marine Transportation*". The National Audit Office of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
12. Kikwasi G., "Case study Mlimani City and Quality Centre in Dar es Salaam by J (2015). "*A Study on the Awareness of Fire Safety Measures for Users and Staff of Shopping Malls*".
13. Kyessi, S.A., Misigaro A. & Shoo, J. "*Formalization of Land Property Rights In Unplanned Settlements*".
14. *United Republic of Tanzania (2000). "National Human Settlements Development Policy"*.

15. United Republic of Tanzania (2009). *“Ministry of Infrastructure Development; A guide to road safety Auditing”.*
16. United Republic of Tanzania (2009). “*National Urban Profile Tanzania*
17. World Health Organization. (2013). *“Global status report on road safety 2013: supporting a decade of action”*. World Health Organization

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Malengo ya Ukaguzi wa Ufanisi Yanayohusiana na Usalama**

| Na. | Jina la Taarifa | Mwaka Ilipochapishwa | Lengo la Ukaguzi | Lengo Mahususi la Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Usimamizi wa Samani za Barabarani | 2017 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kubaini iwapo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano (MoWTC) kupitia Wakala wa Barabara inasimamia kwa ufanisi samani za barabara ambazo ni muhimu kwa usalama barabarani. | a) Kubaini iwapo Wakala wa Barabara unazingatia mahitaji ya watumiaji wa barabara wakati wa kupanga mipango ya uwekaji samani za barabarani;<br>b) Kubaini iwapo Wakala wa Barabara unakarabati samani za barabarani;<br>c) Kutathmini iwapo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano inafuatilia na kutathmini kwa ufanisi shughuli za uwekaji samani za barabarani ;<br>d) Kutathmini iwapo kuna uratibu wa ufanyaji kazi kati ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano; na Wakala wa Barabara, na wadau wengine muhimu katika usimamizi wa samani za barabarani. |
| 2. | Ukaguzi wa Vyombo vya Usafiri wa Majini | 2017 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano; na Mamlaka ya Usafiri wa Nchikavu na Majini inasimamia kwa ufanisi ukaguzi wa vyombo vya usafiri ili kuhakikisha usalama katika usafiri wa majini. | a) Kubaini iwapo Mamlaka ya Usafiri wa Nchikavu na Majini inaandaa mipango ya kutosha kwa tafiti na ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa majini;<br>b) Kutathmini iwapo Mamlaka ya Usafiri wa Nchikavu na Majini inatekeleza ipasavyo mipango ya tafiti na ukaguzi wa vyombo;<br>c) Kutathmini iwapo Mamlaka ya Usafiri wa Nchikavu na Majini inahakikisha viwango vya usalama vinafuatwa kupitia tafiti na ukaguzi wa vyombo vya majini;<br>d) Kutathmini jinsi Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano inavyofanya ufuatiliaji na tathmini ya masuala ya usalama katika usafirishaji majini. |

| Na. | Jina la Taarifa | Mwaka Ilipochapishwa | Lengo la Ukaguzi | Lengo Mahususi la Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Ukaguzi wa Usalama Barabarani | 2012 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo ukaguzi wa usalama barabarani unazingatia viashiria vya hatari na udhibiti wa mwendokasi unafanyika kwa ufanisi. | a) Kubaini iwapo usimamizi wa ukaguzi wa usalama barabarani unafanyika kwa ufanisi na kwa kuzingatia viashiria va hatari;<br>b) Kubaini iwapo udhibiti wa mwendokasi unafanyika kwa ufanisi na kwa kuzingatia viashiria va hatari; |
| 4. | Usimamizi wa Ukaguzi wa Uagizaji Bidhaa | 2014 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapunguza bidhaa zenye viwango duni zinazoagizwa nje ya nchi kwa kufanya ukaguzi wa kutosha na wa mara kwa mara. | a) Kutathmini iwapo usimamizi wa ukaguzi wa uagizaji bidhaa za nje unafanywa kwa kuzingatia viashiria vya hatari;<br>b) Kutathmini iwapo Wizara ya Viwanda na Biashara inafanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za ukaguzi wa bidhaa kutoka nje zinazofanywa na Shirika la Viwango Tanzania;<br>c) Kubaini iwapo kuna udhaifu katika ukaguzi wa bidhaa za nje na kujua sababu za kuwepo kwa udhaifu huo au kutofanyika kabisa kwa ukaguzi husika. |
| 5. | Udhibiti wa Usafi katika Uzalishaji na Uchakataji wa Nyama | 2016 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo Wizara ya Kilimo, Mifugo, na Uvuvi; Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI; na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto zina utaratibu nzuri na wenye ufanisi | Kubaini iwapo:<br>a) Kiwango cha hali ya usafi katika shughuli za uzalishaji wa nyama ili kuhakikisha uzalishaji wa nyama salama kwa umma;<br>b) Wizara ya Kilimo, Mifugo, na Uvuvi; Mamlaka ya Chakula na Dawa; na mamlaka za serikali za mitaa zinafanya ipasavyo na kwa ufanisi shughuli za ukaguzi wa uzalishaji wa nyama; |

| Na. | Jina la Taarifa | Mwaka Ilipochapishwa | Lengo la Ukaguzi | Lengo Mahususi la Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| | | | wa kudhibiti usafi katika mchakato wa uzalishaji na usambazaji wa nyama kwa umma. | c) Kiwango cha ufuatiliaji na tathmini cha utekelezaji wa mifumo ya kudhibiti usafi katika mchakato wa uzalishaji wa nyama uliofanywa na Wizara ya Kilimo, Mifugo, na Uvuvi; Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto. |
| 6. | Usimamizi wa Ukaguzi wa Chakula | 2014 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kubaini iwapo Mamlaka ya Chakula na Dawa inatimiza malengo yake ya udhibiti wa usalama na ubora wa chakula nchini kwa kuendesha na kusimamia ukaguzi wa chakula. | Kubaini iwapo:<br>a) Mamlaka ya Chakula na Dawa ina mipango inayozingatia viashiria vya hatari katika ukaguzi na ufuatiliaji wa viwanda vya usindikaji wa chakula na sehemu za kuingizia chakula mipakani na inagawanya rasilimali ilizonazo katika maeneo yenye hatari kubwa ya usalama wa chakula;<br>b) Mamlaka ya Chakula na Dawa inafanya kaguzi zinazozingatia viashiria vya hatari katika kaguzi za viwanda vya usindikaji wa chakula na sehemu za kuingizia chakula mipakani ili kupunguza uingizaji wa chakula kisicho salama katika soko na kulinda afya ya watumiaji; na<br>c) Mamlaka ya Chakula na Dawa inafanya ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ya ukaguzi wa chakula na kutumia taarifa zinazopatikana katika kaguzi hizo ili kuboresha mwenendo wa ukaguzi. |

| Na. | Jina la Taarifa | Mwaka Ilipochapishwa | Lengo la Ukaguzi | Lengo Mahususi la Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| 7. | Usimamizi wa Usalama dhidi ya Majanga ya Moto katika Majengo ya Umma | 2017 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo Wizara ya Mambo ya Ndani (MoHA) kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linasimamia matakwa ya usalama dhidi ya moto katika majengo ya umma. | Kutathmini:<br>a) Ukaguzi unaofanywa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwenye majengo ya umma dhidi ya hatari ya moto;<br>b) Ufuatiliaji wa Vikosi vya Zimamoto ili kuhakikisha ubora wa shughuli zao;<br>c) Mchakato wa kupitisha michoro ya ujenzi inayofanywa na mamlaka za serikali za mitaa;<br>d) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizofanywa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji,<br>e) Adhabu zinazotolewa kwa wakiukaji wa sheria za usalama dhidi ya moto. |
| 8. | Tathmini za athari za mazingira katika maendeleo ya miradi | 2016 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lilisimamia ipasavyo mchakato wa tathmini za athari za mazingira kabla ya utekelezaji ya miradi ya maendeleo. | Kutathmini iwapo:<br>a) Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira linajipanga ipasavyo kwa shughuli za tathmini za athari mazingira;<br>b) Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira linasajili na linachunguza miradi ili kubaini iwapo tathmini za athari za mazingira zifanyike au zisifanyike;<br>c) Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira linapitia tathmini za athari za mazingira ili kubaini iwapo zilizofanyika ipasavyo;<br>d) Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu mchakato wa kufanya tathmini za athari za mazingira. |

| Na. | Jina la Taarifa | Mwaka Ilipochapishwa | Lengo la Ukaguzi | Lengo Mahususi la Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| 9. | Usimamizi wa mipango-miji | 2015 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo Wizara ya Ardhi, Nyumba,na Maendeleo ya Makazi, na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zilisimamia makazi mijini kupitia mifumo na taratibu za mipango-miji nchini Tanzania. | Kutathmini iwapo:<br>a) Mamlaka za mipangi-miji zinaandaa na kutumia mipango husika katika kutoa miongozo ya uendelezaji wa makazi mijini;<br>b) Mikakati ya mipango-miji iliyoandaliwa na mamlaka za mipango inatatua matatizo yaliyopo katika mifumo ya endelezaji wa miji nchini;<br>c) Wizara ya Ardhi, Makazi, na Maendeleo ya Makazi; na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zinatekeleza mipango ya uendelaji wa miji iliyopo;<br>d) Wizara ya Ardhi, Makazi, na Maendeleo ya Makazi; na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zilifuatilia na kutathmini shughuli za mipango-miji. |
| 10 | Udhibiti wa Maeneo ya Wazi | 2017 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kupitia mamlaka zake za mipango inatekeleza kwa ufanisi Udhibiti wa Uendelezaji wa Maeneo ya Wazi ya Umma yaliyopangwa. | Kutathmini iwapo:<br>a) Mamlaka za mipango zinaandaa mipango na mikakati ili kuhakikisha maeneo ya wazi ya umma yanalindwa na kutunzwa;<br>b) Mamlaka za mipango zinatekeleza kwa ufanisi usimamizi wa mipango ya udhibiti wa uendelezaji katikaa maeneo ya wazi ya umma;<br>c) Ufanisi wa mfumo ya utoaji taarifa za wavamizi wa maeneo ya wazi ya umma na hatua zinazochukuliwa dhidi yao. |
| 11. | Mamlaka ya Udhibiti wa Usalama na | 2013 | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo usalama na afya mahali pa kizi, | Kutathmini iwapo: |

| Na. | Jina la Taarifa | Mwaka Ilipochapishwa | Lengo la Ukaguzi | Lengo Mahususi la Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| | Afya Mahali pa Kazi | | usajili, ukaguzi wa mahali pa kazi, na rasilimali zilizopo zinasimamiwa kwa ufanisi. | a) Mamlaka ya Udhibiti wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi inasimamia ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi kwa ufanisi;<br>b) Mamlaka ya Udhibiti wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi inatumia rasilimali zake kwa ufanisi;<br>c) Mamlaka zinazohusika zinahakikisha kuwa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi inafanywa kwa ufanisi. |
| 12 | Usimamizi wa Mifumo ya Udhibiti wa Mazingira katika Sekta ya Madini | | Lengo la jumla la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Mkurugenzi wa Mazingira na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lina michakato inayofaa ya kuhakikisha kuna sera, sheria, na kanuni za mazingira zinazohusiana na shughuli za utafutaji wa mafuta nchini na iwapo michakato na taratibu zilizopo zinatekelezwa. | a) Kubaini iwapo Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Mkurugenzi wa Mazingira na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira lina mipango inayozingatia viashiria vya hatari ili kupunguza athari za mazingira zinazosababishwa na shughuli za utafutaji wa mafuta;<br>b) Kutathmini iwapo Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira linachunguza, linatoa taarifa, linaadhibu wavunja sheria, au linafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mfumo wa udhibiti wa mazingira katika maeneo yenye shughuli za utafutaji wa mafuta;<br>c) Kutathmini iwapo Mkurugenzi wa Mazingira na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira linaratibu vyema wizara za kisekta, mashirika, idara, na taasisi zingine za serikali katika masuala ya uhifadhi wa mazingira; |

| Na. | Jina la Taarifa | Mwaka Ilipochapishwa | Lengo la Ukaguzi | Lengo Mahususi la Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| | | | | d) Kutathmini iwapo Mkurugenzi wa Mazingira anatathmini utendaji wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na pia jinsi Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira linavyoangalia utendaji wake katika kuhakikisha sheria za mazingira zinafuatwa katika shughuli za utafutaji wa mafuta nchini. |

**Kiambatisho Na. 2: Uchambuzi wa Mawanda na Maeneo Yaliyochaguliwa kwa Kaguzi za Ufanisi katika Eneo la Usalama**

| Na. | Jina la Taarifa | Wakaguliwa | Shughuli Zilizokaguliwa | Kipindi Ukaguzi Ulipofanyika | Maeneo Yaliyochaguliwa wakati wa Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Usimamizi wa Samani za Barabarani | **1.** Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano<br>**2.** Wakala wa Barabara | **1.** Uwekaji wa samani za barabarani (ishara na alama za barabarani)<br>**2.** Matengenezo ya samani za barabarani, ufuatiliaji wa samani za barabarani, na uratibu kati ya watendaji muhimu na wadau. | Miaka mitano ya fedha kunzia 2011/2012 hadi 2015/2016 | Barabara zilizochaguliwa zina urefu wa kilomita 1,395 ambazo ni sawa na asilimia 4 ya kilomita 33,287 za barabara za kitaifa (barabara za kitaifa na mkoa). Kutokana na usawa wa mtandao wa barabara Tanzania, sampuli hii iliyochaguliwa inawakilisha jumla ya idadi ya barabara nchini.<br>Barabara nane (8) zilichaguliwa kinasibu kutoka kwenye mtandao wa barabara kwa kuzingatia uwakilishi wa kijiografia na hali ya barabara, yaani barabara za zamani na zilizojengwa hivi karibuni. Ukaguzi ulihusisha mtandao wa barabara za lami pekee. |
| 2. | Ukaguzi wa Vyombo vya Usafiri wa Majini | 1. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano<br>2. Mamlaka ya Usafiri wa | 1. Kupanga utekelezaji wa mipango<br>2. Utekelezaji wa viwango vya usalama<br>3. Ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi | Miaka mitano ya fedha kuanzia 2011/2012 hadi 2015/2016 | Mikoa mitatu yaani Dar es Salaam, Mwanza, na Tanga ilihusika. Mikoa hii ilipewa kipaumbele kwa sababu ina shughuli nyingi za usafiri wa majini, na shughuli nyingi za utafiti na ukaguzi. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Nchikavu na Majini | wa vyombo vya usafiri wa majini | | |
| 3. | Ukaguzi wa Usalama Barabarani | 1. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano<br>2. Jeshi la Polisi Tanzania | 1. Swali la kwanza la ukaguzi linalenga kubaini iwapo usimamizi wa usalama barabarani unaofanywa na jeshi la polisi unazingatia viashiria vya hatari.<br>2. Mipaka ya mwendokasi inarekebishwa kulingana na ubora, hali na ajali za barabarani | Miaka minne kuanzia Januari 2007 hadi Desemba 2010 | Taarifa zilikusanywa kutoka mikoa tisa (9) kati ya 21 Tanzania Bara. Barabara sita za mikoa na wilaya zilijumuishwa pamoja na pamoja na magari ya abiria na ya mizigo. Mikoa tisa iliyochaguliwa inajumuisha mikoa mitano yenye viwango vya juu vya ajali wakati mikoa minne iliyobaki ilikuwa na viwango vya chini vya ajali za barabrani. |
| 4. | Usimamizi wa Ukaguzi wa Uagizaji Bidhaa | 1. Shirika la Viwango Tanzania<br>2. Wizara ya Viwanda na Biashara | 1. Ukaguzi huu ulilenga sehemu zilizopo mipakani.<br>2. Ukaguzi ulizingatia ukaguzi wa kawaida wa bidhaa zinazoagizwa nchini. Masuala kama vile mipango, miongozo, uratibu, utoaji wa | Miaka mitatu ya fedha kuanzia 2010/11 hadi 2012/13 | Milango minne ya mipaka, Bandari za Nchikavu kumi, na Mamlaka ya Mapato Tanzania<br><br>Uteuzi wa milango ya mipaka na bandari za nchikavu ulizingatia ukubwa wa bandari na bandari za nchikavu zinazotumika kuingizia bidhaa za aina mbalimbali, aina za shehena zilizoingizwa nchini, nchi zinakotokea shehena, na njia za usafirishaji zilizotumika. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | vipaumbele katika ukaguzi, ufanyaji wa kaguzi, utoaji wa taarifa za shughuli za ukaguzi, na utoaji wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya matokeo ya ukaguzi wa bidhaa toka nje.<br><br>3. Masuala mengine yaliyojumuishwa katika ukaguzi yalikuwa ni utekelezaji wa viwango vya usalama wa bidhaa, utekelezaji wa matakwa ya sheria kama vile adhabu, na kampeni za uhamasishaji kwa umma kwa ujumla kuhusu ubora wa bidhaa zinazoagizwa | | |
| 5. | Udhibiti wa Usafi katika Uzalishaji na | **1.** Wizara ya Mifugo na Uvuvi | **1.** Ukaguzi ulijikita katika kuonesha kiwango cha | Miaka mitano ya fedha kuanzia 2010/11 hadi 2014/15 | • Mamlaka saba za serikali za mitaa ziliteuliwa kwa kuzingatia uwepo wa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Uchakataji wa Nyama | **2.** Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI<br><br>**3.** Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto | uzalishaji wa nyama katika mazingira ya usafi, na shughuli za ukaguzi katika uzalishaji na usafirishaji wa nyama.<br><br>**2.** Ukaguzi pia uliangazia shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya utaratibu wa udhibiti wa usafi katika uzalishaji wa nyama uliofanywa na wizara na mamlaka za serikali za mitaa. | | machinjio, uwakilishi wa kijiografia, na idadi ya wanyama waliochinjwa.<br><br>• Ofisi mbili za kanda (Kanda ya Ziwa na Kanda ya Nyanda za Juu-Kusini) kati ya ofisi tano za kanda za Mamlaka ya Chakula na Dawa zilijumuishwa katika ukaguzi huu. Pia, ofisi tatu za kanda (Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa, na Kusini-Magharibi) kati ya ofisi nane za kanda za Idara ya Mifugo zilitembelewa ili kupata taarifa za shughuli za ukaguzi.<br><br>• Machinjio kumi na mbili (12) katika mamlaka za serikali za mitaa yalitembelewa ili kuona hali halisi ya utaratibu wa usafi katika mchakato wa uzalishaji wa nyama.<br><br>• Aina za nyama zinazozalishwa katika machinjio zilikuwa ng'ombe, kuku, mbuzi, na kondoo. |
| 6. | Usimazmizi wa Ukaguzi wa Chakula | 1. Mamlaka ya Chakula na Dawa | **1.** Ndani ya Mamlaka ya Chakula na Dawa, ukaguzi ulijikita katika kuangalia jinsi ukaguzi wa chakula katika viwanda vya | Miaka minne ya fedha kuanzia 2009/10 hadi 2012/13 | Ukaguzi wa chakula unafanywa na ofisi tano za kanda la Mamlaka ya Chakula na Dawa. Ofisi tano za kanda ni Kanda ya Mashariki, Kanda ya Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Kaskazini, na Kanda ya Ziwa. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | usindikaji wa chakula na sehemu za kuingizia chakula mipakani unavyopangwa, kutekelezwa, na jinsi ufatiliaji na tathmini za utekelezaji zinavyofanyika.<br><br>**2.** Mamlaka ya Chakula na Dawa inafanya kaguzi za aina mbalimbali kama uchunguzi, ufuatiliaji, na ukaguzi maalumu na wa kawaida. Hata hivyo, ukaguzi huu wa ufanisi ulilenga ukaguzi wa chakula wa kawaida ambao ndiyo mkubwa na hufanyika mara kwa mara. | | |
| 7. | Usimamizi wa Usalama dhidi ya Majanga ya Moto | **1.** Jeshi la Zimamoto na Uwokoaji | **1.** Utekelezaji wa matakwa ya usalama dhidi ya moto katika majengo ya umma. | **1.** Miaka mitano ya fedha kuanzia 2011/12 hadi 2015/16 | Takwimu zilikusanywa kutoka ofisi tano za moto za kikanda na kwa wadau wengine ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – Idara ya Usimamizi wa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | katika Majengo ya Umma | **2.** Wizara ya Mambo ya Ndani | **2.** Shabaha ya ukaguzi ilikuwa pamoja na uwekazi wa vifaa vya kudhibiti moto, ukaguzi wa mara kwa mara, ufuatiliaji wa vikosi vya zimamoto katika utendaji wao wa shughuli za utekelezaji, kutathmini ya mchakato wa kuidhinisha michoro ya ujenzi, kufanya na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa usalama dhidi ya moto, na utoaji wa adhabu stahiki kwa wakiukaji wa matakwa ya usalama dhidi ya moto. | | Maafa na pia kutoka kwa mamlaka za serikali za mitaa. |
| 8. | Tathmini za Athari za Mazingira katika Maendeleo ya Miradi | 1. Baraza la Taifa la Mazingira | 1. Kupanga shughuli za tathmini ya athari za mazingira | Miaka mitano ya fedha kuanzia 2010/11 hadi 2014/2015 | Timu ya ukaguzi iliteua kinasibu miradi 38 ya maendeleo ambayo imetekelezwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira wakati wa ukaguzi. Miradi hiyo imetekelezwa katika ofisi nne za kanda za |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **2.** Ofisi ya Makamu wa Rais | 2. Usajili wa miradi ya uchunguzi ili kuamua iwapo tathmini ya athari za mazingira itafanyika au la<br><br>3. Kukagua taarifa za tathmini na ukaguzi wa mazingira<br><br>4. Uratibu wa mchakato wa kufanya tathmini ya athari za mazingira | | Baraza la Usimamizi wa Mazingira ambazo ni Mtwara katika Kanda wa Kusini, Mbeya katika Kanda ya Nyanda za Juu-Kusini, Mwanza katika Kanda ya Ziwa, na Arusha katika Kanda ya Kaskazini.<br><br>Miradi hiyo ilihusisha sekta nne kuu ambazo ni maliasili, viwanda, miundombinu, na ujenzi.<br><br>Aidha, halmashauri tano (5) za majiji zilihusishwa, ambazo ni Mbeya, Tanga, Arusha, Mwanza, na Dar es Salaam. Vilevile, manispaa sita (6) na halmashauri moja ya wilaya ziliteuliwa kinasibu. |
| 9. | Usimamizi wa Mipango-miji | **1.** Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Mendeleo ya Makazi<br><br>**2.** Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI | Uandaji mipango na mikakati, na utekelezaji, na ufuatiliaji na tathmini ya mipango | Miaka mitatu kuanzia Julai 2010 hadi Juni 2013 | **1.** Mamlaka saba[16] za serikali za mitaa ziliteuliwa. Uteuzi wa mamlaka za serikali za mitaa ulifanyika kwa kuzingatia makundi manne ya mamlaka za serikali za mitaa nchini Tanzania yaani halmashauri za majiji, manispaa, wilaya, na miji pamoja na uwakilishi wa kijiografia wa nchi. Hata hivyo, uteuzi wa sampuli za halmashauri kwa kutumia sifa hizi ulifanyika kinasibu. |

[16]Halmashauri ya Jiji la Dares Salaam na Mbeya, Manispaa ya Temeke, Halimashauri za Miji ya Babati na Kahama, na Halmashauri za Wilaya za Newala na Kigoma

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **2.** Ukaguzi huu pia ulihusisha Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA) katika Manispaa ya Dodoma kwa sababu ni mamlaka pekee ya kiserikali yenye uwezo wa kushughulikia mipango-miji nchini Tanzania. Kwa hiyo, CDA iliteuliwa kwa madhumuni ya kuanzisha utendaji wake chini ya mamlaka huru. |
| 10. | Udhibiti wa Maeneo ya Wazi | Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI | Utekelezaj wa udhibiti wa uendelezaji kwa ajili ya mipango ya maenao ya wazi ya umma ndani ya mamlaka za mipango-miji.<br><br>Ukaguzi ulilenga zaidi mikakati iliyowekwa, na mipango ya kuhakikisha ulinzi wa maeneo ya wazi yaliyopangwa na utekelezaji wa mipango ya udhibiti wa uendelezaji, na mfumo unaotumiwa wa kutoa taarifa za wavamizi kwa waangalizi pamoja na hatua zilizochukuliwa dhidi ya wavamizi hao. | Miaka mitano ya fedha kuanzia 2011/12 hadi 2015/16 | **1.** Manispaa sita ziliteuliwa kwa kuzingatia uwepo wa idadi ndogo na kubwa ya matukio ya uvamizi wa ardhi na vilevile manispaa zenye idadi kubwa ya watu.<br><br>**2.** Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma iliteuliwa pia ili kuilinganisha kiutendaji na mamlaka zingine za mipango-miji. Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma ilikuwa na wajibu wa kuandaa na kutekeleza mipango wa Dodoma kuwa Mji Mkuu wa Tanzania. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 11. | Mamlaka ya Udhibiti wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi | **1.** Wizara ya Kazi na Ajira<br>**2.** Mamlaka ya Udhibiti wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi | Usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi :<br>**1.** Usajili wa mahali pa kazi<br>**2.** Ukaguzi<br>**3.** Ugawanyaji wa rasilimali<br>**4.** Ufuatiliaji na tathmini | Miaka mitatu kuanzia Julai 2009 hadi Juni 2012 | Taarifa zilikusanywa kutoka mikoa minne (4) kati ya mikoa 24 ya Tanzania Bara. Mikoa minne iliyotembelewa iliteuliwa kutoka katika kanda nne za Mamlaka ya Udhibiti wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (yaani, mkoa mmoja kutoka kila kanda). Uteuzi wa maeneo ulizingatia shughuli za kiuchumi zilizofanywa katika kila mkoa. Pia, maeneo yenye ofisi na viwanda (mahali pa kazi) vingi na vichache zilizingatiwa. |
| 12. | Usimamizi wa Mifumo ya Udhibiti wa Mazingira katika Sekta ya Madini | 1. Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na<br>2. Ofisi ya Makamu wa Rais - Kurugenzi ya Mazingira | Sehemu zilizokaguliwa ni pamoja na mfumo wa uandaaji, utelezaji wa mipango, uratibu, ufatiliaji na tathmini ya shughuli za mazingira katika sekta ya mafuta | Miaka mitano ya fedha kuanzia 2010/11 hadi 2014/15 | Ukaguzi ulifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, na Kigoma. Ukaguzi ulizingatia zaidi shughuli zinazofanyika katika maeneo yaliyopo ndani ya maji na yale ya nchikavu. Mkoa wa Mtwara na Lindi ulitembelewa kwa sababu shughuli nyingi zilikuwa zikifanyika majini wakati Kigoma shughuli nyingi zilikuwa zikifanyika nchikavu. |